
# Urithi wa Ulimwengu Kwenye Mikono Michanga



TUJUE, TUHIFADHI NA TUTENDE

## Chombo mufti cha kuelimisha

ASPnet

# Kwa msaada kutoka:

Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Norway (NORAD)

# Hati ya kukataa:

Waandishi ndio wenye jukumu la uteuzi na uwasilishi wa ukweli unaopatikana katika rasilmali hii ya kielimu na maoni yanayoelezwa humu ambayo aghalabu si ya UNESCO na kwa hivyo hawalihusishi shirika hili.

Muundo na uwasilishaji uliotumika katika chapisho hili haudokezi maelezo ya maoni yoyote kabisa ya UNESCO kuhusu hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo, jiji au sehemu au mamlaka yake au kuhusu mipaka ya maeneo yaliyotajwa.

Chapa ya kwanza kwa Kiingereza 1998
Kimetolewa mwaka wa 2002 na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO)
7 Place de Fontenoy
F-75352 Paris 07 SP
France

Tafsiri ya Kiswahili 2004
Kimepigwa chapa na UNON, Kenya

© UNESCO 2004
ISBN 92-3-103843-5

# Dibaji

## NA MKURUGENZI MKUU WA UNESCO



### Kwa heshima ya waalimu: waanzilishi wa Elimu ya Urithi wa Ulimwengu

Katika karne zilizopita urithi wetu mwingi umepotea kabisa bila tamaa ya kupatika tena. Tumeshuhudia na tunazidi kushuhudia uharibifu na kuchakaa kwa hazina adimu kutokana na maafa ya kiasilia, vita, umaskini, ujenzi wa viwanda na uchafuzi wa mazingira. Sababu zingine zinazochochea janga hili la muda mrefu ni ujinga, kutojali na kutothamini.

Kwa kupitisha *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* (ya 1972), jumuiya ya ulimwengu ilijitolea kuzuia kutoweka kwa urithi wetu adimu wa kiasilia na kitamaduni. Tangu kupitishwa kwa *Mapatano* hayo, maeneo 754 katika mataifa zaidi ya 129 kote ulimwenguni yameandikwa katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Kila mwaka orodha hii huongezeka. Kila eneo lina thamani kuu na ni sehemu halisi na adimu ya ustarabu wa kiulimwengu. Kila eneo ambalo linahatarishwa au kuangamizwa ni hasara isiyoweza kubatilishwa kwa binadamu wote.

Hali ya baadaye ya urithi uliobakia itategemea maamuzi na vitendo vya kizazi cha sasa cha watu wachanga ambao hivi karibuni watakuwa viongozi na waamuzi wa siku za usoni.

Kulingana na kifungu cha 27 cha *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* kinachoarifu kuwa 'Mataifa ambayo yanahusika katika *Mapatano* haya yatajitahidi kwa njia mwafaka na hasa kwa njia za kielimu na utaratibu wa kimatangazo, kutilia nguvu kupendezwa na kuheshimiwa kwa urithi wa kitamaduni na kiasilia na watu wanaohusika'. Makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu yalianzisha katika mwaka wa 1994 mradi wa Urithi wa Ulimwengu Katika Mikono Michanga, kupitia kwa Mradi wa Shirikisho la Mashule (ASPnet).

Mradi huu umefaulu katika utoaji, upimaji na utathmini wa kifaa hiki: *Chombo Mufti cha Kuelimisha*. Kwa walimu, kifaa hiki ni silaha muhimu kuwapatia changa moto watu wachanga kuhusu umuhimu wa kuhifadhi urithi wa makazi, mataifa na hata ulimwengu wao. Kifaa hiki pia kitawapatia ustadi unaofaa na kuwawezesha kujitolea daima kwa shughuli hii muhimu.

Walimu wa ASPnet wamejitolea kikamilifu katika ukuzaji wa elimu ya Urithi wa Ulimwengu na kusambaza kifaa hiki na nawatolea heshima maalum. Nawapongeza pia walimu na wataalamu wa urithi kote ulimwenguni kwa michango anzilishi. Ubora wa chapisho hili unatokana na juhudi maalum, ubunifu na mielekeo mipya walioitumia walimu hawa. Pamoja na kuwachochea watu wachanga kupendezwa na kushiriki katika kulinda urithi wa ulimwengu, bidii za walimu hawa zinaimarisha mbinu za ufundishaji katika shule na jamii.



© UNESCO 2004

Elimu ndio msingi wa kujitosheleza, wa maendeleo, wa uhifadhi, wa amani na wa hali njema. Elimu huwapatia motisha watu wachanga kujitolea na kuchukua hatua za kuhifadhi urithi wetu wa kitamaduni na kiasilia (unaonekana na usioweza kuonekana) wa maeneo na wa ulimwengu mzima. Juhudi zao zitafaidi kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Urithi wa Ulimwengu ni dhana inayobadilika. Kamati ya Urithi wa Ulimwengu hukutana kila mwaka kuongezea maeneo mapya katika *Orodha ya Urithi wa Ulimwengu*. Elimu ya Urithi wa Ulimwengu pia ni elimu madhubuti inayohusisha nguzo nne muhimu za elimu katika karne ya ishirini na moja—kujifunza ujue, kujifunza utende, kujifunza ukue kibinafsi, na kujifunza kuishi pamoja na watu. Elimu hii inahusiana na kuboresha elimu kama inavyoelezwa na 'Education for All' Framework for Action iliyokubaliwa na Muungano wa Ulimwengu wa Elimu mjini Dakar nchini Senegal, mwaka wa 2000.

Elimu ya Urithi wa Ulimwengu inatetea kutilia maanani kitambulishi cha binafsi, heshima kwa kila mtu, kushauriana, umoja dhidhi ya tofauti zilizopo, umoja na mwingiliano wa kuridhisha miongoni mwa tamaduni tofauti. Natarajia ya kwamba kifaa hiki cha kielimu kitatumika kwa wingi na walimu kupitia kwa mitalaa yote—walimu wa historia, sayansi, jiografia, sanaa, hesabu, lugha, na masomo na taaluma zingine. Kwa kutumia kifaa hiki, kuendeleza vifaa vipya na kuboresha harakati za ufundishaji, walimu watahamasisha vijana kwa njia ambazo zitawashirikisha binadamu katika mazingira ya kuaminiana, kudhaminiana na umoja.

**Koichiro Matsuura**



UNESCO 2004

# CHOMBO MUFTI CHA KUELIMISHA

## Yaliyomo


| | Ukurasa |
|---|---|
| Utangulizi | 7 |
| *Jinsi ya kutumia* kifaa hiki | 11 |
| Mitazamo ya kielimu ya Urithi wa Ulimwengu | 17 |
| Maafikiano kuhusu Urithi wa Ulimwengu | 39 |
| Urithi wa Ulimwengu na kujitambulisha | 85 |
| Urithi wa Ulimwengu na *utalii* | 103 |
| Urithi wa Ulimwengu na mazingira | 125 |
| Urithi wa Ulimwengu na amani | 147 |
| Marejeleo | 163 |




© UNESCO 2004

# Utangulizi



Havana ya kale na ngome zake. ©Patrimoine. 2001/R Gaillarde.

Karibu kwa toleo la Kiswahili la *Urithi wa Ulimwengu: Chombo Mufti cha Kuelimisha* ambacho kimetayarishwa kama sehemu ya mradi wa UNESCO wa Urithi wa Ulimwengu Katika Mikono Michanga.

Mradi huu ulizinduliwa na Makao ya Urithi wa Ulimwengu ya UNESCO na Mradi wa Shirikisho la Mashule (ASPnet) katika mwaka wa 1994. Mradi huu unalenga kukuza elimu ya kiuvumbuzi ya uhifadhi kwa kuwawezesha wanafunzi kufanya yafuatayo:

✓**Kujifunza** zaidi kuhusu utamaduni na maeneo ya kiasilia yaliyo na thamani yaliyoandikwa katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu;

✓**Kupata** stadi mpya zinazohitajika ili kuhifadhi sehemu hizi ambazo zinalindwa na *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* ya UNESCO ya 1972;

✓**Kukuza** mitazamo mipya na kujitolea daima kuhifadhi utamaduni na maeneo tofauti ya kiasilia ya ulimwengu kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo;

✓**Kuchukua** nafasi muhimu katika ulinzi wa tamaduni na maeneo tofauti ya kiasilia ya ulimwengu kwa kupitia ushirikiano wa kimataifa.

Mradi huu unalenga kuwahusisha wanafunzi katika elimu ya urithi na uhifadhi katika shule zao, maeneo ya kwao na sehemu za urithi wa kitaifa. Haya yatatekelezwa kupitia kwa mtazamo wa taaluma mbali mbali, kwa ushirikiano na makavazi, wasimamizi wa maeneo ya uhifadhi na jamii za maeneo mbali mbali.

Ili kutangaliza dhana hii mpya ya elimu ya Urithi wa Ulimwengu darasani na hata kwengineko, hiki *Chombo Mufti cha Kuelimisha* kilitayarishiwa na UNESCO katika mwaka wa 1999 kwa Kiingereza, kwa msaada wa Wakfu wa Rhone-Poulenc ya Taasisi ya Ufaransa pamoja na Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Norway (NORAD). Kifaa hiki kilibuniwa kutokana na maoni ya wanafunzi na walimu kutoka zaidi ya mataifa 130 ambao wamechangia katika kuendeleza harakati mpya za kielimu za watu wachanga na kushiriki katika baadhi ya mikutano ya kimaeneo na ya kimataifa ya Urithi wa Ulimwengu iliyotayarishwa na UNESCO huko Norway (1995), Kroatia (1996), Zimbabwe (1996), Uchina (1997), Japan (1998), Senegal (1999), Moroko (1999), Australia (2000), Peru (2001) na Uswidi (2001).

Toleo la kwanza la kifaa hiki lilichapishwa kwa Kiarabu, Kichina, Kiingereza, Kifini, Kifaransa, Ki-indoneshia, Kijapani, Kilao, Kirusi, Kihispania, Ki-uzbek na Ki-vietnam na kimefanyiwa majaribio



© UNESCO 2004

na *walimu wa ASPnet na wanafunzi* wa shule zinazoshirikiana na UNESCO katika zaidi ya mataifa 130. Kifaa hiki pia kinaweza kurejelewa kwenye tovuti (web SITE) ya Elimu ya Urithi wa Ulimwengu: www.unesco.org/whc/education
Kupitia kwa *upangaji wa kozi za kufunza* walimu katika sehemu nyingi za ulimwengu, mikakati ya kimaeneo na ya kitaifa kuwahusisha watu wachanga katika elimu ya Urithi wa Ulimwengu na harakati za kushiriki zimekuzwa ili kusaidia mataifa katika dhana hii mpya ya kielimu.

Si rahisi kuandaa vifaa vya kielimu vinavyoweza kutumiwa sawa katika masomo tofauti na walimu wa shule za sekondari kote ulimwenguni. Kifaa hiki kilitayarishwa kwa umakini na kutilia maanani mitazamo ya *kielimu* na *harakati zilizoendelezwa* na walimu wa nchi kadhaa. Watayarishi pia walizingatia ushauri na mapendekezo ya wanafunzi na walimu kote ulimwenguni. Hata hivyo, ni wazi kuwa kifaa hiki lazima kizingatie hali za maeneo na mataifa husika.

Wanafunzi na walimu waliotumiya toleo la kwanza wametoa maoni muhimu ambayo yametumika kuboresha toleo linalochapishwa kwa mara ya kwanza kwa Kiswahili. Hata hivyo, kutokana na utathmini uliofanywa hitimisho muhimu *ni ya kuwa kifaa hiki ni* zana muhimu ya kutayarisha harakati za kieneo na kitaifa. Washiriki wengi ulimwenguni wamekiomba kifaa hiki, na UNESCO imeajibika kuchapisha toleo hili la Kiswahili baada ya kuliboresha na kuhakikisha halitofautiani sana na toleo la kwanza lililoandikwa kwa Kiingereza.

Walimu, wataalamu wa urithi na wakuza mitaala ulimwenguni waliyohusika katika majaribio na kutoa maoni yao juu ya dhana hii mpya ya kielimu wamesaidia ukuzaji *zaidi wa vifaa vya kieneo* na kitaifa vya kuendeleza elimu ya Urithi wa Ulimwengu. Kwa mfano, chini ya usimamizi wa Tume za Kitaifa za UNESCO, kifaa hiki kinatafsiriwa katika zaidi ya lugha 22 za kitaifa. Kifaa hiki kilitafsiriwa mwaka wa 2004 kutumika eneo la Pasifiki. Huko Marekani ya *Kusini kamati* za kitaifa za elimu ya Urithi wa Ulimwengu zinachunguza njia za kudhibiti harakati za kimaeneo na za kitaifa.

Ukuzaji wa mitaala ni utaratibu unaoendelea wenye malengo ya mbali na unahitaji utafiti, utahini *na utathmini*. Enzi tuliyopo ya milenia mpya ni ya kuanzisha dhana mpya ya kielimu tukiwa na matumaini mapya na matarajio ya ulimwengu wenye amani na afya ambapo watu wote watapambana pamoja kuhifadhi urithi adimu wa ulimwengu sasa na katika siku za usoni.



## Wahariri kutoka UNESCO

| Elizabeth Khawajkie | Breda Pavlic | Sarah Titchen |
| --- | --- | --- |
| Elizabeth Khawajkie | Breda Pavlic | Sarah M Titchen |

© UNESCO 2004

# Nembo ya Urithi wa Ulimwengu na Patrimonito

*Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* huunganisha pamoja uhifadhi wa utamaduni na wa rasilmali asilia kama yanavyoashiriwa katika nembo ya Urithi wa Ulimwengu.

Nembo hii inaashiria kutegemeana kwa utamaduni na maeneo asilia: sehemu ya miraba iliyo katikati ni umbo lililobuniwa na watu na mviringo unawasilisha uasilia, mambo haya mawili yameungana kidhabiti. Nembo ni ya mviringo kama ulimwengu, lakini wakati huo huo ni ishara ya ulinzi.



Patrimonito ni 'mtu' aliyebuniwa na kundi la wanafunzi wanaofahamu Kihispania waliotaka kujitambulisha naye wakati wa warsha ya kwanza ya Muungano wa Vijana Wanaohusika na Urithi huko Bergen, Norway, mwaka wa 1995. Patrimonito inamaanisha 'mlinzi mdogo wa urithi ' katika Kihispania na kielelezo hiki kinawakilisha msaidizi mdogo katika harakati za ulinzi wa urithi.




*Patrimonito anawaaga watu wachanga katika Muungano wa kwanza wa Vijana Wanaohusika na Urithi wa Ulimwengu, Zimbabwe. © UNESCO.*



© UNESCO 2004

# Jinsi ya kutumia kifaa hiki cha elimu

## Kifaa hiki kimetayarishiwa walimu wa shule za sekondari:

✓wanaofundisha sehemu mbali mbali za ulimwengu zilizo na hali tofauti huku wengine wakifundisha katika hali ngumu (kama vile mazingira duni, ukosefu wa vifaa vya kufundisha, kuwa na wanafunzi wengi kupindukia madarasani, mitalaa yenye mambo mengi) na baadhi ambao wako kwenye shule zilizo vifaa vya kisasa vya teknolojia ya elimu (kama vile, nafasi ya kutumia mdahalishi (Internet), n.k)

✓ katika masomo mengi kama vile jiografia, historia, lugha, sayansi, hesabu, sanaa, na mengineyo

✓ kuwafundisha wanafunzi wenye miaka 12 hadi 18



## Kifaa hiki kimetayarishwa kama 'sanduku la vifaa vya kikazi' ambapo:

✓unaweza kuchagua vifaa utakavyotumia darasani au nje ya darasa wakati wowote

✓utaanzia sehemu ya mwanzo ya kifaa hiki na kusoma kuhusu mitazamo ya kielimu iliyopendekezwa


✓ unaweza kuchagua mada mojawapo: *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu,* Urithi wa Ulimwengu na kujitambulisha, Urithi wa Ulimwengu na mazingira, Urithi wa Ulimwengu na amani

✓utachunguza malighafi yaliyomo kwenye kifaa hiki kama vile *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu,* Ramani ya Urithi wa Ulimwengu, picha zilizotayarishwa kwa njia maalum

✓utaongeza malighafi yako mwenyewe, kama vile habari iliyotayarishwa na nchi yako kuhusu maeneo ya Urithi wa Ulimwengu, shughuli zinazoendelea za kuhifadhi urithi katika nchi yako na kwengineko, picha, ramani au malighafi ambayo wewe au wanafunzi wako au nyote pamoja mumetayarisha

© UNESCO 2004

**Ili kurahisisha matumizi ya kifaa hiki ishara kadha zimehusishwa:**



Ishara hii ikitumika pembeni, inaonyesha haja ya kurejelea sehemu zingine za kifaa hiki.

Maneno yaliyoandikwa **kwa mkazo** yameelezwa katika Istihali iliyo katika sehemu ya Marejeleo.



Anwani

Anwani zimeonyeshwa kwenye sehemu ya mwisho ya kifaa hiki unapotaka kuwasiliana na mashirika mbali mbali ili upate habari zilizohifadhiwa kuhusu Urithi wa Ulimwengu.



Orodha ya Marejeleo

Kwa sababu ni vigumu kuorodhesha habari zote zinazohusiana na Urithi wa Ulimwengu katika sehemu ya Marejeleo, kuna Orodha ya Marejeleo ambayo unaweza kuagiza bila malipo au kwa kuinunua.



© UNESCO 2004



Harakati za wanafunzi

Chombo hiki kinahusisha **Harakati za Wanafunzi** 42 zilizopendekezwa ambazo zimeonyeshwa kwenye vijisanduku. Harakati hizi zinaweza kurekebishwa, kubadilishwa na kuendelezwa zaidi kutegemea muktadha wa eneo fulani na mahitaji ya wanafunzi wako. Picha zimeandaliwa ili kurahisisha kushiriki kwako katika harakati hizi.

## Aina ya harakati

 Majadiliano

 Utafiti

 Mazoezi

 Kikao cha kutazama

 Ziara za maeneo ya Urithi wa Ulimwengu

 Uigizaji

## Maelezo ya harakati

 Harakati darasani

 Harakati nje ya darasa

 Muda unaopendekezwa

 Masomo yanayopendekezwa

 Vifaa

 Vifaa vingine



© UNESCO 2004

Kifaa hiki kinahusisha **Kurasa za harakati za wanafunzi** ambazo zinaweza kunukulishwa na kusambazwa darasani kwa matumizi ya wanafunzi..



Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu

Inarejelea vifungu mahsusi vya *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* ambayo taarifa yake kamili inapatikana kwenye sehemu ya Marejeleo.



Maelezo kwa ufupi

Inarejelea Maelezo kwa ufupi, hati inayopatikana katika kituo cha UNESCO cha Urithi wa Ulimwengu inayohusisha maelezo ya kila eneo la Urithi wa Ulimwengu ambalo lililoorodheshwa kufikia May 2004, na pia vigezo vinavyo-tambulisha pamoja na tarehe ya kuandikishwa maeneo hayo.



Ramani ya Urithi wa Ulimwengu

Inarejelea *Ramani* ya Urithi wa Ulimwengu inayoorodhesha tarehe ya kuidhinishwa kwa mataifa yote washiriki katika *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* kulingana na majimbo.





Picha

Inarejelea picha 26 za maeneo ya Urithi wa Ulimwengu zinazoonyesha maeneo ya kiasilia na ya kitamaduni (jina na maelezo mafupi, tarehe ya kuorodhesha, na vigezo vilivyo-tumika vya kila eneo vimeelezwa nyuma ya kila picha).

Tunawatakia ufanisi katika shughuli hii mpya inayohitaji kujikakamua inayo-pendekezwa katika kifaa hiki. UNESCO iko tayari kutoa habari au msaada wowote kwenu.

© UNESCO 2004

# Mitazamo ya kielimu ya Urithi wa Ulimwengu



Vijana wanafurahia mchongo wa dragoni wakiwa Forbidden City, Beijing, Uchina, wakati wa Muungano wa Vijana Wanaohusika na Urithi wa Ulimwengu Asia-Pacific. ©UNESCO

**‘Walimu walikubaliana kuwa tatizo kuu lilikuwa kuanzisha na kuhusisha elimu ya Urithi wa Ulimwengu katika viwango vyote vya shule, kwa wanafunzi wote ulimwenguni.’**

**Muungano wa Kiafrika wa Kwanza wa Vijana Wanaohusika na Urithi wa Ulimwengu**

**Victoria Falls, Zimbabwe/Zambia**

# Mitazamo ya kielimu ya Urithi wa Ulimwengu


## Ufundishaji-mseto 18

Harakati za wanafunzi zinazopendekezwa 18
- Majadiliano 18
- Utafiti 19
- Mazoezi 19
- Vikao vya kutazama 19
- Ziara za maeneo ya Urithi wa Ulimwengu 20

*Harakati ya* kwanza ya wanafunzi: Mtihani kuhusu maeneo ya Urithi wa Ulimwengu 20

## Ziara za maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na makavazi 21

Ziara za maeneo 21
- Matayarisho 21
- Ziara tayarishi 21
- Ziara ya eneo 22
- Ziara ya kufuatilia 22

Ukurasa wa harakati za wanafunzi: Ziara ya eneo la Urithi wa Ulimwengu 24

Ziara za makavazi 26
- Hotuba maalum wakati wa ziara ya makavazi 26
- Kuchunguza vifaa vilivyohifadhiwa 26

Ukurasa wa harakati za wanafunzi: *Uchunguzaji wa kifaa cha* makavazi 27
- Ziara za karakana za kiufundi 28

## Uigizaji 28

Uigizaji darasani kupitia tamthilia 28

Kufufua historia kwa uigizaji katika maeneo ya Urithi wa Ulimwengu 29

Utatuzi wa mzozo kwa njia ya amani 30

## Ushurikiano wa ulimwengu na mdaha*lishi* 31


Ushirikiano wa ulimwengu 31

Mdahalishi waunga mkono elimu ya Urithi wa Ulimwengu 32
- Mdahalishi 32
- Barua pepe 32
- Tovuti 32
- Kwa nini tutumie mdahalishi? 33

Urithi wa Ulimwengu na mdahalishi 34

ASPnet kwenye mdahalishi 36

Anwani muhimu kwenye mdahalishi 36



## Ufundishaji-mseto

Uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu una umuhimu mkubwa unaohusiana na kuendelea kustawi kwa sayari yetu. Shughuli hii huandaa fursa za kipekee za kielimu na tena zinazoingiliana kimasomo na zinazohusisha nyanja nyingi za ufundishaji na nafasi za kujifunza.

Mitaala imejaa mambo mengi na shughuli za walimu zinazidi kuongezeka. Wanaohamasisha watu wachanga juu ya umuhimu wa kuhifadhi urithi wa kiulimwengu wameamua kutumia njia ya kuelimisha ya mseto.

Elimu hii ya mseto inayohusisha nyanja tofauti huwawezesha walimu wa masomo tofauti kama vile historia, jiografia, sayansi na lugha, kutanguliza vipengele vya elimu ya Urithi wa Ulimwengu katika ufundishaji. Katika mwisho wa kila sehemu kuu za kifaa hiki, mitazamo ya ufundishaji kupitia kwa nyanja zingine inapendekezwa. Si mitazamo yote itakuwa mwafaka kwa wanafunzi wako, lakini unaweza kuibadilisha ili iwe ya manufaa kwa hali yako na ile ya mitaala.

Elimu ya Urithi wa Ulimwengu huwahimiza walimu wa nyanja mbali mbali kufanya kazi katika makundi ili wawahimize wanafunzi na kuwapatia ilhamu ya kujua, kuhifadhi kwa dhati na kuchukua hatua za kupendelea uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu.



## ▲ Harakati za wanafunzi zinazopendekezwa

Harakati za wanafunzi zinazopendekezwa katika kifaa hiki zimebuniwa kurahisisha njia ya ufundishaji wa mseto unaopendekezwa. Harakati hizi kwa kiasi zimevumbuliwa, kutahiniwa na kukadiriwa na baadhi ya walimu waliochaguliwa kutoka sehemu mbali mbali za ulimwengu ambao tangu mwanzo wamehusika na Mradi wa Elimu ya Watu Wachanga Wanaohusika na Urithi wa Ulimwengu wa UNESCO. Mbinu zilizopendekezwa zinaweza kubadilishwa na kutumika katika kila nchi ili kukabiliana na mahitaji na mifumo tofauti ya elimu. Hatimaye, lengo kuu la mbinu zilizopendekezwa za ufundishaji ni kuwavutia na kujitolea kwa watu wachanga katika shughuli za uhifadhi na kujaribu kupunguza mpaka baina ya shule na jamii kwa kuandaa harakati za kusisimua ambazo zinakuza hali ya kujihusisha na harakati za kijamii.

Harakati za wanafunzi zinazopendekezwa zinamulika maeneo sita ya harakati:

- Majadiliano
- Utafiti
- Mazoezi
- Vikao vya kutazama
- Ziara za maeneo ya Urithi wa Ulimwengu
- Uigizaji

## Majadiliano

Elimu ya Urithi wa Ulimwengu huwawezesha watu wachanga kutafakari na kujadiliana juu ya maana na thamani ya urithi, mbinu zinazohitajika za kusimamia

© UNESCO 2004

Urithi wa Ulimwengu, faida na tisho la utalii wa halaiki katika maeneo ya Urithi wa Ulimwengu, na kadhalika. Kwa kuwa elimu hii inahusisha kujipatia maarifa na ujuzi, vikao vya majadiliano ni muhimu kwa kuwafahamisha wanafunzi kuhusu uhifadhi na kuwahimiza wajihusishe na ulinzi wa uridhi kwa vitendo.



*Mwanafunzi wa Slovenia anagawana na washiriki wa Muungano wa Vijana huko Dubrovnik peremende, ambazo ni sehemu ya urithi wa Kislovenia © UNESCO*

# Utafiti

Maendeleo ya sayansi na teknolojia yameziwezesha baadhi ya jamii kupitia mabadiliko makubwa ya usambazaji wa habari. Idadi kubwa ya shule tayari zimeshapata au zitapata baadaye hifadhi ya habari nyingi, matokeo ya utafiti, muhtasari wa takwimu aidha kwenye maktaba au kupitia mdahalishi. Elimu ya Urithi wa Ulimwengu inawatangulizia wanafunzi mbinu za kimsingi za utafiti kama vile kutafuta na kuchambua habari, kufikia maamuzi na kutoa mapaendekezo yanayostahili juu ya uhifadhi wa urithi huu.

# Mazoezi

Elimu ya Urithi wa Ulimwengu huhimiza umuhimu wa kujifunza kwa vitendo, ambapo wanafunzi hufunzwa harakati za kiutendaji. Njia hii ya ufundishaji inajulikana kama kujifunza kwa tajriba au uzoefu. Harakati hizi huhusisha ubunifu wa wanafunzi, mbinu za kutatua matatizo, ujuzi wa kisanaa na kiujumi, na ujuzi wa uigizaji. Baadhi ya mazoezi yanayopendekezwa katika kifaa hiki yanahusu kurasa za harakati za wanafunzi ambazo zinaweza kutumiwa na kukamilishwa na wanafunzi.

# Vikao vya kutazama

Elimu ya Urithi wa Ulimwengu inawatia moyo wanafunzi kujifunza kuhusu maeneo yaliyoonyeshwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu **(maeneo 754 kufikia May 2004)**. Kifaa hiki kinarahisisha kujielimisha kwa kuandaa picha mbali mbali. Watu wengi wachanga watakuwa wanaona maeneo haya kwa mara ya kwanza na sio rahisi kuyasahau. Walio na nafasi ya kufaidika kutokana na teknolojia mpya ya elimu kama vile 'CD-ROM' na mdahalish wanahimizwa kutumia njia hizi ili kuvumbua maajabu ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu.



© UNESCO 2004



*Wanafunzi wa Hungary wanafunzwa na mtaalamu kuhusu pango za Aggtelek Karst na Slovak Karst.*
*© UNESCO*

# Ziara ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu

Mradi wa UNESCO wa Watu Wachanga na Elimu ya Urithi wa Ulimwengu umeonyesha kuwa kadiri mtu anapopata elimu hii ndivyo pia anapata ilhamu ya kujifunza na kuvumbua zaidi na hata kuchunguza mambo nje ya mipaka ya taifa lake au hata bara. Baadhi ya harakati zilizo-pendekezwa katika kifaa hiki zinaandaa ufahamu bora wa sifa na thamani na uhifadhi wa maeneo ya kitamaduni na asilia yaliyoteuliwa katika sehemu mbali mbali za ulimwengu. Inatarajiwa kuwa habari ya msingi na picha zilizoandaliwa zitawapatia moyo wanafunzi kuwazia kuwa wamesafiri na kuvumbua maeneo ya mbali na kwa hivyo kukuza mapenzi maalum na kuyajali maeneo hayo.



## ■ Harakati ya wanafunzi ya 1

### MTIHANI KUHUSU MAENEO YA URITHI WA ULIMWENGU


### Lengo: Kuamua ufahamu wa wanafunzi kuhusu maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na kukuza hamu ya kuyahifadhi


**Mazoezi**


**Harakati darasani**


**Somo la kipindi *kimoja***


**Jiografia na masomo ya jamii**


**Picha, Orodha ya Urithi wa Ulimwengu, na Maelezo kwa ufupi**

✓ Waeleze wanafunzi kuwa utawapatia mtihani kuhusu Urithi wa Ulimwengu. Waambie waandike nambari 1 hadi 26 na majina ya kila eneo linaloonyeshwa kwenye picha. Iwapo hawana uhakika kuhusu jina la eneo linalohusika wanaweza kuandika jina la nchi eneo hilo linapopatikana. Waonyeshe picha 26 zilizo kwenye kifaa hiki, moja baada ya nyingine, ndio wapate nafasi ya kuandika jina la eneo linalohusika (jina la kila eneo limeandikwa nyuma ya kila picha).

✓ Baada ya kuwaonyesha picha zote, waambie wabadilishane hizo picha na wanafunzi wanaoketi karibu nao na wasahihishe mtihani wao kwa kupatiana alama moja kwa kila jibu sahihi na nusu alama kwa kila jibu sahihi kuhusu nchi (yaani pale ambapo hawakutambua eneo lakini walitambua liko nchi gani).



UNESCO 2004

# Ziara za maeneo na makavazi

Sifa muhimu ya elimu ya Urithi wa Ulimwengu ni nafasi vijana wanayopata ya kuzuru maeneo na makavazi katika jamii na nchi zao, au hata ng'ambo. Ili kuhakikisha athari inayofaa, ni muhimu kuwa na mpangilio wenye uangalifu, usimamizi madhubuti na harakati za kufuatilia ziara hizo.

## ▲ Ziara za maeneo

Tajriba imedhihirisha kwamba kilele cha elimu ya Urithi wa Ulimwengu ni ziara za maeneo hayo. Hatua zifuatazo zitawafurahisha walimu na wanafunzi na hawatazisahau.

### Matayarisho

Ili ziara ya eneo ifanikiwe, matayarisho kamili lazima yatekelezwe. Matayarisho yatahusisha:

- ziara tayarishi itakayotekelezwa na walimu
- kutayarisha hojaji au orodha ya maswali yatakayoulizwa wanafunzi kabla na baada ya ziara ili kukadiria mabadiliko ya maarifa, mielekeo, ujuzi na tabia kuhusu eneo fulani na uhifadhi wake.
- kutayarisha wanafunzi kwa mazoezi maalum kama vile kuhadithia kuhusu wakati wa kale, kutambiana hadithi na ngano kuhusu eneo linalohusika au kuchora eneo lenyewe
- kutayarisha kazi ambayo wanafunzi watapewa kama kifuatilizi cha ziara hiyo

### Ziara-awali

Jaribu kuhusisha kundi la walimu kutoka nyanja nyingi za masomo kama iwezekanavyo, kukusaidia kuwatayarisha wanafunzi kwa ziara. Mwalimu wa historia, kwa mfano anaweza kutoa habari kuhusu eneo hilo katika vipindi tofauti vya kihistoria. Mwalimu wa jiografia naye anaweza kuonyesha eneo lenyewe na kueleza sifa maalum za kijiografia za eneo hilo. Mwalimu wa lugha anaweza kuonyesha maandishi maalum (ya kifasihi, kishairi na kitamthilia). Mwalimu wa sanaa anaweza kuwauliza wanafunzi kuchora picha ya eneo hilo au kutayarisha kielelezo, naye mwalimu wa hesabu anaweza kuwauliza wanafunzi waonyeshe kihesabu jinsi lilivyojengwa eneo la kitamaduni au wakisie idadi ya aina mbali mbali ya vitu vinavyopatikana hapo. Mwalimu wa sayansi anaweza kuwafahamisha



Wanafunzi wa ASPnet kama wamevalia mapambo ya kichwa ya kale ya Misri wakati wa ziara yao ya piramidi zenye ncha kali huko Saggara, Misri. © UNESCO



© UNESCO 2004

wanafunzi kuhusa vitisho vinavyoweza kulikabili eneo hilo kutokana na utalii, uharibifu wa mazingira na kutotunzwa.

Ifanye ziara hii kuwa na tajriba *isiyosahaulika* kwa kuwashauri wanafunzi wavalie nguo za kitamaduni, na pia uwaletee muziki wa kitamaduni au uwaulize wanafunzi waimbe nyimbo hizo, alikeni mgeni maalum na kadhalika. Uliza iwapo eneo hilo lina afisa wa elimu ili awasaidie katika utayarishaji wa safari. Iwapo kuna habari za kielimu ambazo zimetayarishwa kuhusu eneo hilo, zitumie na wanafunzi wako kabla ya safari. Tafuta habari zote za maana ambazo zitahitajika kama vile ada ya kuingia, masaa ya kufungua na kufunga, idhini ya kupiga picha, kuwepo kwa vyakula na vinywaji, duka za kuuza vifaa vya ukumbusho, vyoo na huduma ya kwanza.

Tayarisha kurasa za harakati za wanafunzi zitakazojazwa wakati wa ziara, na vifaa mbali mbali vitakavyohitajika kama vile makaratasi ya kuandikia na kuchorea, kamera na penseli. Kama una video, ziara hii inaweza kurekodiwa na kuonyeshwa wanafunzi, wazazi na watu wengine baadaye.



Ukurasa wa harakati za wanafunzi
Ziara ya eneo



## Ziara ya eneo

Wazia kuhusu harakati mbali mbali wakati wa ziara kama vile kuchora, kupiga picha, kutayarisha mahojiano (pamoja na waelekezi wa maeneo hayo au wafanyikazi au hata baina ya wanafunzi wenyewe), utayarishaji wa ripoti ya kila mwanafunzi *kuhusu ziara hiyo*, utayarishaji wa video, kuwapatia fursa ya kustarehe (kwa mfano, uimbaji, vyakula vilivyotayarishwa na wazazi vyaweza kugawanywa na wafanyikazi wa mahala hapo).



*Wanafunzi wanaotembelea Hekalu ya Heaven wakati wa Muungano wa Vijana Wanaohusika na Urithi wa Ulimwengu, Beijing, wanachora eneo hilo la kiasilia kwenye karatasi ya mita 25.*
*© UNESCO*



*Muungano wa Wanafunzi Wanaohusika na Elimu ya Urithi wa Ulimwengu huko Victoria Falls (Mosi-oa-Tunya) Zambia na Zimbabwe, wakijadiliana kuhusu ziara yao ya eneo hilo.*
*© UNESCO*

## Kufuatilia ziara ya eneo

Ufuatiliaji wa ziara ya maeneo haya ni muhimu kama ziara yenyewe kwani wanafunzi hukumbuka kikamilifu waliyoyaona *na kuwafahamisha* wenzao. Mapendekezo kuhusu ufuatiliaji huu yanahusisha:

- → kujadiliana na wanafunzi kuhusu walioyaona na kujifunza, na pia waliyoyafurahia sana na yale ambayo hawakuyafurahia

© UNESCO 2004

- kupendekeza mradi mwingine wa utafiti, kama vile njia za kuboresha eneo hilo ili kuvutia watalii zaidi na kuendelea kulitunza eneo, kuchunguza vitisho vyovyote vinavyolikabili eneo hilo na kupendekeza suluhisho, kupendekeza vijana waelekezi wasaidie katika usimamizi wa shughuli za kitalii
- uchoraji picha kwa rangi na uchongaji unaotokana na michoro wakati wa ziara. Wanafunzi pia wataweza kuonyesha kazi yao
- kuhimiza wanafunzi kutayarisha picha walizozipiga wakati wa ziara na kisha watayarishe mahali pa kuzionyesha ambapo wanafunzi au wazazi wanaweza kuchagua picha zinazotia fora zaidi na kutoa zawadi ndogo kwa washindi
- uandikaji wa makala kuhusu ziara zao na kuyatumia magazeti ya shule au ya umma
- wanafunzi kupendekeza eneo lingine la kutemebelewa



Muungano wa Vijana wa Ulimwengu, Beijing.
© *UNESCO*



© UNESCO 2004

Kukamilishwa na kila mwanafunzi kabla ya ziara na mara tu baada ya ziara (hasa eneo la Urithi wa Ulimwengu)

**Jina la eneo** ..........................................................................................................

**Jina la mwanafunzi** ..........................................................................................................

**Tarehe ya ziara katika eneo** ..........................................................................................................

**Andika matarajio yako ya ziara (unachotaka kuvumbua, kujifunza, n.k.)**

## Wakati wa ziara

Chora sehemu ya eneo ambalo limekuvutia (tumia karatasi tofauti)

Andika rekodi kuhusu sifa za eneo husika ambazo umejifunza

Andika uliyoyavumbua kutokana na hisia: ulipofunga macho yako eleza ulichosikia, ulichonusa, na ueleze sifa ya eneo hili iliyokuathiri zaidi:

**Sauti:** ..........................................................................................................

..........................................................................................................

**Harufu:** ..........................................................................................................

..........................................................................................................

***Ulichoona:*** ..........................................................................................................

..........................................................................................................

## Baada ya ziara

Je, matarijio yako ya ziara ya eneo yalitimizwa? ❑ Ndio ❑ Hapana

**Eleza**

Eleza umuhimu wa eneo hili

Maoni yako ya mwisho

Sahihi

Tarehe:

## ▲ Ziara za makavazi

Ziara za makavazi ni mbinu muhimu ya ufundishaji wa *elimu* ya Urithi wa Ulimwengu. Wafanyikazi wa makavazi na wanachama wa Shirika la Kimataifa la Makavazi wanaweza kuwa washiriki katika ufundishaji. Makavazi aghalabu ndiyo mahali pekee ambapo ushahidi wa sifa fulani ya kitamaduni au kiasilia inaweza kupatikana, kuonekana na kuchunguzwa.

Kwa shule ambazo haziko karibu na makavazi jamii ya eneo hilo wanaweza kuwasaidia wanafunzi kuhusisha historia na wakati wa sasa.



*Wanafunzi wanatembelea makavazi ya kihistoria, nyumba iliyokuwa ya watumwa katika Kisiwa cha Goree, Senegal.*
*© UNESCO*



*Wanafunzi wa ASPnet wanasikiliza mhadhara maalum katika Makavazi ya Roma Alexandra, Misri.*
*© UNESCO*

### Hotuba maalum wakati wa kuzuru makavazi

Baadhi ya makavazi ni kubwa mno na huwa na vitu vingi pamoja na vitu vilivyohifadhiwa vya kale ambavyo vijana hawawezi kuvielewa na kuvithamani katika ziara moja. Walimu wengine huamua kumulika mada moja katika ziara yao ya makavazi na kupanga mhadhara na *mhadhiri* aliye stadi na mchangamfu.

### Kuchunguza vifaa vilivyohifadhiwa

Kabla ya kuzuru makavazi, kila mwanafunzi anaweza kupewa jukumu la kukichunguza kitu kilichohifadhiwa wakati wa ziara. Kila mwanafunzi anaweza kupewa Ukurasa wa harakati za wanafunzi unaohususisha kuchunguza vitu hivi. Baada ya ziara, wanafunzi wanaweza kuwasilisha waliyojifunza darasani.



© UNESCO 2004

Waonyeshe wanafunzi kitu kilichohifadhiwa wakichunguze:

| Sifa itakayo chunguzwa | Maswali | Uchunguzi | Utafiti wa ziada unaohitajika |
|---|---|---|---|
| **Sifa za asilia** | ▪ Ni cha rangi gani?<br>▪ Kinanukia kama nini?<br>▪ Kinasikika kama nini?<br>▪ Kimetengenezwa kwa nini?<br>▪ Ni cha kiasilia au cha kutengenezwa?<br>▪ Je, kimekamilika?<br>▪ Je, kimebadilishwa, kurekebishwa au kutengenezwa?<br>▪ Kimezorota? | | |
| **Ujenzi** | ▪ Kimetengenezwa kwa mkono au mashini?<br>▪ Je, kiliundwa kwa kufinyangwa au kipande kwa kipande?<br>▪ Je, kimeunganishwaje? | | |
| **Utenda kazi** | ▪ Kimekuwa kikitumika kwa njia gani?<br>▪ Matumizi yake yamebadilika? | | |
| **Kilivyobuniwa** | ▪ Kinaweza kikatelekeza jukumu lililokusudiwa awali?<br>▪ Kimerembeshwa?<br>▪ Kimetengenezwa kwa vifaa bora?<br>▪ Je,kinakupendeza?<br>▪ Je, ungekibuni vipi? | | |
| **Thamani** | ▪ Kina thamani gani?<br>▪ Kwa watu walioikitengeneza?<br>▪ Kwa watu waliokitumia?<br>▪ Kwa watu wanaokiweka?<br>▪ Kwako wewe?<br>▪ Kwa makavazi?<br>▪ Kwa mkusanyaji? | | |

## Ziara za karakana za kiufundi



Orodha ya Marejeleo

Bidhaa fulani za ufundi kama vile ufinyanzi huweza kupatikana katika makavazi. Ufundi huu bado huendelezwa hata sasa na mafundi ambao wameuridhi ujuzi huu kutoka kizazi hadi kizazi. Kwa kupanga ziara za karakana za aina hii, wanafunzi watajionea wenyewe jinsi bidhaa za ufundi wa kienyeji wanazoziona kwenye makavazi zinavyoendelea kutengenezwa hadi leo. Kwa njia hii watajionea uhusiano baina ya kitambulishi chao, urithi wao (pamoja na urithi wa ulimwengu) na ufundi wa kienyeji.



*Watoto wanajifunza sanaa ya ufumaji huko Guatemala kama sehemu ya Mradi wa Kutambulisha Sanaa na Ufundi.*
*© UNESCO*



# Uigizaji

Walimu wengi wanaonuia kuwavutia wanafunzi kwa shughuli za uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu wametambua uigizaji kuwa na manufaa sana. Uigizaji unahusisha malengo matano makuu ya ufundishaji:

- → kuelimisha
- → kurahisisha uelewaji wa mada ngumu au za kidhahania
- → kuwapatia wanafunzi mbinu mpya za utafiti
- → kuimarisha mielekeo inayofaa na kujitolea daima
- → kukuza uwezo wa kubuni wa wanafunzi

## ▲ Uigizaji darasani

Uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu huhusisha mambo na maswala mengi kama vile uamuzi wa kuongezea maeneo mapya katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu, uteuzi wa vifaa na mbinu tofauti za uhifadhi, maendeleo (ubomoaji wa nyumba kuukuu, uendelazaji wa utalii, ujengaji wa barabara mpya, na kadhalika), upangaji wa uhifadhi na usimamizi, ukaguzi wa maeneo, kampeini za kuendeleza shughuli hizi, au uamuzi wa kuunga mkono kifedha eneo moja dhidhi ya lingine.

Kupitia kwa uigizaji wanafunzi wanafikia hali ya kuelewa maswala haya na kuchukua uamuzi unaofaa. Mwalimu anaweza kugawanya wanafanunzi katika makundi madogo na kuuliza kila kikundi kuwazia na kutafiti juu ya nafasi ya kundi au mhusika watakayemuigiza. Mwalimu atawasaidia wanafunzi kwa kuwapendekezea namna ya kupata habari inayotakikana. Au, anaweza

© UNESCO 2004

kutayarisha mapema kadi zinazoeleza sifa za kila kikundi kitakachoigizwa na wanafunzi. Kila kikundi cha wanafunzi kitapata kadi na kujadili kuhusu nafasi waliopewa na kumteua mmoja wao kuigiza nafasi hiyo. Atakayeteuliwa atatetea msimamo wa kikundi chake. Wanafunzi wale wengine watachukua nafasi ya waamuzi au kamati itakayopiga kura kutoa uamuzi kutokana na uigizaji huo.

Ili wanafunzi waelewe kikamilifu harakati hii ya uigizaji, hatua zifuatazo zinaweza zikachukuliwa:

- → ainisha tisho linalokabili juhudi za kuhifadhi eneo la Urithi wa Ulimwengu
- → wanafunzi wanaowakilisha makundi yenye maslahi tofauti watawasilisha njia tofauti za kukabiliana na tisho hilo
- → wanafunzi watatathmini suluhisho zilizotolewa
- → wanafunzi wataamua jinsi ya kutekeleza suluhisho bora
- → wanafunzi watatathmini matokeo ya uteuzi wao

## ▲ Kufufua historia kupitia kwa tamthilia katika maeneo ya Urithi wa Ulimwengu

Kuigiza michezo ya kihistoria katika eneo la Urithi wa Ulimwengu huwacha kumbukumbu ya kudumu katika fikra za watu wachanga. Michezo kadhaa maarufu imeshaigizwa katika maeneo haya, kama vile *Hamlet* ya Shakespear iliyoigizwa katika kasri ya Kronburg, Denmark na *Verdi's Opera Aida* huko Luxor, Misri. **Wanafunzi wa mradi wa UNESCO wa ASPnet,** waliigiza tamthilia iliyomhusu mfalme mkuu Diocletian, katika magofu ya makao yake, mjini Split huko Kroatia. Mji wa Split ni eneo mojawapo la Urithi wa Ulimwengu.





*Wanafunzi wa ASPnet kutoka mji wa Split wanafufua historia kupitia kwa tamthilia (mji wa kihistoria wa Split pamoja na makao ya Diocletian, Croatia) © UNESCO*

© UNESCO 2004

## ▲ Kutatua mzozo kwa amani

Wakati mwingine mzozo hutokea kuhusiana na uhifadhi wa *Urithi* wa Ulimwengu. Mzozo huu unaweza kusababishwa na ubishi kuhusu umiliki au vita na mapendekezo ya maendeleo na unapaswa kutatuliwa kwa njia ya amani na haki. Uigizaji utawafaa watu wachanga katika kutatua mizozo bila kupigana, *kuwasaidia* wawe na mitazamo tofauti, na kuwaeleza umuhimu na mbinu za kutekeleza dhana ya kuafikiana. Walimu wanaweza kubuni *hali mbili tofauti; moja* inayoonyesha mradi wa maendeleo na nyingine inayoonyesha ulinzi wa eneo la Urithi wa Ulimwengu. Wanafunzi watagawanywa katika makundi tofauti na kila kikundi kupewa nafasi mahsusi, kama vile msimamizi wa maendeleo, mlinzi wa *kitamaduni* wa eneo, afisa mwangalizi wa eneo la makumbusho, meya wa eneo husika, mjenzi katika eneo husika au mtalii. Orodha hii inayofuatia *inastahili* kupewa kila kundi ili kuwasaidia kujitayarisha kwa mjadala ambao utaleta suluhisho ambalo litamridhisha na kumtuliza kila mmoja na ambalo halitasababisha shida baadaye.

Mambo yanayostahili kumulikwa katika kutatua mzozo kwa amani kupitia kwa uigizaji:

1. **Tilia mkazo maswala na wala siyo anaye zungumza.**
2. **Jaribu kujiweka katika hali ya wapinzani wako na ukumbuke ya *kuwa kikundi* kimoja kinaweza kuwa na maslahi kadhaa.**
3. **Wapatie wapinzani wako nafasi ya kuzungumza kiwazi *kuhusu* maoni na hisia zao. Sikiliza kwa makini.**
4. **Jaribu kuwaelewa wapinzani wako na ubishani wao mkuu.**
5. **Uliza maswali badala ya kutoa taarifa za kijumla.**
6. **Hakikisha kuwa wapinzani wako wanaelewa maoni yako.**
7. **Usipeane maelezo kupita kiasi.**
8. **Tafuta suluhisho ambalo litaridhisha makundi yote ikiwezekana. Lengo ni kutafuta suluhisho mwafaka.**
9. **Usiwatishe wapinzani wako.**
10. **Usikubali kushindwa hata kama upinzani *una* nguvu zaidi.**
11. **Toa mchango wa kusisimua na wa manufaa.**
12. **Tatua mzozo kwa hatua, ukikabiliana na maswali *mazito* moja hadi lingine.**
13. **Shirikiana ili kuepuka mizozo mipya.**
14. **Mkubaliane kuhusu njia za kutatua mizozo ya baadaye.**



Mwalimu anastahili kukaa kando na kuzingatia yanaoyendelea lakini atoe msaada iwapo *utahitajika*.

# Ushirikiano wa ulimwengu na mdahalishi

Tunaishi wakati wa maendeleo ya kisasa ya *upashaji* habari. Kupitia kwa mdahalishi tunaweza kufikia maktaba, hifadhi ya data mbali mbali, nyaraka za kale zilizohifadhiwa, ripoti za hali ya anga, bidhaa mbali mbali zinazotumiwa na



© UNESCO 2004

binadamu. Habari na data ni vipengele muhimu vya elimu ya Urithi wa Ulimwengu na utafiti, na utumiaji wa teknolojia ni njia muhimu inayowawezesha walimu na wanafunzi kuvumbua thamani ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na kujifunza mambo zaidi ya uhifadhi.

Sio watu wote ulimwenguni waliobahatika kutumia huduma hii ya mdahalishi. Hata hivyo gharama za tarakilishi zinapoendelea kushuka na huduma za kimawasiliano kusambaa kote ulimwenguni, idadi ya watumiaji inatarajiwa kuongezeka kwa kasi.

## ▲ Ushirikiano wa *ulimwengu*

Mradi wa Elimu ya Urithi wa Ulimwengu wa Vijana wa UNESCO unaruhusu shule kuwa sehemu ya mtandao wa ulimwengu unaohusisha aina mbali mbali za shule za sekondari katika sehemu zote za ulimwengu. Lengo muhimu la mradi huu ni kujifunza pamoja na kuelezea njia mpya na dhabiti za kuanzisha dhana ya Urithi wa Ulimwengu kwenye mitaala.

Shule nyingi zinazohusika katika mradi huu ni wanachama wa **Mradi wa Shirikisho la Mashule** (ASPnet) wa UNESCO. Mradi huu umebuniwa kutilia nguvu dhana ya ubinadamu, utamaduni, na elimu ya kimataifa kwa kuanzisha miradi ya majaribio kama vile Mradi wa Elimu ya Urithi wa Ulimwengu kwa Watu Wachanga unaoendeshwa kupitia kwa ASPnet pamoja na **Makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu.** Shule za mradi wa ASPnet huanzisha uhusiano na shule zingine na kuzungumzia tajriba zao tofauti na kugawana vifaa.

Ushirikiano wa UNESCO huwaleta wanafunzi na walimu pamoja kutoka sehemu tofauti za ulimwengu na hutekelezwa kupitia kwa Muungano wa Vijana Wanaohusika na Urithi wa Ulimwengu kwa kuandaa warsha za kitaifa na kimaeneo kwa walimu. **Mataifa wanachama** wa UNESCO pia huhimizwa kuandaa mafunzo maalum kwa walimu na wanafunzi.

Bila shaka ni gharama kubwa kuwaleta pamoja wanafunzi na walimu kutoka sehemu mbali mbali za ulimwengu. Matumizi ya teknolojia kuwaunganisha watu kama vile utumiaji wa mdahalishi, ni njia muhimu ya kujuanisha watu, kuendeleza mawasiliano na kubadilishana mawazo.

Ushirikiano halisi unahitaji usambazaji thabiti wa habari na uhusiano wa karibu. Shirika la UNESCO mara kwa mara hutoa habari kuhusu mradi huu wa Urithi wa Ulimwengu kwenye mdahalishi na katika chapisho zake.

# ▲ Mdahalishi waunga mkono elimu ya Urithi wa Ulimwengu

Njia za kufikia taarifa tofauti zinaendelea kubadilika sana na kuendelezwa wakati teknolojia za mawasiliano zinaibuka. Jukumu kubwa linalowakabili vijana siku hizi ni kuchuja taarifa zitakazowafaa zilizopo katika msitu wa taarifa na data zilizo kwenye mdahalishi.



© UNESCO 2004

Orodha ya Marejeleo

## Mdahalishi

Mdahalishi ni mtandao wakubadilishana taarifa ulimwengu mzima unaotegemea mfumo sawa wa mawasiliano. Mfumo huu huhifadhi taarifa, majarida, chapisho za kielimu na hutoa nafasi ya kupasha na kueneza habari.

Mdahalishi unaenea kwa ukasi ambao haukutarajiwa hapo awali. Kurasa-tovuti mpya zinaongezwa kila siku. Katika mwaka wa 1995 kulikuwa na watumiaji milioni 56. Katika mwaka wa 2001, idadi hii ilifika watumizi milioni 211.

## Barua pepe (e-mail)

Barua pepe ni njia ya kutuma ujumbe kwa kutumia tarakilishi. Ujumbe unapigwa taipu katika tarakilishi ambayo imeunganishwa na tarakilishi nyingine kupitia kwa modemu na simu za *kisasa, au kupitia* kwa umeme.


Shule yeyote ambayo ina tarakilishi ya aina yeyote, na modemu pamoja na simu inaweza kupata huduma ya barua pepe na kuwa sehemu ya mawasiliano mapya ya kimtandao.

Ni rahisi, kwa mfano kujiandikisha kwa *WHNEWS*, huduma ya UNESCO ya *kusambaza* habari za Urithi wa Ulimwengu, au kutumiwa *World Heritage Newsletter* ya UNESCO kupitia kwa barua pepe. Na hata taarifa zinapatikana kutoka kwa tovuti kupitia kwa barua pepe.

## Tovuti au Web au WWW



Tovuti ni mojawapo wa vifaa vinavyopatikana kwenye mdahalishi. Vifaa hivi huwawezesha watumiaji kutandaza taarifa kwa hadhira ya ulimwengu. Watumiaji wa *tarakilishi* 'hubandika' taarifa kama kwamba imo kwenye ubao wa utangazaji. Kurasa zilizo kwenye tovuti hujulikana *kama kurasa-tovuti* (web pages). Tovuti huwa na maneno yaliyosisitizwa (links) ambayo yatakuelekeza kwa taarifa zingine muhimu (kwa mfano, hati, mashirika, n.k.) zinazopatikana kwenye tovuti.



Kurasa zingine za tovuti hutoa taarifa kama makala, na zingine huwa na picha, picha-sinema, au sauti. Mkusanyiko wa kurasa-tovuti zilizotolewa na taasisi, shirika, *shule, n.k.*, hujulikana kama eneo-tovuti (web site).

## Kwa nini tutumie mdahalishi?

Mdahalishi huwapatia walimu na wanafunzi fursa ya kujitafutia taarifa mpya papo hapo na pia nafasi ya kuwasiliana na walimu wengine, wanafunzi na mashule mbali mbali *ulimwenguni*. Wanafunzi wanahitaji kupata ujuzi na vifaa ili wanufaike kutokana na taarifa ambazo mdahalishi huu unaweza *kuwasilisha*.

Utumiaji wa mdahalishi una manufaa yafuatayo:

- huwajulisha wanafunzi juu ya matumizi ya kimsingi ya mdahalishi
- hukuza ujuzi wa kutumia teknolojia ya mawasiliano ili kutafiti juu ya Urithi wa Ulimwengu

© UNESCO 2004

- → huandaa fursa ya kupata taarifa, uchapishaji wa magazeti kwneye mdahalishi, programu za kutumika katika tarakilishi, na fursa ya *kubadilishana* habari kuhusu mada mahsusi za Urithi wa Ulimwengu
- → hukuza ufundishaji na uelewano kati ya tamaduni tofauti kwa kuwapatia wanafunzi nafasi ya kuwasiliana na wenzao kutoka sehemu tofauti
- → huwahimiza wanafunzi kutumia teknolojia ya mawasiliano kutatua matatizo kadhaa.

Kupitia kwa mdahalishi na barua pepe wanafunzi wanaweza kujijulisha, kueleza tamaduni, mila, kanuni za kijamii, na urithi wao kwa wenzao. Hata bila ya kutoka nje ya madarasa wanaweza kuwasiliana moja kwa moja na wanafunzi wenzao katika nchi zao au ng'ambo ili kuwajulia hali, na pia *kujifahamisha kuhusu mila* na ustaraabu wao na maeneo ya urithi yaliyomo. Shule kutoka sehemu mbali mbali za ulimwengu zinaweza kufanya kazi pamoja katika miradi inayolenga kulinda urithi wa watu wote ambao unakabiliwa na tisho au uharibifu kutokana na uchafuzi wa *mazingira, ukuaji wa miji*, vita au kutotunzwa.

### Harakati

1. **Tafuta tovuti la UNESCO na uchunguze shughuli wanazofanya za *kuhifadhi* Urithi wa Ulimwengu: http://www.unesco.org/whc**
2. **Chunguza tovuti la ASPnet na utambue shule inayohusika na elimu ya Urithi wa Ulimwengu. http://www.unesco.org/education/asp**
3. **Anzisha mradi wa elimu ya Urithi wa Ulimwengu, kwa mfano, mradi wa kueleza na kulinganisha *utalii wa maeneo* ya Urithi wa Ulimwengu katika mataifa mawili.**
4. **Andika majina ya maeneo yanayopendekezwa kuhusishwa katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Badilishana orodha *yako na ya* shule nyingine.**
5. **Andika hadithi ya kikatuni kumhusu Patrimonito akitembelea eneo la karibu la Urithi wa Ulimwengu, na uitumie shule nyingine hadithi yako.**
6. **Tafuta ushauri kutoka maktaba kuu ya chuo kikuu katika nchi nyingine ili kutayarisha marejeleo *juu ya eneo* mahsusi la Urithi wa Ulimwengu.**
7. **Changisha pesa ili kuitafutia vifaa na kuiingiza kwenye mdahalishi shule inayohusika na ufundishaji wa Urithi wa *Ulimwengu* ambayo haina vifaa hivi.**
8. **Buni ukurasa-tovuti wa shule yenu na ueleze miradi yenu ya kielimu ya urithi wa ulimwengu.**
9. **Tumia mtandao kuwasiliana na wenzako walio nchi zingine ili kujadili maswala maalum ya elimu ya Urithi wa Ulimwengu.**
10. **Jiandikishe upate gazeti la *World Heritage Newsletter* kupitia barua pepe, *WHNEWS*, chunguza tovuti la ASPnet, na utafute ushauri kutoka kwa tovuti la Elimu ya Urithi wa Ulimwengu.**

## ▲ Urithi wa Ulimwengu kwenye mdahalishi

Tovuti ya Urithi wa Ulimwengu, yaani tovuti rasmi ya Ofisi ya *Mapatano Kuhusu Ulinzi wa Urithi wa Ulimwengu wa Kitamaduni na Kiasilia*, ndio chanzo madhubuti



© UNESCO 2004

zaidi cha habari kuhusu Orodha ya Urithi wa Ulimwengu, *Mapatano*, na washiriki kote ulimwenguni. Kwa kutumia tecknolojia mpya ya kukusanya data, eneo hili la tovuti linaandaa taarifa za maeneo, *Mapatano*, vichapo, habari, harakati, jinsi ya kuchanga, na namna ya kuwasiliana na washiriki wanaohusika *na ulinzi* wa urithi huu wa watu wote. Kila moja ya maeneo 754 yaliyo kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu yameelezwa *katika* kurasa-tovuti, na kuelekezwa kwa mashirika mengine yanayo taarifa zaidi. Kila moja ya Mataifa Husika 178 wa *Mapatano* vile vile yana kurasa-tovuti yake inyotoa habari kuhusu kuwasiliana nao pamoja na mashirika yanoyohusika, na harakati zinazohusu Urithi wa Ulimwengu.

*Tovuti ya Urithi* wa Ulimwengu kwa sasa imegawanwa katika maeneo yafuatayo:

MAPATANO
ORODHA YA URITHI WA ULIMWENGU
KILA MMOJA NA KAZI YAKE
TUFANYAVYO KAZI
SHIRIKIANA NASI
TAARIFA NA MATUKIO
VIFAA

MAPATANO hueleza jinsi *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* yanavyo fanya kazi.

ORODHA YA URITHI WA ULIMWENGU ina ramani inayofuatwa kwenye tarakilishi kuangalia maeneo pamoja na orodha ya maeneo yote ya Urithi wa Ulimwengu yaliyopangwa kwa jimbo na kategoria.



KILA MMOJA NA KAZI YAKE na TUFANYAVYO KAZI hutoa *taarifa kuhusu* washiriki tofauti wa *Mapatano* (Wanaopendekeza maeneo, Wanaochagua, Wanaotoa ushauri, Jinsi mradi unavyosimamiwa) na taratibu za kuteua na kuendeleza kwa Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu.

Sehemu ya HARAKATI huandaa miradi ya kuendeleza na kulinda Maeneo ya Urithi wa *Ulimwengu*. Harakati za kielimu zitapatikana hapa.

SHIRIKIANA NASI: makusidio ni kuanzisha ushirikiano wa kudumu ili kuandaa rasilmali za kudhibiti na kupanua utaalamu uliopo wa kiufundi na usimamizi, na vile vile kutoa msaada wa kifedha wa kusaidi usimamizi bora wa Urithi wa Ulimwengu.

TAARIFA NA MATUKIO huandaa matangazo mapya kuhusa ulinzi wa Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu.


Tazama tovuti la Urithi wa Ulimwengu kwenye anwani ifuatayo:
**http://www/unesco.org/whc**

Anwani zingine muhimu
Orodha ya Urithi wa Ulimwengu: **www.unesco.org/whc/heritage/htm**
Orodha ya maeneo yaliyo *hatarini*: **www.unesco.or.whc.danglist.htm**
Matifa wanachama wa *Mapatano*: **www.unesco.org/wldrat/htm**

## Mtandao wa Taarifa za Urithi wa Ulimwengu

Mtandao wa Taarifa za Urithi wa Ulimwengu (World Heritage Information Network au WHIN) unashirikisha Makao ya Urithi wa Ulimwengu na mashirika mengine yanayohusika na *utunzaji* wa maeneo hayo. Iwapo yatadumisha maeneo

© UNESCO 2004






ya tovuti, mashirika haya yatakuwa washiriki wa WHIN na wanahimizwa kushiriki kwa vitendo katika utoaji taarifa halisi kuhusu maeneo ya Urithi wa Ulimwengu. Anwani za kuwasiliana na washiriki wengine wa WHIN ziko kwenye *kurasa*-tovuti zinzohusiana na maeneo ya Urithi wa Ulimwengu.

Kwa maelezo zaidi tembelea kurasa-tovuti ya WHIN:
**http://www.unesco.org/whc/whin/enindex.htm**
au tuma barua pepe kwa anwani ifuatayo: **wh-info@unesco.org**

### *World Heritage Newsletter* na WHIN


*Gazeti* la *World Heritage Newsletter* limechapishwa tangu mwaka wa 1992. Ni chapisho la kurasa nne linalotolewa mara *mbili kwa mwezi* na kusambazwa bila malipo kwa waliojiandikisha kulipokea. Ili kujiandikisha tuma barua pepe kwa wheditor@unesco.org au andika barua kwa: Newsletter, UNESCO World Heritage Centre, 7 Place de Fontenoy, 75352 Paris 07 SP, FRANCE. Makala ya sasa na ya awali ya gazeti hili yanaweza kupatikana kwenye kurasa-tovuti zifuatazo:
**http://www.unesco.org/whc/news/index-en.htm** (kwa Kiingereza) au
**http://www.unesco.org/whc/fr/news/index-fr.htm** (kwa Kifaransa)

## ▲ ASPnet kwenye mdahalishi

Eneo la tovuti la ASPnet linahusisha taarifa za kijumla kuhusu mtandao, malengo yake, idadi ya shule na nchi zinazoshiriki, miradi ya kielelezo, hati na vitabu ambavyo vinapatikana za ASPnet Practical Manual, na vijitabu.

© UNESCO 2004

## ▲ Anwani muhimu kwenye mdahalishi




Mradi wa Shirikisho la Mashule (ASPnet)
http://www.unesco.org/education/asp

Makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu
http://www.unesco.org/whc/
barua pepe: wh-info@unesco.org

Orodha ya Urithi wa Ulimwengu
http://www.unesco.org/whc/nwhc/pages/sites/main.htm

Umoja wa Ulimwengu wa Uhifadhi (IUCN)
http://www.iucn.org

Baraza la Kimataifa la Makavazi
http://www.icom.org

Halmashauri ya Ulimwengu ya Majengo na Maeneo ya Kumbukumbu
http://www.icomos.org

Makao ya Kimataifa ya Masomo ya Uhifadhi na Ujenzi wa Mali-tamaduni
http://www.iccrom.org

Rasilmali za Mdahalishi za Uhifadhi wa Urithi
http://www.cr.nps.gov/ncptt/irg/

Shirika la Miji ya Urithi wa Ulimwengu
http://www.ovpm.org



© UNESCO 2004

# Mapatano ya



**'... kuchakaa au kutoweka kwa... urithi wa kitamaduni au wa kiasilia husababisha kudunishwa kunakodhuru kwa urithi wa mataifa yote ya ulimwengu.'**

**Dibaji ya *Mapatanao ya Urithi wa Ulimwengu***

Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu

# *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu*

Ukurasa


**Maarifa** **39**
Mielekeo 39
Ujuzi 39

**Ufahamu wa urithi wetu** **40**

Urithi ni nini? 40

**Harakati za wanafunzi za 2:**
Maana ya urithi 41
Vitisho vinavyokumba uhifadhi wa urithi 42

**Uokoaji wa Urithi wa Ulimwengu** **43**

Kampeini iliyofaulu ya Abu Simbel 44
**Harakati za wanafunzi za 3**:
Miujiza Saba ya Ulimwengu 45
Kuandika mapatano ya kuokoa Urithi wa Ulimwengu 46
**Harakati za wanafunzi za 4:**
*Uelezaji wa maana ya urithi na uhifadhi* 46

***Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* ya UNESCO** **47**

Dhana ya Urithi wa Ulimwengu 48
***Harakati za wanafunzi za 5:***
Uhifadhi na urithi-sheria na mapatano ya kimataifa 49
*Asilia na utamaduni yanahusiana kwa karibu* 50
Urithi wa kitamaduni na kiasilia 50
Mandhari ya kitamaduni 50

**Utaratibu wa kuhifadhi Urithi wa Ulimwengu** **51**

Orodha ya Urithi wa Ulimwengu-maeneo yenye thamani kuu 53
Mkakati wa kiulimwengu unayohakikisha kuwa na Orodha aya Urithi wa Ulimwengu sawazishi na wakilishi 53
**Harakati za wanafunzi za 6**: Kubuni kielelezo cha eneo la Urithi wa Ulimwengu 54
**Harakati za wanafunzi za 7:** 55
*Kutambua maeneo* ya Urithi wa Ulimwengu katika sehemu unayoishi
Ukurusa wa harakati za wanafunzi 56
*Utambuaji wa maeneo* ya Urithi wa Ulimwengu katika jimbo lako

**Vigezo vya kuchagua maeneo ya Urithi wa Ulimwengu** **57**

Vigezo vya kuchagua maeneo *yenye urithi* wa kitamaduni 57
Vigezo vya kuchagua maeneo yenye urithi wa kiasilia ya Urithi 58
Vigezo vya kuchagu maeneo yenye urithi wa sifa za kitamaduni na kiasilia 68
Utumiaji wa vigezo 59
**Harakati za wanafunzi za 8**: 60
Utambuaji wa eneo la Urithi wa Ulimwengu katika jimbo lako
Ukurasa wa harakati za wanafunzi: 61
Utambuaji wa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu 63

**Harakati za wanafunzi za 9**: 63
Uelewaji wa vigezo vya kutambua maeneo ya Urithi wa Ulimwengu
Ukurasa wa harakati za wanafunzi: 64
Utambuaji wa vigezo vya Urithi wa *Ulimwengu*
**Harakati za wanafunzi za 10:** 66
Uteuzi wa maeneo ya kitamaduni na ya kiasilia
Ukurasa wa harakati za wanafunzi: 67
Uteuzi wa maeneo ya kitamaduni na ya kiasilia

**Kamati ya Urithi wa Ulimwengu na Makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu** **69**

**Harakati za wanafunzi za 11:** 70
Mkutano wa Kamati ya Kitaifa ya Urithi
***Harakati za wanafunzi za 12:*** 71
Makao ya Kihistoria ya Santa Cruz de Mompox, Kolombia

**Kufuatilia hali ya uhifadhi ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu** **74**

Orodha ya maeneo ya ulimwengu yaliyo hatarini 74
**Harakati za wanafunzi za 13:** 76
Yellowstone, Marekani
**Harakati za wanafunzi za 14**:
*Kutayarisha* kipindi cha radio kuhusu Urithi wa Ulimwengu 79
Hazina ya Urithi wa Ulimwengu 79

Harakati za wanafunzi za 15: Kuzusha ufahamu 82

Kupitia kwa mitaala: Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu 83

# Ufahamu wa urithi wetu

## ▲ Urithi ni nini?

Urithi ni yale tuliyoachiwa na mababu zetu, yale tunayoishi nayo sasa, na yale tutakayowaachia vizazi vijavyo wajifunze nayo na kuyaonea fahari.

Kwenye kamusi urithi umeelezwa kama kitu ambacho kimerithiwa.

**Urithi**

1. Kile ambacho kimerithiwa au kitarithiwa
2. Hali ya kurithi, kuwachiana urithi
3. Kitu chochote ulichopatiwa au kupokea kama mali yako
4. Sehemu iliyorithiwa

Tafsiri kutoka Shorter Oxford Dictionary


Urithi unaweza kuchukuliwa kama mahala penye umuhimu wa kitamaduni na kiasilia ambapo tungependa kupahifadhi. Urithi pia ni vitu ambavyo tungependa kuviweka daima. Mahala na vitu hivi tunavithamini kwa sababu vinatokana na mababu zetu, vinapendeza, vina umuhimu wa kisayansi na ni vielelezo adimu vya asili ya maisha, na vinavutia. Urithi ni kielelezo muhimu na kitambulishi chetu. Urithi huu humulika maisha ya mababu zetu na bado upo leo kwa sababu juhudi mahsusi zimefanywa za kuuhifadhi.




Urithi wa Ulimwengu na Kitambulishi

Je, unaweza kuwazia sehemu unayoishi bila urithi wowote? Fikiria, kwa mfano, kuhusu mahali ambapo wewe na wanafunzi wenzako mnakoishi. Mambo ya kale, ya sasa na ya usoni yanawakilishwaje? Ni vitu gani vinastahili kuhifadhiwa? Ni vitu gani vinavyoweza kubadilishwa na vingine? Ni vitu gani ambavyo thamani yake ikipotea haiwezi kurudishwa upya?

Dunia ina urithi wa kitamaduni na wa kiasilia. Katika sehemu unayoishi pengine umejionea eneo muhimu la kiakiolojia au mahali penye sanaa-miamba, makanisa, au mahali maarufu au patakatifu kwa sababu ya dini, au mji wa kihistoria. Sehemu hizi zinaitwa **urithi wa kitamaduni.** Pengine unaishi karibu na msitu au sehemu ya kupendeza sana ya pwani. Sehemu hizi zinaitwa **urithi wa kiasilia.** Urithi wa aina hii ni urithi usiosogezeka (yaani hauwezi kuhamishwa kwa urahisi). Vitu vinavyoweza kurithiwa kama vile sarafu, sampuli za kibotania, michoro, sanamu au sanaa za kiakiolojia ni **urithi unaosogezeka** (yaani unaweza kuhamishwa eneo moja hadi lingine).




*Urithi usiosogezeka: Taj Mahal, India.*
*© UNESCO/P. Leclaire*



*Urithi unaosogezeka: barakoa (maski) ya Kiafrika*
*©UNESCO/P. Leclaire*


© UNESCO 2004



## Harakati za wanafunzi za 2

## MAANA YA URITHI

### Lengo: Kuelewa maana, thamani na aina mbali mbali za urithi



| Majadiliano | Harakati darasani | Vipindi viwili | Lugha, historia, masomo ya jamii | Picha | Vitu vya kibinafsi |
|---|---|---|---|---|---|

### Urithi unaosogezeka

✓ Waonyeshe wanafunzi kitu ambacho unakimiliki (kwa mfano, mchoro, kito, pambo, mkeka, au kijisehemu cha nyungu,) ulichorithi kutoka kwa vizazi vya kale vya familia yako na ambavyo unavithamini. Waeleze vitu hivyo ni urithi wa kusogezeka. Je, ni urithi wa kitamaduni au wa *kiasilia?*

✓ Majadiliano

→ Je, ni kitu gani? Kwa nini unakithamini, kukitunza na kukihifadhi? Kama unataka kukitunza kiwe urithi wa *watoto* wako, utakilindaje?

→ Waulize wanafunzi walete vitu wanavyovithamini darasani siku ifuatayo. Buni makavazi ya muda darasani kwa kuweka vitu hivyo kwenye maonyesho na kuvijadili. Vitu hivi vina thamani gani kwa wanafunzi inayowafanya watake virithiwe na vizazi vijavyo?

✓Waeleze kuwa UNESCO husimamia mapatano mengine ya kimataifa yanayohusika na ulindaji wa urithi wa kitamaduni unaosogezeka *(Mapatano juu ya Kukataza, Kuzuia Uingizaji Kiharamu, Upelekaji Nchi za Nje, na Uhamishaji Umiliki wa Mali-tamaduni,* Novemba 14, 1970).



Orodha ya Marejeleo

### Urithi usiosogezeka

Eleza ya kuwa maeneo yaliyoandikwa kwenye orodha ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu ni ya urithi usiosogezeka, kumaanisha si rahisi kuuhamisha. Chagua mfano kutoka kwenye picha.



Picha


✓Majadiliano

→ Waulize wanafunzi kuwazia kuhusu maeneo ambayo wameyaona au kusoma juu yao (ya kitaifa na kimataifa) na waorodheshe habari na maana ya maeneo haya (mifano ya usanifu wa majengo, mimea na wanyama adimu)

→ Waulize wanafunzi *wafikirie* juu ya maeneo ya kiasilia ambayo wangetaka kuyadumisha kama yalivyo kwa siku za usoni. Eleza umuhimu wa kudumisha maeneo haya na wajadiliane darasani.



© UNESCO 2004



*Urithi usioshikika: wachezaji ngoma kutoka Burundi.*
*© UNESCO/M. Claude*

Urithi wa Ulimwengu na Kitambulishi

Urithi wa Ulimwengu na utalii

Orodha ya Marejeleo

Urithi wa Ulimwengu na mazingira

## ▲ Vitisho vinavyokabili uhai wa urithi wetu

Urithi wetu wa kitamaduni na wa kiasilia ni hafifu na umekabiliwa na tisho kubwa, hasa katika miaka mia iliyopita. Kwa mfano, wakati wa vita vya kwanza na vya *pili vya dunia, miji na majiji* mengi ya kale yaliangamizwa. Majengo ya kumbukumbu muhimu ya kitamaduni yaliangamia au kutoweka. Urithi wetu pia unakabiliwa na vitisho la ukuaji mkubwa wa miji, umaskini, majanga ya kiasilia, *nauchafuaji wa mazingira*. Uongezekaji wa utalii-halaiki pia unatisha kuangamia kwa majengo na maeneo mengi ya kumbukumbu. Mojawapo ya vitisho vikubwa vinavyokabili urithi huu ni kutojali kwa watu kuutunza.

Ili kukabiliana na vitisho hivi vilivyozuka baada ya vita viwili vikuu vya ulimwengu, Shirikisho la Mataifa (League of Nations) lilotangulia **Umoja wa Mataifa (United Nations)**, lilitafuta mbinu za kuulinda urithi huu. Shirikisho hili liliyaomba mataifa ya ulimwengu kushirikiana katika uhifadhi. Wakati **Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO)** lilipoanzishwa mwaka wa 1945, baada ya vita vya pili vya ulimwengu, kazi hii ilishika kasi kwa kuanzishwa kwa kampeini za *kuokoa* maeneo yenye umuhimu maalum na kuandikwa kwa mapatano ya kimataifa na mapendekezo ya kulinda urithi wa mwanadamu. Mojawapo ya mapatano haya yamebuniwa hasa kulinda urithi wa kitamaduni wakati wa *vita-yaani Mapatano ya Kulinda Mali-Tamaduni Iwapo Kutatokea Ugomvi wa Kutumia Silaha (au Mapatano ya Hague ya 1954)*

## Urithi wa Ulimwengu

Ni wangu, wako na wetu pia
Kwa hivyo acha tuutunze vyema, kwa mataifa ya kesho

Maji yaliyotulia ya Ziwa Victoria
Maporomoko ya maji ya Victoria na maji yanayovutia ya
Mto Danube na ndege wanaoishi humo na
Mito inayojipindapinda ya Mississippi na Missouri


Naangalia juu, na je naona nini?
Naona ardhi ya kupendeza na magofu ya Zimbabwe
Piramidi za kimiujiza za Misri katika nchi ya Farao


© UNESCO 2004

Naona kuta za kale za Jerusalem na Kuta Kuu ya Uchina
Natazama juu
Naona milima mikuu ya Drakensburg
Vilima vyenye ncha kali vya Genge ya Muchinga
Milima Himalaya na Urals ya Urusi
Nahesabu milima ya Rocky ya Canada na Kilimanjaro inayovutia

Kwa hivyo mimi, wewe na watu ulimenguni
Ulimwengu ni urithi wetu
Ni wako kuhifadhi
Usiangamize urithi wetu
Usiangamize mandhari na milima ya kupendeza
Usiangamize mbuga za wanyama na wanyama wa mwituni
Pia pori na misitu ya Congo na Amazon
Tafadhali okoa na hifadhi urithi wetu

Mauyaneyi Marebesa, Mwanafunzi, Zambia, Muungano wa Vijana Wanaohusika na Urithi, Victoria Falls, Zambia na Zimbabwe.



*Victoria Falls (Mosi-oa-Tunya), Zambia na Zimbabwe. © UNESCO/D. Reed*



# Uokoaji wa Urithi wa Ulimwengu


Juhudi za UNESCO za kwanza za kimataifa za kuokoa maeneo muhimu ya urithi, zilichochewa na uamuzi wa kujenga Bwawa la Aswan nchini Misri katika miaka ya hamsini. Mafuriko ya bonde la Mto Nile—ambalo lina hazina muhimu za ustaarabu wa Misri ya kale, hekalu za Abu Simbel—zilichochea hisia kali za kimataifa na kusababisha *jamii ya* ulimwengu kuchukua hatua za haraka za kulinda urithi huu. Kutokana na ombi la serikali za Misri na Sudan, UNESCO ilianzisha kampeini ya kimataifa ya kuokoa Abu Simbel mwaka wa 1959. Juhudi za UNESCO ziliungwa mkono na mataifa hamsini ambayo yalitoa mchango wa dola milioni themanini za kimarekani katika kipindi cha miaka kumi na nane cha *kampeini hiyo* ya kidharura ya uhifadhi.

Hekalu zilizokuwa katika Kisiwa cha Philae zilipambuliwa mawe kwa mawe na kujengwa upya katika kisiwa kilicho karibu cha Agilkia, mbali kabisa na mafuriko

© UNESCO 2004

ya Mto Nile. Hiki kilikuwa kitendo kigumu cha uhandisi wa kisasa. Ili kupatia nafasi majumba ya *ukumbusho*, majabali yalibomolewa kwa baruti, na mawe mazito yaliyoambuliwa yalirudishwa mahali pake kwenye kuta za hekalu. Mawe haya yalikuwa na uzani wa baina ya nusu tani na tani kumi na mbili. Karibu mawe elfu arubaini yalihamishwa. Kila jiwe liliandikwa nambari maalum ili kuhakikisha ya kuwa litawekwa mahali mwafaka katika eneo jipya.

Baada ya kujengwa kwa Bwawa la Aswan, Hekalu za Abu Simbel zingefunikwa kabisa na maji ya Mto Nile. Kupambuliwa na kuhamishwa kwa majengo haya ya kumbukumbu ilikuwa njia ya pekee ya kuokoa hekalu hizi (mfano wa urithi wa kitamaduni usiosogezeka). Wahifadhi wa urithi kote ulimwenguni hawapendelei uhamishi wa majengo ya kumbukumbu isipokuwa iwe ndiyo njia pekee ya kuokoa urithi kama ilivyokuwa kuhusiana na Abu Simbel.



*Majengo ya kumbukumbu ya Kinubi yakihamishwa kutoka Abu Simbel hadi Philae, Misri.*
*© UNESCO/NENADOVIC*

## ▲ Kampeini iliyofanikiwa ya Abu Simbel

Kampeini ya kuokoa Abu Simbel ilionyesha kuna maeneo ulimwenguni ambayo thamani yao kubwa ya kiulimwengu inawahusisha na kuwashughulisha watu wengi hata walio mbali na maeneo hayo. Kampeini hii pia ilisisitiza umuhimu wa kushirikiana na kuungana kwa mataifa mbali mbali katika uhifadhi wa urithi. Kufanikiwa kwa kampeni hii kulisababisha kampeini zingine za kimataifa za kiulinzi katika nchi zingine kama vile Venice, Italia; *Moenjodaro*, Pakistani; na Borobudur, Indonesia na kwengineko. Baadhi ya kampeini hizi bado zinaendelea, kwa mfano Mradi wa Ulinzi wa Kimataifa (International Safeguarding Programme) huko Angkor, Kambodia.




© UNESCO 2004



## ■ Harakati za wanafunzi za 3

## MAAJABU SABA YA ULIMWENGU

### Lengo: *Kuwazia dhana ya maeneo ya kipekee tangu kale hadi leo*



**Majadiliano**



**Harakati darasani**



**kimoja Kipindi**




**Historia, jiografia, masomo ya jamii**



***Ramani* ya Urithi wa Ulimwengu, Maelezo kwa ufupi**

Wazo la kubuni orodha ya maeneo muhimu ni la kale. Wagiriki wa kale walichukulia maajabu saba ya *ulimwengu kuwa:*

- → Piramidi za Misri
- → Bustani zinazoninginia za Babiloni
- → Hekalu ya Artemis ya Efeso
- → Sanamu ya Zeus ya Olympia
- → *Kaburi* kubwa la Halicarnassus
- → Sanamu ya Rhode
- → Mnara wa taa wa Alexandria



*Memphis na makaburi yake—Uwanja wa Piramidi kutoka Giza hadi Dahsur, Misri.*
*© UNESCO/F. Alcoceba*

Ingawa piramidi za Misri bado zingalipo, maajabu yale sita ya ulimwengu karibu yameshatoweka, na ishara hafifu tu katika rekodi za *kiakiolojia ndizo* zilizobaki.

Maajabu Saba ya Ulimwengu yalichukuliwa na Wagiriki kuwa mifano bora kabisa ya urithi wa kitamaduni wa ulimwengu wa Bahari ya Mediterania. Orodha ya Urithi wa Ulimwengu pia inahusisha maeneo ya kitamaduni na kiasilia ya sehemu zote za *ulimwengu*, na muhimu ni kwamba yanalindwa kisheria na *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu*. Katika karne zijazo tunatarajia kuokoa maeneo yote ya ulimwengu yaliyo na urithi tofauti na Maajabu Saba ya Ulimwengu.

✓ Waulize wanafunzi waandike orodha ya maeneo saba muhimu sana kwao—maajabu saba yao ya ulimwengu—na *walinganishe mapendekezo* yao na maeneo ambayo yameandikwa katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Jadili matokeo.



Ramani ya Urithi wa Ulimwengu



Maelezo kwa ufupi



© UNESCO 2004



Anwani



Urithi wa Ulimwengu na mazingira

## ▲ Kuandika mapatano ya kuokoa Urithi Wa Ulimwengu

Kutokana na matokeo bora ya kuokoa Abu Simbel, UNESCO kupitia kwa usaidizi wa mashirika yasiyo ya kiserikali, **Baraza la Kimataifa la Majengo na Maeneo ya Kumbukumbu (International Council on Monuments and Sites, ICOMOS)** lilianza kutayarisha mapatano ya *kulinda urithi* wa kitamaduni. Marekani na **Umoja wa Kimataifa wa Uhifadhi (World Conservation Union [IUCN]),** ambao unajulikana sasa kama Umoja wa Uhifadhi wa Ulimwengu (shirika lingine lisilo la kiserikali), yalipendekeza kuunganishwa kwa uhifadhi wa kiasilia na maeneo ya kitamaduni *kwa kubuni* kifaa kimoja cha kisheria. Pendekezo hili liliwasilishwa kwa kongamano la Umoja wa Mataifa juu ya Mazingira ya Binadamu (UNEP) huko Stockholm, Uswidi mnamo Septemba 1972. Kongamano hili lilifuatiliwa na lingine; mkutano mkuu juu ya sayari, au Rio Earth Summit, miaka ishirini baadaye (1992). Kwa hivyo, msingi ulitayarishwa wa kubuni kifaa cha kisheria cha kimataifa cha kulinda urithi wa kitamaduni na wa kiasilia ulio na thamani ya kiulimwengu. Kongamano la Stockholm liliikabidhi UNESCO jukumu la kufafanua mapatano yanayohifadhi asilia na utamaduni kwa kuwa UNESCO ndiyo wakala pekee wa kitaalamu katika Umoja wa Mataifa ambao una mamlaka mapana yanayohusu elimu, sayansi na utamaduni.


Miezi michache baada ya Kongomano la Stockholm juu ya mazingira, mnamo Novemba 16, 1972, *Mapatano ya Ulinzi wa Urithi wa Kitamaduni na Kisilia ya Ulimwengu (Convention Concerning the Protection of the World Cultural and Natural Heritage)* yalikubaliwa na kikao cha 17 cha **Kongomano la Kijumla la UNESCO** lilokutana katika makao makuu ya UNESCO huko Paris, Ufaransa.



### ■ Harakati za wanafunzi za 4

### KUELEZA MAANA YA URITHI NA UHIFADHI

### Lengo: Kufahamu vyema dhana za urithi na uhifadhi



| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Majadiliano** | **Harakati darasani** | **Vipindi viwili** | **Lugha** | **Sherehe** | **Makamusi** |

✓Waulize wanafunzi waeleze maana ya urithi na uhifadhi na waandike insha fupi juu ya dhana hizo mbili. Waulize wanafunzi iwapo wanajua mifano yoyote ya miradi ya uhifadhi katika sehemu wanazoishi na pia wapendekeze mingine.



© UNESCO 2004

**Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni**
**Organización de las Naciones Unidas para la Educatión, la Ciencia y la Cultura**
**Organisation des Nations Unies pour l'éducation, la science et la culture**
**Организация объединенных наций по вопросам образования, науки и культуры**
**منظمة الامم المتحدة للتربية والعلم والثقافة**

## Mapatano kuhusu ulindaji wa Urithi wa Utamaduni na Asilia wa Ulimwengu

***yaliyokubaliwa na Kongamano Kuu katika kikao chake cha 17 huko Paris, Novemba 16, 1972***

## Convención sobre la protección del patrimonio mundial, cultural y natural

***aprobada por la Conferencia General en su decimoséptima reunión Paris, 16 de noviembre de 1972***

## Convention concernant la protection du patrimoine mondial, culturel et naturel

***adoptée par la Conférence générale à sa dix-septième session Paris, 16 novembre 1972***


## Конвенция об охране всемирного культурного и природного наследия

**принятая Генеральной конференцией на семнадцатой сессии, Париж, 16 ноября 1972 г.**

## اتفاقية لحماية التراث العالمى الثقافى والطبيعى

أقرها المؤتمر العام فى دورته السابعة عشرة
باريس ، ١٦ نوفمبر/تشرين الثانى ١٩٧٢

© UNESCO 2004



*Makao makuu ya UNESCO, Paris, Ufaransa.*
*© UNESCO/ F. Dunouau*

*Mapatano* hayo ndiyo kifaa cha kwanza cha kimataifa kinachoelezea na kufafanua haja ya dharura ya kutambua na kulinda utajiri wetu wa kitamaduni na kimazingira uliyo na thamani isiyoweza kurudishwa ipoteapo.


*Mapatano* haya yanasisitiza ya kuwa ni wajibu wetu sote kulinda kwa hali na mali urithi wetu wa pamoja wa kitamaduni na kiasilia, kupitia kwa ushirikiano wa kimataifa.



## Dhana ya Urithi wa Ulimwengu

- → Uhifadhi wa urithi ulio na thamani ya kiulimwengu
- → Urithi wa kitamaduni na kiasilia
- → Urithi usiosogezeka
- → Uhifadhi wa urithi usioweza kurudishwa upoteapo
- → Uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu unategemea hatua za pamoja za kimataifa

© UNESCO 2004



## ■ Harakati za wanafunzi za 5

## UHIFADHI WA URITHI—SHERIA NA MAPATANO YA KIMATAIFA

### Lengo: Kuongeza utambuaji wa kutekeleza uhifadhi wa urithi wa kitaifa na wa kimataifa



| Utafiti | Harakati *darasani* | Kipindi kimoja | Lugha, historia, masomo ya kijamii | Ramani ya Urithi wa *Ulimwengu*, Mapatano ya Ulimwengu ya Urithi | Marejeleo |
|---|---|---|---|---|---|

✓Waweke wanafunzi katika makundi mawili na uwapatie majukumu ya kutafiti na kujibu maswali yafuatayo:

(a) *Uliza kundi la kwanza* kuchunguza iwapo na ni lini nchi yao ilikuwa taifa mwanachama wa *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* (tazama Ramani ya Urithi wa Ulimwengu na kuchunguza lini nchi tofauti zilipokuwa taifa wanachama wa *Mapatano*). Je, nia na faida za kujiunga na *Mapatano* ni zipi?

(b) Uliza kundi la pili kuorodhesha sababu ambazo ziliifanya jamii ya kimataifa (UNESCO) kuamua *kuyapitisha Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu.*

(c) Waulize wanafunzi wasome *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* na kuyaandika kwa muhtasari na kuyajadili.






Sehemu ya *sita ya kifungu* cha ishirini na saba cha *Mapatano*, kinasisitiza umuhimu wa kuhusisha Urithi wa Ulimwengu katika mipango ya *kielimu*. Sehemu hii inahimiza mataifa yote wanachama kujaribu kwa njia zote, hasa kupitia kwa mipango ya kielimu na ya kusambaza taarifa, kuwahimiza watu kuonea fahari na kuheshimu urithi wao wa kitamaduni na kiasilia.


Ahadi yetu

Elimu inayopendelea urithi wa kitamaduni na kiasilia ili tuelewe Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu, ambayo yanastahili kuingizwa kwenye mitaala ya kitaifa. Elimu ya aina hii inastahili kuhusisha ziara za maeneo (ya urithi) pamoja na vipindi vya ufundishaji kuhusu mada hii.

Wanafunzi waliohudhuria Muungano wa Kwanza wa Vijana wa Urithi wa Ulimwengu, Bergen, Norway.

*Je, kuna haja gani ya kulinda na kuhifadhi urithi kupitia kwa taasisi maalum na kubuni sheria za kitaifa iwapo hatutasisitiza sababu hizi kwenye fikra za watu wachanga?*

Bozo Biskupic, Waziri wa Utamaduni, Kroatia, wakati wa sherehe ya kuzindua Muungano wa Kwanza wa Vijana wa Uropa wa Urithi wa Ulimwengu, Dubrovnik



*Washiriki kwenye Muungano wa Vijana wanaohusika na Urithi wa Ulimwengu huko Bergen, Norway. © UNESCO*

© UNESCO 2004

Urithi wa Ulimwengu na kitambulishi

## ▲ Asilia na utamaduni zinahusiana kwa karibu

*Mapatano* hayo yana ubunifu wa kipekee kwani yanahusisha uhifadhi wa asilia na utamaduni. Sheria za kitaifa ni chache, na hakuna mapatano ya kimataifa yanayohusisha kwa ukamilifu uhifadhi wa utamaduni na asilia. Asilia na utamaduni zinategemeana: kitambulishi cha utamaduni wa watu tofauti hubuniwa katika mazingira wanamoishi. Uzuri wa majengo ya kumbukumbu na maeneo ya kupendeza hutokana na mazingira yao asilia. Isitoshe, maeneo ya kuvutia sana huonyesha ushahidi wa harakati za binadamu za karne nyingi ama yaliyo na umuhimu wa kidini, kitamaduni na kisanaa kwa wenyeji.

Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu

Nembo ya Urithi wa Ulimwengu huashiria uhusiano uliopo baina ya maeneo ya kitamaduni na kiasilia, na baina ya utamaduni na asilia.

## ▲ Urithi wa kitamaduni na wa kiasilia

Mapatano yanaeleza urithi wa kitamaduni katika kifungu cha kwanza, na urithi wa asilia katika kifungu cha pili.

Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu



*Wanafunzi wa mradi wa ASPnet wa Nepal wakifagia ngazi zinazoelekea kwenye Hekalu ya Bajrayogini.* © UNESCO



*Walinzi kamili wa urithi wa utamaduni wa miji ni raia wake. Watapatikana wapi? Wapo kila mahali, lakini mahali pakuanzia ni mashule. Mtandao wa UNESCO pia unaweza kutumika kwa shughuli hii na Mradi wa Shirikisho la Mashule (ASPnet) una maelfu ya mashule yanayohusika katika ushirikiano wa kimataifa.*
Ms Ase Kleveland, Waziri wa Utamaduni, Norway (1995)

Urithi wa Ulimwengu na kitambulishi

## ▲ Mandhari ya kitamaduni

Tangu mwaka wa 1992, Kamati ya Urithi wa Ulimwengu imeutambua mwingiliano wa utamaduni na asilia kama mandhari ya kitamaduni.

Anwani

Maeneo yafuatayo yameandikwa katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu: Mbuga ya kitaifa ya wanyama ya Tongariro, New Zealand; Mbuga ya kitaifa ya wanyama ya Uluru-Kata Tjuta ya Australia; Matuta ya mkingamo ya mpunga ya Ufilipino; Mandhari ya kitamaduni ya Sintra, Ureno; Lednice-Valtice, Jamhuri ya Cheki; Mandhari ya kitamaduni ya Hallstat-Dachsten/Salzkammergut, Austria; Pyrenees-Mont Perdu, Ufaransa/Uhispania; Costeria Amalfitana, Italia na Portovenere, Cinque Terre, na visiwa vya Palmaria, Tino na Tinetto, Italia na Mandhari ya Kilimo ya Oland Kusini, Uswidi. Habari zaidi kuhusu urithi wa mandhari ya kitamaduni zinapatikana kutoka kwa **Makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu** na katika tovuti.

© UNESCO 2004



*Mandhari ya kitamaduni ya Sintra, Ureno.* *© UNESCO*


# Utaratibu wa kuhifadhi Urithi wa Ulimwengu

Uhifadhi wa urithi wa ulimwengu ni utaratibu wa kila siku na unahusisha hatua kadhaa muhimu. Hatua ya kwanza ni kujitolea kwa nchi kuwa mataifa mwanachama wa mapatano ya uhifadhi wa ulimwengu na kuteua maeneo yaandikwe kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Vielelezo vifuatavyo vinaonyesha hatua za uteuzi.






**1** Nchi inakuwa taifa mwanachama kwa kuweka sahihi *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* na kuahidi kulinda urithi uliopo nchini wa kitamaduni na wa kiasilia.



**2** Taifa mwanachama hutayarisha orodha ya muda ya maeneo inayoyathamini ya kitamaduni na kiasilia .




**3** Taifa mwanachama huchagua maeneo kutoka kwa orodha ya muda yateuliwe kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu.

© UNESCO 2004




**4** Fomu iliyokamilishwa ya uteuzi inatumiwa Makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu.

**5** Makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu inahakikisha kuwa uteuzi umekamilika na kutumwa kwa Umoja wa Mataifa wa Uhifadhi (IUCN) na Baraza la Kimataifa la Majengo na Maeneo ya kumbukumbu (ICOMOS) kwa utathmini.






**6** Wataalamu wanatemebelea eneo kutathmini ulinzi na usimamizi wake.




**7** ICOMOS na/au IUCN zinatathmini uteuzi kwa kutumia vigezo vya urithi wa kitamaduni na wa kiasilia.






**8** ICOMOS na/au IUCN zinatayarisha ripoti ya utathmini.



**9** Wanachama saba wa Ofisi ya Urithi wa Ulimwengu wanapitia upya uteuzi na utathmini na kufanya mapendekezo kwa kamati.



**10** Uamuzi wa mwisho wafanywa na wanachama 21 wa Kamati ya Urithi wa Ulimwengu kuamua: kuliandika, kuahirisha uamuzi, au kulikataa ombi hilo.

© UNESCO 2004

## ▲ Orodha ya Urithi wa Ulimwengu: maeneo yenye thamani ya kiulimwengu

Baada ya kutia sahihi *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* nchi inakuwa taifa mwanachama na inaahidi kuhifadhi urithi wa kitamaduni na wa kiasilia ndani ya mipaka yake kwa faida ya vizazi vya sasa na vya baadaye. Taifa mwanachama likiyakubali *Mapatano*, litaanza kuteua maeneo ndani ya mipaka yake yaingizwe katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Mapendekezo ya awali kuhusu uteuzi wa eneo yanaweza kutolewa na kikundi cha watu wa eneo fulani, lakini uteuzi huo lazima utumiwe UNESCO kupitia kwa serikali. Kwanza, lazima taifa mwanachama liamue maeneo yatakayoteuliwa. Njia za uteuzi mara nyingi huitwa utambuzi. *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* huyahitaji mataifa wanachama kuanzisha orodha ya maeneo ya kitamaduni na kiasilia ambayo yanachukuliwa kuwa na thamani ya kiulimwengu katika nchi yao. Majina ya maeneo yaliyotambuliwa na taifa mwanachama kama maeneo ya urithi wa ulimwengu, yanastahili kupelekwa kwa makao ya UNESCO kama orodha ya muda.



Ukurasa wa harakati za wanafunzi. Uteuzi wa maene ya kitamaduni na kiasilia

Wakati taifa mwanachama linapoamua kuteua eneo fulani, hatua hii hukamilika kwa kujaza fomu maalum ya kuteua. Taifa mwanachama lazima litoe sababu za kuonyesha umuhimu wa eneo hilo zinalolifanya kustahili kuandikwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu, na pia kutoa mifano dhahiri kuonyesha kuwa eneo hilo linalindwa kikamilifu na kusimamiwa vyema.

Ni muhimu kuchanganua jinsi eneo lililochaguliwa linavyolingana na maeneo mengine ya sampuli hiyo. ICOMOS na/au IUCN hutathmini uteuzi huo na kutoa mapendekezo kwa Kamati ya Urithi wa Ulimwengu ambayo hutoa uamuzi wa mwisho wa maeneo ambayo yataandikwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu.



Maelezo kwa ufupi

Kufikia Mai 2004, maeneo 754 yalikuwa yameshaandikwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu—maeneo 582 ya kitamaduni, 149 ya kiasilia na 23 yanayohusisha maeneo yaliyo na sifa za kitamaduni na kiasilia pamoja katika nchi 129.

## ▲ Mkakati wa kiulimwengu unaohakikisha Orodha ya Urithi wa Ulimwengu sawazishi na wakilishi




Ramani ya Urithi wa Ulimwengu

Kamati ya Urithi wa Ulimwengu huhakikisha kuwa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu yamegawanywa vyema katika bara zote—Afrika, mataifa ya Kiarabu, Bara Hindi, Visiwa vya Bahari ya Pacifik, Uropa, Marekani ya Kaskazini, Marekani ya Kusini na Karibea. Katika mwaka wa 1944 Kamati ya Ulimwengu ya Urithi iliamua kuhakikisha kuwa orodha inahusisha anuwai za majimbo, utamaduni, na uasilia na kuukubali 'Mkakati wa kiulimwengu unaohakikisha Orodha ya Urithi wa Ulimwengu sawazishi na wakilishi' (Global Stratey for a representative and balanced World Heritage List).

*Nitawaambia wenzangu vile ninahisi sasa. Nahisi ya kuwa hakuna taarifa ya kutosha kuhusu urithi wa Kiafrika.*

Mwanafunzi wa Msumbiji, Muungano wa Vijana Wanaohusika na Urithi wa Ulimwengu, Victoria Falls, Zambia/Zimbabwe



## ■ Harakati za wanafunzi za 6

# KUBUNI KIELELEZO CHA ENEO LA URITHI WA ULIMWENGU

## Lengo: Kuhamasisha wanafunzi kuwa na mbinu za ubunifu na kujifunza kikamilifu kuhusu maeneo ya Urithi wa Ulimwengu

|  |  |  |  |  |  |
|---|---|---|---|---|---|
| Mazoezi | Harakati darasa au harakati nje ya darasa | Vipindi kadhaa | Hesabu, sanaa, historia, jiografia | Picha | Ubao, gundi, udongo |


✓ Waonyeshe wanafunzi wako picha. Waulize wachague moja au kadhaa za maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na watengeneze kielelezo. Mwalimu wa hesabu anaweza kueleza jinsi ya kutengeneza kielelezo chenye vipimo (scale model). Mwalimu wa sanaa au mwanasanaa wa eneo hilo au msanifu majengo anaweza kushauri jinsi ya kuunda kielelezo hicho. Mwalimu wa historia anaweza kushauri kuhusu uhakika wa kihistoria. Baada ya kumaliza kuunda kielelezo hicho chenye vipimo, au vielelezo, wanafunzi wanaweza kuandaa maonyesho na kuwakaribisha wazazi au wanajamii.

*Kielelezo chenye vipimo cha Ukuta Mkuu wa China.*
© UNESCO





© UNESCO 2004



## ■ Harakati za wanafunzi za 7

# KUTAMBUA MAENEO YA URITHI KATIKA SEHEMU UNAYOISHI

## Lengo: Kutambua maeneo ya urithi katika sehemu unayoishi



**Utafiti** | **Harakati darasani** | **Kipindi kimoja au viwili** | **Jiografia, *historia*** | **Ukurasa wa harakati za wanafunzi: kutambua maeneo ya Urithi wa Ulimwengu katika sehemu unayoishi Ramani ya Urithi wa Ulimwengu Maelezo kwa ufupi.**

✓ Tumia ukurasa wa harakati za wanafunzi na umpatie kila mwanafunzi ukurasa ikiwezekana.

Waulize wanafunzi waorodhesha maeneo kumi ya Urithi wa Ulimwengu yaliyo katika nchi yao au karibu na nchi yao.

Je, nchi yako imetia sahihi *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu*?

Je, ni taasisi au mamlaka gani yanayohusika kwa kutekeleza *Mapatano* katika nchi yako (urithi wa kitamaduni na wa kiasilia)?

Kuna uhusiano gani baina ya nchi yako na UNESCO? Je, kuna tume ya kitaifa ya UNESCO katika nchi yako?



© UNESCO 2004



Ramani ya Urithi wa Ulimwengu

Ramani ya Urithi wa Ulimwengu inaonyesha *orodha ya mataifa* wanachama wa *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* na mahali maeneo 754 yalipo ambayo tayari yameorodheshwa.

Tafuta maeneo kumi ya Urithi wa Ulimwengu yaliyo ndani au karibu na nchi yako na uandike majina yao na uonyeshe yalipo kwenye visanduku vilivyo hapo chini. Onyesha iwapo *maeneo haya ni* ya kitamaduni, kiasilia au yanahusisha sifa za kiasilia na kitamaduni.



Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu

Jadilianeni matokeo:

| Nambari | Mwaka ambao eneo *hilo* liliandikwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu | Taifa *mwanachama* | Jina la eneo la Urithi wa Ulimwengu | Aina ya eneo (la kitamaduni, la kiasilia, au lenye sifa za kiasilia na kitamaduni pamoja) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| 6 | | | | |
| 7 | | | | |
| 8 | | | | |
| 9 | | | | |
| 10 | | | | |

# Vigezo vya kuchagua maeneo ya Urithi wa Ulimwengu

## Ujumbe maalum kwa walimu kuhusa vigezo vya Urithi wa Ulimwengu



Orodha ya Marejeleo

Kigezo ni sifa ya kimsingi ya uhifadhi wa urithi wa kiulimwengu na kinapaswa kikumbukwe wakati mnapofundisha juu ya Urithi wa Ulimwengu.

Ustawishaji wa Orodha ya Urithi wa Ulimwengu ni shughuli ngumu kwa jumuiya ya kimataif. Swala hasa ni, utafikiaje uamuzi kwamba eneo moja au majengo ya kumbukumbu ya eneo fulani yanastahili yawe sehemu za urithi wa ulimwengu? Kwa ufupi, ni sifa gani ya kipekee iliyo katikika eneo la kitamaduni au la kiasilia inayotambuliwa kama thamani ya kiulimwengu?


Mwongozo uitwao *Operational Guidelines for the Implementation of the World Heritage Convention* umeendelezwa na kamati ya Urithi ya Ulimwengu kwa miaka mingi. Kamati inaeleza jinsi ya kuteua eneo litakaloandikwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu na vigezo vitakvyozingatiwa.

## ▲ Vigezo vya kuchagua maeneo ya urithi wa kitamaduni




Mwongozo huu unahusisha vigezo sita vinavyopaswa kutumiwa katika uchaguzi wa urithi wa kitamaduni wa majengo ya kumbukumbu, majengo ya kipekee na maeneo mengine yanayostahili kuchukuliwa kama sehemu za Urithi wa Ulimwengu.

Maeneo ya kitamaduni yaliyoteuliwa yanahitaji:




**(i)** kuwakilisha kazi bora inayodhihirisha ubunifu wa hali ya juu

*Tassili n'Ajjer, Algeria.*
*© UWIG/OPNT*



Great Zimbabwe National Monument, Zimbabwe

**(ii)** kuonyesha kuathiriana kwa muda mrefu kwa mambo yanayofaidi jamii, hasa katika eneo la kitamaduni, kuhusu maendelo ya usanifu mijengo au teknolojia, sanaa za kumbukumbu, upangaji miji au upambaji mandhari.



**(iii)** kuonyesha ushahidi wa kipekee au usio wa kawaida wa utamaduni na desturi au ustaarabu uliopo au ulioangamia; au

*Jelling Mounds, Runic Stones and Church, Denmark.*
*© UNESCO*



Brasília, Brazil

**(iv)** yawe na mifano bora ya mijengo au nyumba iliyosanifiwa au kifaa cha kiteknolojia cha kielelezo au mandhari ya kupendeza zinazoonyesha kipindi muhimu cha historia ya binadamu; au

© UNESCO 2004

Jesuit Missions of the Chiquitos, Bolivia

Memphis na makaburi yake na eneo la piramidi kutoka Giza hadi Dahshur, Egypt

**(v)** *yaonyeshe mfano* bora wa makaazi ya binadamu au matumizi ya ardhi ambayo


yanawakilisha utamaduni (au tamaduni) hasa wakati yanakabiliwa na vitisho vitakavyosababisha mabadiliko ya kudumu; au

**(vi)** kuhusisha matukio au desturi, na mawazo au mila au kazi za kisanaa na kifasihi za hali ya juu (Kamati inasisitiza kuwa kigezo hiki kinaweza kuhalalishwa kwa sababu za kipekee na *kuhusishwa na vigezo vingine* vya kitamaduni au vya kiasilia).

Ni muhimu kutambua uhalisi wa urithi wa kitamaduni na ulinzi wake pamoja na usimamizi.


## ▲ Vigezo vya kuchagua maeneo ya kiasilia ya Urithi wa Ulimwengu

Mwongozo endeshaji unahusiha vigezo vinne vifuatavyo vya kuchagua maeneo ya kiasilia yenye thamani.



*Eneo la Messel Pit Fossil, Ujerumani.*
*© UNESCO*

**(i)** Maeneo yawe ni mifano bora inayowakilisha hatua muhimu za historia ya dunia na inayohusisha rekodi ya uhai, taratibu muhimu ya kijiolojia inayoathiri miundo ya *ardhi, ama miundo* muhimu ya kijiomofiki na kifiosografia; au



*Mfumo wa Uhifadhi wa mwamba tumbawe , Belize.*
*© UNESCO*

**(ii)** Yawe ni mifano muhimu inayoendelea ya kiikolojia na kibayolojia yanayoadhiri mabadiliko na maendeleo ya nchi kavu, maji yasiyo na chumvi, *pwani na mfumo* wa ikolojia baharini na jamii za mimea na wanyama; au

Great Barrier Reef, Australia

**(iii)** Yawe na *finomena ya kiasilia ya* kuvutia au yawe maeneo yenye umuhimu wa kiujumi

**(iv)** Yawe yana makazi asilia muhimu ambayo yanahifadhi anuwai ya kibayolojia (biodiversity), pamoja na makazi yaliyo na spishi zenye thamani ya *kiulimwengu* zilizo hatarini.

Rio Platano Biosphere Reserve, Honduras

Jambo lenye umuhimu sawa *ni ukamilifu* wa urithi wa asilia na ulinzi na usimamizi wake.

## ▲ Vigezo vya kuteuwa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu yanayojumulisha sifa za kitamaduni na za asilia

Maeneo yaliyo na sifa za kitamaduni na asilia yana thamani ya juu na kwa hivyo yanaingizwa kwenye Orodha *ya Urithi* wa Ulimwengu kutokana na vigezo



© UNESCO 2004

vinavyojumlisha sifa hizi mbili. Hivi sasa kuna maeneo ishirini na matatu yaliyo na sifa za kitamaduni na asilia kwa pamoja (kwa mfano, Hifadhi ya Kihistoria ya Machu Picchu huko Peru na eneo la Laponia huko Uswidi).



Maelezo kwa ufupi

## ▲ Utumiaji wa vigezo

Vigezo hutekelezwa kwa udhati kuepuka hali ya Orodha ya Urithi wa Ulimwengu kuwa ndefu zaidi au kuifanya iwe orodha ya kawaida ya maeneo yote ambayo mataifa yangependa yaorodheshwe.



Urithi wa Ulimwengu na Kitambulishi

**Mataifa yote yana maeneo yanayovutia watu na yenye umuhimu wa kitaifa ambayo mataifa husika huyaonea fahari. *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* yanahimiza yatambuliwe na yalindwe iwapo yatawekwa kwenye orodha au la.**



© UNESCO 2004

## Harakati za wanafunzi za 8

## UTAMBUAJI WA MAENEO YA URITHI WA ULIMWENGU

### Lengo: Kujifunza kutambua maeneo ya kijiografia na aina tofauti za maeneo ya Urithi wa Ulimwengu

Utafiti — Harakati *darasani* — Vipindi kadhaa — Ukurasa wa harakati za wanafunzi: utambuaji wa maeneo ya urithi — Maelezo kwa ufupi Ramani ya Urithi wa Ulimengu picha

✓ Tumia ukurasa wa harakati za wanafunzi, kila mwanafunzi apewe ukurasa wake ikiwezekana.

✓ Waulize wanafunzi waoanishe maeneo ya *Urithi wa Ulimwengu* yanayo-onyeshwa kwenye ramani iliyoambatishwa (iliyo na herufi A hadi J) na maeneo yaliyoorodheshwa hapo chini (yaliyo na nambari 1 hadi 10). Wanafunzi waonyeshe iwapo *maeneo hayo ni* ya kitamaduni, kiasilia au ni ya mchanganyiko wa kitamaduni na kiasilia.

✓ Waulize wanafunzi wabadilishane majibu ili wajisahihishe. Je wanafunzi wamefuzu? Wapatie washindi zawadi kama vile mapambo ya kubandika ya Patrimonito.

Baada ya wiki mbili au tatu ya mafundisho *darasani*, *rudia* zoezi hili kwa kuongeza maeneo kumi zaidi kwenye ramani. Mazoezi haya yanaweza kurudiwa mara kadhaa.



## Majibu

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Chile | Mbuga ya *Taifa ya Rapa Nui* (Kisiwa cha Easter) |
| 2. | Cuba | Havana ya kale na ngome zake |
| 3. | Mexico | Hifadhi ya Nyangumi ya El Vizcaino |
| 4. | Ghana | Ngome na Kasr, Volta, Accra Kuu, Maeneo ya Kati na Magharibi |
| 5. | Japan | Minara ya kumbukumbu ya Kyoto ya kale (miji ya Kyoto, Uji na Otsu) |
| 6. | Jordan | Petra |
| 7. | France | Mont-Saint–Michael na ahuba yake |
| 8. | China | Mlima Taishan |
| 9. | Tanzania | Mbuga ya Wanyama ya Kitaifa ya Serengeti |
| 10. | Niger | Hifadhi za wanyama za Air na Tenere |




*Hifadhi za wanyama za Air na Tenere.*
*© IUCN/J. Thorsell*

© UNESCO 2004

Ramani ya ulimwengu inaonyesha maeneo kumi yaliyo katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu.

Oanisha maeneo ya Urithi wa Ulimwengu yanayoonyeshwa kwenye ramani (yaliyo na herufi A *hadi* J) na orodha iliyoandaliwa (yenye nambari 1 hadi 10). Andika majina ya maeneo haya na ma*jimbo* yao na uonyeshe iwapo ni maeneo ya kitamaduni, ya kiasilia au ya mchanganyiko. Bahati nzuri!

| **Herufi** | Oanisha na nambari sahihi (1 hadi 10) | Jina la eneo la Urithi wa Ulimwengu | Nchi mwanachama | Aina ya eneo (ya kiasilia ya kitamaduni, au ya mchanganyiko wa kitamaduni na kiasilia) |
|---|---|---|---|---|
| **A** | | | | |
| **B** | | | | |
| **C** | | | | |
| **D** | | | | |
| **E** | | | | |
| **F** | | | | |
| **G** | | | | |
| **H** | | | | |
| **I** | | | | |
| **J** | | | | |


J
I
G
H
F
E
D
B
A
C

## ■ Harakati za wanafunzi za 9

## UELEWAJI WA VIGEZO VYA KUAMULIA MAENEO YA URITHI WA ULIMWENGU

### Lengo: Kuelewa vyema vigezo vinavyotumika kuamua maeneo yatakayoandikishwa kwenye orodha ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu



**Mazoezi**




**Harakati darasani**



**Vipindi viwili au zaidi**



**Jiografia**



**Ukurasa wa harakati za wanafunzi: Uelewaji wa vigezo vya Urithi wa Ulimwengu, Ramani ya Urithi wa Ulimwengu, Maelezo kwa ufupi**

Vigezo vilivyoamuliwa na kamati ya Urithi wa Ulimwengu lazima vitoshelezwe kabla eneo halijaingizwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu.



Maelezo kwa ufupi

✓ Waweke wanafunzi katika makundi madogo na uwaulize wachunguze Ramani ya Urithi wa Ulimwengu na Maelezo kwa ufupi na waandike kwenye kurasa hizo, *eneo moja* kwa kila jimbo kulingana na kila kigezo (maeneo mengi yaliyo kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu yaliandikwa *kutokana na* zaidi ya kigezo kimoja).

✓ Kwa maeneo yaliyo na sifa zaidi ya moja, taja eneo moja au mawili kwa kila jimbo na uonyeshe vigezo vilivyotumiwa kwa kila eneo.

✓ Jadili *matokeo* na wanafunzi.

| Maeneo ya kitamaduni | Kigezo (i): Kazi bora inayoonyesha ubunifu | Kigezo (ii): Ubadilishanaji wa mambo yanayodhaminiwa na jamii | Kigezo (iii): Ushahidi wa *kipekee* utamaduni, mila au ustaarabu ulio hai au uliotoweka | Kigezo (iv): Mifano ya hali ya juu ya majengo, au usanifu mijengo, au teknolojia ya kipekee, au mandhari ya kupendeza ya nchi | Kigezo (v): Mifano ya hali ya juu ya makazi ya kitamaduni au utumizi wa kitamaduni wa ardhi | Kigezo (vi): Kinahusiana na matukio ya utamaduni unaoendelea, mawazo, mila, sanaa, na fasihi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Afrika | | | | | | |
| Marekani ya Kusini na Karibea | | | | | | |
| Mataifa ya Kiarabu | | | | | Mji wa kale wa Ghadames (Libya, Jamahariya ya Kiarabu) | |
| Bara Hindi na visiwa vya Pasifiki | | | | | | |
| Uropa na Marekani ya Kaskazini | | | | | | |



| Maeneo ya kitamaduni | (i): Hatua muhimu za historia ya dunia | Kigezo (ii): Miundo ya kiekolojia na kibayolojia inayoendelea | Kigezo(iii): Finomena ya kiasilia ya kuvutia au maeneo yenye umuhimu wa kiujumi | Kigezo (iv): Makazi asilia muhimu ya uhifadhi wa anuwai ya kibayolojia wa aina mbali mbali |
|---|---|---|---|---|
| Afrika | | Mbuga ya Kitaifa ya Wanyama Manovo-Gounda ya St. Floris (Jamhuri ya Afrika ya Kati) | | |
| Marekani ya Kusini na Karibea | | | | |
| Mataifa ya Kiarabu | | | | |
| Bara Hindi na visiwa vya Pacific | | | | |
| Uropa na Marekani ya Kaskazini | | | | |

| Eneo | Eneo lenye sifa zaidi ya moja | Vigezo vya Urithi wa kiasilia (i), (ii), (iii) na/au (iv) | Vigezo vya urithi wa kitamaduni (i), (ii), (iii), (iv), (v) na/au (vi) |
|---|---|---|---|
| **Afrika** | | | |
| **Marekani ya Kusini na Karibea** | | | |
| **Mataifa ya Kiarabu** | | | |
| **Bara Hindi na visiwa vya Pasifiki** | | | |
| **Uropa na Marekani ya Kaskazini** | *Mbuga* ya Kitaifa ya Wanyama ya Goreme na Maeneo ya Miamba ya Cappadocia, Uturuki. | iii | i, iii, v |





*Mbuga ya Kitaifa ya Wanyama ya Goreme na Maeneo ya Miamba ya Cappadocia, Uturuki.*
*© UNESCO/D. Roger*



## ■ Harakati za wanafunzi za 10

## UTEUZI WA MAENEO YA KITAMADUNI NA KIASILIA

### Lengo: Kuzielewa hatua za kuteua maeneo yatakayoongezwa kwenye orodha ya urithi wa kulindwa



**Mazoezi**




**Harakati darasani**



**Kipindi kimoja au zaidi**



**Lugha na sanaa**



**Ukurasa wa harakati za wanafunzi: Uteuzi wa maeneo ya kitamaduni na asilia, Miongozo ya *wanafunzi***

✓ Tumia ukurasa wa *harakati za wanafunzi na miongozo* kuwahusisha wanafunzi kuteua maeneo ya mitaa na majimbo yatakayoandikwa kwenye orodha ya kitaifa.

✓ Waweke wanafunzi katika makundi madogo. Kila kikundi kitateua eneo moja la mtaa.

✓ Orodha ya kila kikundi cha wanafunzi inaweza kutumika kama bango ya ukutani au orodha hizo zinaweza kuwekwa pamoja kama kitabu. Tuma nakala ya kijitabu hiki kwa mamlaka ya mtaa au jimbo lenu pamoja na salamu kutoka kwa wanafunzi na maoni ya mkutano wenu na *kamati ya kitaifa ya urithi*.



Harakati za wanafunzi za 11



UNESCO 2004

## Mwongozo wa wanafunzi

## Kuteua eneo la nchi ili liandikwe katika orodha au rejista ya kitaifa ya urithi

Nchi yako intayarisha orodha ya kitaifa ya maeneo ya urithi wa kitamaduni na kiasilia. Darasa lako limeulizwa kuchukua hatua za kuteua eneo moja au zaidi za kitamaduni au kiasilia yaandikishwe kwenye orodha hii.

### *Mwongozo wa kutayarisha uteuzi*

Tumia fomu iliyoambatishwa kutayarisha uteuzi na utilie maanani mambo yafuatayo:

Sehemu ya ***maelezo*** itahusisha:

- → maelezo ya eneo na sura ya nchi (k.m. milima, mabonde, mito, ziwa, wanyama, mimea, na aina za makazi, usanifu wa mijengo ya kitamaduni, n.k.)
- → historia ya eneo
- → ramani
- → picha (ziambatishwe)
- → orodha ya marejeleo mafupi yanayoonyesha chanzo cha taarifa kuhusa eneo hilo.

Sehemu ya kuhalalishwa kwa eneo hilo kuandikwa kwenye orodha sharti izingatie:

- → sababu ambazo zinalifanya eneo hili kuwa na umuhimu wa kitaifa. Iwapo nchi yako ina vigezo vya kuamua kama eneo lina umuhimu wa kitaifa, vitumie wakati huu.

Sehemu ya ***uhifadhi wa eneo*** inastahili kuwa na:

- → maelezo juu ya anayeshughulikia na kutunza eneo hilo. Je, wenyeji ndiyo wanaohifadhi eneo wenyewe au kuna shirika la mtaa au la kijimbo au la kitaifa linalohusika? Je, watu wanaotunza eneo lenyewe wanao uwezo wa kulihifadhi? Wana pesa za kutosha na utaalamu unaohitajika? Zipo sheria za kulinda eneo lenyewe?

Eneo litakalolinganishwa ***na maeneo mengine*** linastahili kuwa na:

- → taarifa za maeneo mengine kama hayo nchini na katika sehemu zinazopakana na nchi yenu

- → tathmini ya hali ya sasa ya uhifadhi wa eneo, ikilinganishwa na maeneo ya aina hiyo ya kitaifa.

Je, eneo hilo linakabiliwa na *hatari ya kupungua* thamani kiasi ya kuwa haliwezi kuokolewa? Kwa mfano, kama ni eneo la kiasilia, uliza iwapo baadhi ya mimea au wanyama wako katika hatari ya kuangamia.

Eneo hilo liko nchi gani?..........................................................................................................

Majina ya watu waliyotayarisha *uteuzi*...............................................................................

Tarehe:... ..................................................................................................................................

**Jina la eneo**

**Sifa za kijiografia za eneo hilo**

## Maelezo ya eneo

**Sababu za kuhalalishwa kwa eneo *hilo* kuandikwa kwenye orodha ya urithi wa kiasilia na kitamaduni**

**Vigezo vilivyotoshelezwa:**

**Uhifadhi wa eneo:**

**Ulinganishi na maeneo mengine:**

# Kamati ya Ulimwengu ya Urithi na Makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu



*Kamati inayohusika na Urithi wa Ulimwengu ikiwa kazini.*
*© R. Milne*

Uamuzi wa maeneo ambayo yatahusishwa au kuandikwa kwenye orodha ya urithi hufanywa na Kamati ya Ulimwengu ya Urithi.

Kamati hii inayokutana mara nne kwa mwaka ina majukumu makuu manne:

→ Kueleza Urithi wa Ulimwengu kwa kuchagua maeneo ya kitamaduni na kiasilia yatakayoandikwa kwenye orodha. Kamati hii inasaidiwa katika jukumu hili na ICOMOS na IUCN ambao hukagua uteuzi kutoka mataifa wanachama kwa uangalifu na kisha kuandaa ripoti ya mateuzi hayo. Makao ya Kimataifa ya Kuchunguza Utunzaji na Urekebishaji wa Mali-tamaduni (The International Centre for the Study of the Preservation and Restoration of Cultural Property, [ICCROM]) pia hushauri kamati hiyo (kwa mfano, kuhusu mafunzo ya urithi wa kitamaduni na mbinu za uhifadhi.)






→ Kukagua ripoti za hali ya uhifadhi wa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na kuwashauri mataifa wanachama kuchukua hatua mahsusi za uhifadhi wakati maeneo hayasimamiwi na kulindwa vyema.

→ Kuamua iwapo maeneo yanayokabiliwa na vitisho yanaweza kuongezwa kwenye orodha ya maeneo ya urithi yaliyo hatarini baada ya kushauriana na taifa mwanachama linalohusika.


→ Kusimamia hazina ya Urithi wa Ulimwengu na kuamuwa usaidizi wa kiufundi na kifedha utakaotengewa mataifa ambayo yameomba msaada wa kuhifathi urithi wao.

Ofisi kuu ya utekelezaji wa *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* huandaliwa na UNESCO. Makao haya husaidia mataifa wanachama katika utekelezi wa *Mapatano* na hupendekeza na kutekeleza maamuzi ya Kamati ya Ulimwengu ya Urithi.




© UNESCO 2004

## ■ Harakati za wanafunzi za 11



## MKUTANO WA KAMATI YA KITAIFA YA URITHI

### Lengo: Kuelewa hatua za kuchukua uamuzi wa kuteua maeneo ya urithi


Uigizaji


Darasa


Harakati nje ya darasa


Vipindi kadhaa


Lugha, jiografia, masomo ya jamii

Katika harakati hii wanafunzi wataigiza nafasi za wanachama wa Kamati ya Kitaifa ya Urithi. Kamati itachunguza maeneo ya mtaa na ya kitaifa yanayopendekezwa na darasa lako litaamua kama yanastahili kuhifadhiwa au la.

✓ Chagua mwenyekiti mmoja, manaibu wawili wa wenyekiti na mwandishi. Hakikisha kuwa kuna usawazishi wa wavulana na wasichana. Wanafunzi hawa wanne watatayarisha majadiliano na kuongoza mjadala.


Harakati za wanafunzi




✓ Waweke wanafunzi wengine katika makundi. Kila kikundi kitachunguza eneo moja halafu watoe mapendekezo kwa kamati nzima (iwapo eneo hilo litahifadhiwa na kuhusishwa katika orodha ya kitaifa ya urithi).

✓ Chunguza fomu ya uteuzi na uangalie yafuatayo:

(a) Je, eneo lina thamani kwa mtaa, jimbo fulani, taifa au ya kimataifa?
(b) Je, eneo limehifadhiwa vizuri?
(c) Je, kuna ulinzi wa kutosha wa kisheria wa eneo hilo?
(d) Je, kuna mipango ya kutosha ya usimamizi na uhifadhi wa eneo?
(e) Je, wenyeji wa eneo hilo wameshauriwa kama wanakubaliana na uteuzi wa eneo hilo?

✓ Wasilisha utathmini wa makundi katika majadiliano. Amua ni maeneo gani yana umuhimu wa kitaifa. Waulize wanafunzi wapige kura kuamua maeneo yanayostahili kuongezwa kwenye orodha ya kitaifa ya urithi. Kisha uwaulize iwapo baadhi ya maeneo haya yanastahili kuongezwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu.


© UNESCO 2004



## ■ Harakati za wanafunzi za 12

# MAKAO YA KIHISTORIA YA SANTA CRUZ DE MOMPOX, KOLOMBIA

**Lengo: Kuelewa vyema hatua mbali mbali zinazotekelezwa za kuteua eneo la kuingizwa katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu**



Ziara | Harakati darasani | Vipindi kadhaa | Historia na jiografia | Picha, Maelezo kwa ufupi, Ramani ya Urithi wa Ulimwengu

Ili wanafunzi waelewe vizuri hatua zinazochukuliwa katika uteuzi na uandikishaji wa eneo katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu, tutachunguza eneo lililoteuliwa na Kolombia katika mwaka wa 1994 na kuorodheshwa mwaka wa 1995.

✓ Wasilisha habari ifuatayo kwa wanafunzi.

## Kuhalalisha hatua ya kuweka eneo hili katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu

Wakati wa kipindi cha ukoloni wa Wahispania huko Marekani ya Kusini, kulitokea ufanisi wa *kipekee* wa kisanaa huko Mompox ambao haupatikani katika maeneo mengine.

Aina ya urithi wa kitamaduni (tazama sehemu ya kwanza ya *Mapatano*): Majengo

## Historia

Mompox ilianzishwa katika mwaka wa 1540 na Juan de Santa Cruz, gavana wa Cartagen, ambaye alilipatia eneo hili jina lake. Mji huu ulikuwa kando kando ya Mto Magdalena na ulikuwa na umuhimu mkubwa wa usafirishaji wa watu na bidhaa. Usafirishaji baina ya bandari ya Cartagena na bara ulitumia mito na barabara za kuingia bara zilikutania hapo. Ukuaji wa Mompox uliharakishwa na kuibuka kwa tabaka la wakoloni ambao waliajiriwa na utawala wa ukoloni na kupendelewa katika umiliki ardhi na waliwachukua wahindi wawafanyie kazi kama mahabusu. Wahindi walinyanganywa mashamba yao na kulazimishwa kuishi katika vitongoji maalum *vilivyotengwa*. Hali hii pamoja na hali duni ya anga na mazingara ziliadhiri ukulima na kusababisha mji huu usipanuke haraka. Hali hii iliwavutia watu waovu ambao walifaidika na biashara ya magendo. Ukuaji wa mji huu ambao ulitokea wakati wa ukoloni ulitokana na kikundi cha matajiri waliohamia hapo na kutajirika kutokana na ukulima na biashara. Wengine walikuja Mompox kutoka Cartagena pamoja na mafundi wao wenye ujuzi tofauti kutimiza mahitaji yao. Makasisi na viongozi wa dini tofauti pia waliunda kikundi kingine cha watawala.



© UNESCO 2004

## Usimamizi na ulinzi

Hali ya kisheria: Umiliki umegawanwa baina ya watu binafsi, taasisi, Kanisa Katoliki na serikali za mitaa. Makao haya ya kihistoria yaliorodheshwa kuwa Eneo la Kumbukumbu la Kitaifa na mji umesimamiwa na sheria za ujenzi za munispaa tangu mwaka wa 1970.

Usimamizi: Hakuna mpango au usimamizi wa makao haya ya kihistoria. Hata hivyo, sheria kali ya ujenzi na kanuni za miji zinahakikisha usimamizi unaofaa.

## Uhifadhi na uhalisia

Uhifadhi: Kazi kubwa ya kurekebisha na uhifadhi imetekelezwa katika miongo kadhaa iliyopita. Makao haya ya kihistoria yamehifadhiwa vizuri. Wamiliki wa kibinafsi wanaionea fahari mali yao waliyoitunza bila msaada kwa serikali.

Uhalisia: Mompox iliupoteza umuhimu wake wa kiuchumi kwa kiasi kikubwa katika karne ya kumi na tisa na mji huu umekosa kushughulikiwa kimaendeleo. Kwa hivyo makao yake ya kihistoria hayajaadhiriwa kama miji mingine ya Marekani ya Kusini. Mpango wa awali wa mabarabara umehifadhiwa na hata vifaa vya ujenzi. Muundo na vifaa vya makao haya ya kihistoria ni halisi.

## Utathmini wa ICOMOS



ICOMOS iliutembelea mji wa Mompox mnamo Februari 1995 na kupendekezea Kamati ya Urithi ya Ulimwengu kuwa uandikishwe kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu kufuatana na vigezo vya kitamaduni vya (iv) na (v).

ICOMOS pia ilitoa mapendekezo kadhaa kwa mamlaka ya Kolombia kuhusu hatua za siku za usoni za uhifadhi wa Mompox. Mapendekezo haya yalielekezewa Kamati ya Urithi ya Ulimwengu, na yalihusu kupakwa rangi upya sehemu za nje za majengo, kuondolewa kwa soko lililokuwa limejengwa hapo karibuni na ubomoaji wa majengo yake, kuyabadilisha majengo ya soko ya kale kuwa eneo la kutia nanga mashua na kituo cha habari cha watalii, usafishaji wa kingo za mito, uchaguaji wa mfumo sawa wa kujenga barabara za makao haya, ukuzaji wa mpango dhabiti wa utalii, na utambulishaji upya wa mpaka wa kaskazini wa eneo lililopendekezwa.



Kabla ya mkutano wa Ofisi ya Kamati ya Urithi wa Ulimwengu mnamo July 1995, Kolombia ilihakikishia ICOMOS kuwa hoja hizi zote zitatiliwa maanani katika uhifadhi wa Mompox.

*Makao ya Kihistoria ya Santa Cruz, Kolombia.*

*© H. van Hooff*

© UNESCO 2004

## Mkutano wa Ofisi ya Kamati ya Urithi wa Ulimwengu, Julai 1995

ICOMOS ilifahamisha ofisi hii kwamba Kolombia ilikuwa na mpango mpya wa kubadilisha mipaka ya eneo lililotengwa kulingana na mapendekezo ya ICOMOS. Ofisi ya urithi iliamua kamati iandikishe makao ya kihistoria ya Santa Cruz de Mompox kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu kutokana na vigezo vya kuamulia ambavyo tayari vilikuwa vimependekezwa.

## Mkutano wa Kamati ya Urithi, Desemba 1995

Kamati ilihitimisha kuwa Santa Cruz de Mompox ni mfano mzuri wa makao ya kikoloni ya Kihispania yaliyoanzishwa kwenye kingo za mto mkubwa, ambayo yamehifadhiwa vyema hadi leo, na hutekeleza wajibu muhimu wa kibiashara. Kamati iliamua kuyaandikisha kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu kwa kutumia vigezo (iv) na (v).

Mamlaka ya Kolombia yalikuwa yameomba msaada wa dola elfu thelathini za kimarekani kutoka kwa Hazina ya Urithi wa Ulimwengu ili kuchunguza athari ya utalii kwenye eneo hili. Hilo ombi lilikubaliwa.



## Historia fupi

| | |
|---|---|
| 1994 | Uteuzi wa Mompox uliwasilishwa na Kolombia kwa Makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu |
| Februari 1995 | Utathmini na ICOMOS |
| Julai 1995 | Ofisi ya Urithi wa Ulimwengu yakagua uteuzi |
| Desemba 1995 | Kamati ya Urithi wa Ulimwengu iliandikisha Mompox kwenye Orodha ya *Urithi wa Ulimwengu* kupitia kwa vigezo vya (iv) na (v)<br><br>Kamati ilitoa dola elfu thelathini za marekani za kugharamia uchunguzi wa athari ya utalii kwenye eneo. |

Jadiliana na wanafunzi wako hatua mbali mbali za uteuzi na uandikishaji kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Pamoja na wanafunzi chagueni eneo la mtaa au la kitaifa ambalo linaweza kuwa na thamani ya kiulimwengu na uwaulize wapendekeze hatua zinazostahili kuchukuliwa ili eneo liandikishwe kwenye orodha.

### Muhtasari

Baada ya kubuni orodha ya muda, mataifa wanachama huteua maeneo yaingizwe kwenye orodha ya urithi kwa kutuma fomu ya uteuzi iliyokamilishwa kwa Makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu. ICOMOS na/au IUCN hutathmini uteuzi na kutoa mapendekezo. Kamati ya urithi wa *ulimwengu hufanya* uamuzi wa mwisho kuhusu maeneo ambayo yataandikwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Pamoja na haya, maeneo *lazima* yawe yanalindwa vyema na yawe makao ya kitamaduni halisi.

# Kufuatilia hali ya uhifadhi wa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu

Uhifadhi wa urithi wa ulimwengu ni shughuli inayoendelea daima. Mataifa wanachama wa *Mapatano* na IUCN na ICOMOS hutoa ripoti za mara kwa mara kwa Kamati ya Urithi wa Ulimwengu juu ya hali ya uhifadhi wa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu, hatua zinazochukuliwa *kuyatunza* na juhudi za kuendeleza utambuaji wa thamani ya urithi wa kitamaduni na kiasilia.

Mataifa wanachama wanachukulia jukumu lao kwa udhati. *Mapatano* yana idhini bayana ya kuhakikisha kuwa mataifa yanatekeleza wajibu wao. Endapo wajibu huu unap*uuzwa na eneo* kukabiliwa na hatari basi eneo hilo linaweza kuondolewa kwenye orodha. Kufikia sasa hakuna eneo lolote ambalo limeshaondolewa kwenye orodha.



Wakati UNESCO inapofahamishwa kuhusu hatari inayokabili eneo la urithi wa ulimwengu—na onyo hilo linaweza kuhalalishwa—eneo litawekwa kwenye orodha ya maeneo yaliyo hatarini. *Orodha hii inakusu*diwa kufanya ulimwengu utambue hali za kiasilia na zinazosababishwa na binadamu ambazo zinatishia sifa zilizofanya eneo fulani kuingizwa kwenye orodha. Maeneo yaliyo hatarini yana haki ya kupewa uhifadhi maalum na kuchukuliwa hatua za kidharura.

*Ni katika* hali zisizo za kawaida tu au hali za dharura (kwa mfano, Dubrovnik mwaka wa 1991) kama vile kuzuka kwa vita, ambapo Kamati ya *Urithi wa* Ulimwengu inaweza kuamua kuweka eneo fulani katika maeneo ambayo yamo hatarini bila kuombwa kufanya hivyo na taifa mwanachama.

## ▲ Orodha ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu yaliyo hatarini

Kuandikishwa kwa eneo fulani kwenye orodha ya maeneo yaliyo hatarini hukusudiwa kuufanya ulimwengu kuzingatia hali hii na kuhakikisha hatua za uhifadhi za kidharura, hasa wakati sifa na thamani za eneo hilo zilizolifanya kuingizwa kwenye orodha zinapohatarishwa.

## Orodha ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu uliyo hatarini

Kamati ya Urithi wa Ulimwengu imeamua kuyaweka mali thelathini na moja ambazo kwenye orodha ya maeneo yaliyo hatarini kulingana na kifungu 11 (4) ya Mapatano. Orodha hii ni ya hadi May 2004. Ukitaka kuiangalia orodho iliyosawazishwa tazama tovuti la http://whc.unesco.org/pg.cfm?cid=86.

| | |
|---|---|
| Afganistani | Mandhari ya ardhi na kumbukumbu za kiakiolojia za Bamiyan Valley Minaret na kumbukumbu za kiakiolojia za Jam |
| Albania | Butrint |
| Aljeria | Tipasa |
| Azerbaijan | Mji ndani kuta wa Baku na ngome ya Shirvanshah na Maiden Tower |
| Benin | Makao matukufu ya Abomey |
| Bulgaria | Hifadhi ya asilia ya Srebarna |
| Kambodia | Angkor |
| Jamhuri ya Afrika ya Kati | Mbuga ya wanyama ya Kitaifa Manova-Gounda St Floris |
| Cote d'Ivoire na Guinea | Hifadhi ya Mt Nimba* na Hifadhi ya wanyama ya Comoe |
| Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | Hifadhi ya wanyama ya Garamba<br>Hifadhi ya wanyama ya Kahuzi-Biega<br>Mbuga ya wanyama ya Okapi<br>Hifadhi ya wanyama ya Salonga<br>Hifadhi ya wanyama ya Virunga |
| Ecuador | Hifadhi ya wanyama ya Sangay |
| Marekani | Mbuga ya wanyama ya Everglades |
| Misri | Abu Mena |
| Ethiopia | Hifadhi ya wanyama ya Simien |
| Guinea | Hifadhi ya Mt Nimba* |
| Honduras | Uhifadhi wa Biosphere ya Rio Planato |
| India | Hifadhi ya wanayama ya Manas<br>Majengo ya kumbukumbu Hampi |
| Iran | Eneo la Bam na mandhari ya kiutamaduni |
| Iraq | Ashur (Qal'at Sherqat) |
| Jerusalem | Mji wa kale wa Jerusalem na kuta zake |
| Mali | Timbuktu |
| Nepal | Bonde la Kathmandu |
| Niger | Hifadhi ya asilia ya Air na Tenere |
| Pakistan | Ngome na Bustani ya Shalamar, Lahore |
| Peru | Ukanda wa kiakiolojia ya Chan Chan |
| Ufilipino | Matuta ya mkingamo ya mpunga ya Ufilipino |
| Ujerumani | Cologne Cathederal |
| Senegal | Hifadhi ya kitaifa ya ndege ya Djoudj |
| Tanzania | Kumbukumbu za Kilwa Kisiwani na Songo Mnara |
| Tunisa | Mbuga ya wanayama ya Ichkeul |
| Uganda | Mbuga ya wanyama ya Mlima Ruwenzori |
| Yemen | Mji wa kihistoria wa Zabi |



*Mbuga ya Kitaifa ya Wanyama ya Virunga, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo.*
*© UNESCO/INCAFO/G. Grande*

Harakati za wanafunzi 13



© UNESCO 2004


'Yellowstone' iliyo Marekani ni mfano mzuri unaoonyesha vile kuwekwa kwa eneo la Urithi wa Ulimwengu kwenye orodha ya maeneo yaliyo hatarini kulivyosababisha hali hii kushughulikiwa kitaifa na hata *kimataifa* kwa kutambua haja ya kulinda bustani hii wakati, inaendelea kukabiliwa na tisho (kwa mfano, *utalii* na uchimbaji madini katika eneo linalopakana na bustani hilo).



## ■ Harakati ya wanafunzi 13

## YELLOWSTONE, MAREKANI

### Lengo: Kuelewa sababu na mbinu zinazotumika kuandikisha eneo kwenye orodha ya maeneo yaliyo hatarini



**Ziara** | ***Harakati* darasani** | ***Vipindi* kadhaa** | **Lugha, jiografia, sayansi** | **Picha, Maelezo kwa ufupi, *Ramani ya Urithi wa* Ulimwengu**

Waeleze wanafunzi yafuatayo.

### Historia fupi

1973 Marekani ilikuwa nchi ya kwanza kuratibisha *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu*

1978 Yellowsone, mbuga ya kwanza ya wanyama ulimwenguni, ilikuwa mojawapo ya maeneo kumi na mawili yalioandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa *Ulimwengu*

1995 Kamati ya Urithi wa Ulimwengu iliamua kuandikisha eneo hili kwenye Orodha ya Maeneo yaliyo Hatarini

### Thamani ya Urithi wa Ulimwengu ya Yellowstone

Yellowstone inatapakaa katika eneo kubwa kwenye kona ya kaskazini-magharibi ya Wyoming na maeneo ya karibu ya Montana na Idaho. Bustani hili hasa lina eneo tambarare la volkano na maeneo madogo ya mwamba mashapo. Ina makorongo ya kuvutia, maporomoko ya maji na mabonde membamba. Harakati za *kivolkano zinazoendelea* husababisha chemichemi 10,000 za maji moto yanayoruka juu na zingine za kutiririka. Wingi wa maji hukuza anuwai ya mimea na wanyama. Sehemu ya kati ina shimo la kivolkano ambalo ndilo kubwa zaidi ulimwenguni. Ni kubwa mara mia moja kuliko lile la Krakatoa *lilipo Indonesia.* Majabali ya zamani sana ni ya miaka bilioni 2.7 na yale machanga bado *yanaundika*. Ndani ya shimo hili kuu kuna misitu ya visukuku ishirini na saba.

### Spishi zinazokabiliwa na tisho (la kuangamia)

Bustani hili lina makazi ya kiikolojia ambayo ni mazingira mazuri kwa spishi zinazotishwa na kuangamia kama vile, dubu wa kijivu, simba wa milimani, tai-vipara na hata spishi moja ya *mbwa mwitu iliyosalia*.



© UNESCO 2004



Yellowstone, Marekani. © UNESCO

## Vitisho vinanavyoikabili Yellowstone

Mnamo Februari 1995 Makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu yalifahamishwa kuhusu vitisho kadhaa vilivyokabili bustani hii hasa kutokana na mapendekezo ya kuanzisha shughuli za kuchimba madini, na pia ukataji miti, athari ya utalii, na sera kuhusu wanyama pori.

## Kikao cha 19 cha Ofisi ya Urithi wa Ulimwengu, Julai 1995

Taifa mwanachama (Marekani) iliwasilisha barua kwa mkutano wa Ofisi ya Urithi wa Ulimwengu, uliofanyika makao makuu ya UNESCO, *Julai* 1995, ambapo walieleza kufadhaishwa kwao na tisho ambalo lilikabili Yellowstone. Waliwauliza wawakilishi wa Kamati ya Urithi wa Ulimwengu na ile ya IUCN kuchukua hatua za kuchunguza bustani hilo. Marekani pia ikaomba Kamati ya Urithi wa Ulimwengu kufikiria kuweka eneo hili katika orodha ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu yaliyo hatarini.

## Sauti zilizopinga pendekezo la kuanzisha migodi karibu na Yellowstone

*Mgodi unaopendekezwa ni 'janga' linalotisha kito cha kitaji cha mfumo wa Bustani za Marekani.*
New York Times

*Hakuna faida yoyote ambayo inaweza kutokana na mgodi huo ambayo inaweza kufidia hasara ya kudumu kwa Yellowstone.*
Bill Clinton, Raisi wa Marekani

*Kama wahaudumu wa eneo hili maalum, wamarekani wana jukumu la kupalinda siyo kwa raia wao, ila kwa raia wote wa ulimwengu, na siyo kwa kizazi hiki tu bali pia kwa vizazi vijavyo.*

Shirika la Mbuga za Wanyama na Uhifadhi, Septemba 1995



© UNESCO 2004

## Ujumbe wa pamoja wa kufanya uchunguzi, Septemba 1995

Ujumbe wa pamoja wa kufanya uchunguzi ulikutana Septemba 1995. Mijadala ya umma ilipangwa wakati wa uchunguzi huu na ripoti kadhaa za kitaalam kutoka kwa viwanda, serikali na makundi ya kuhifadhi mazingira ziliwasilishwa.

## Kikao cha 19 cha Kamati ya Urithi wa Ulimwengu cha Desemba 1995

Taifa mwanachama na IUCN waliripoti matokeo yao kwa Kamati ya Urithi wa Ulimwengu iliyokutana Desemba 1995. Vitisho vifuatavyo vilikabili mbuga hii: mradi mkubwa wa uchimbaji madini, uchafuzi wa maji kutokana na kuvuja kwa mifereji na utupaji ovyo wa taka, ujenzi wa barabara na mkazo kutoka kwa utalii, upungukaji wa spishi fulani za wanyama pamoja na spishi adimu za 'trout' (aina ya samaki wa mtoni), na uchafuzi wa mbogo kwa magonjwa.

Baada ya majadiliano marefu yaliyotokana na vitisho bayana na vinavyoweza kutokea, Kamati ya Urithi wa Ulimwengu iliamua kuindakisha Yellowstone kwenye orodha ya ya maeneo yaliyo hatarini.

## Tangazo la Rais wa Marekani, Septemba 1996

Rais alitangaza hadharani juhudi zake za kutatua kwa njia ya kuridhisha swala la uchimbaji madini.

## Ni mambo gani yaliyofuata?

Kama njia moja ya kuhakikisha uhifadhi wa eneo hili, kamati inatoa ripoti za mara kwa mara kuhusu matokeo ya uchunguzi wa mazingira na hatua za uhifadhi. Kwa njia hii, hali ya eneo itafuatiliwa na kamati ya Urithi wa Ulimwengu. Katika siku za baadaye kama kamati itatosheka na maendeleo yaliyofanywa kuhusu uhifadhi wa Yellowstone, inawezekana kuiondoa kutoka kwenye orodha ya maeneo yaliyo hatarini. Kuiweka Yellowstone kwenye orodha hii kumeongezea juhudi za watu wa Marekani, Rais mwenyewe akiwemo, na jamii ya kimataifa za kuhifadhi mbuga hii ya wanyama ya kipekee.





*Yellowstone hatarini: 'Yellowstone' Marekani.*
*© UNESCO/M. Spier-Donati*

© UNESCO 2004



## ■ Harakati za wanafunzi za 14

## KUTAYARISHA KIPINDI CHA RADIO KUHUSU URITHI WA ULIMWENGU

**Lengo: Kukuza uwezo wa wanafunzi katika mbinu za mawasiliano kwa faida ya uhifadhi wa urithi wa *ulimwengu***



| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mazoezi** | **Harakati darasani au *nje ya darasa*** | **Vipindi kadhaa** | **Lugha, muziki** | **Maelezo kwa ufupi, Ramani ya urithi wa *ulimwengu*** | **Vitabu, CDs, kanda za sauti n.k.** |

✓Waweke wanafunzi katika makundi na kisha mpange kipindi cha radio kuhusu Urithi wa Ulimwengu. Kipindi hiki kinaweza kuhusisha:

- Mazungumzo baina ya wanafunzi kutetea au kupinga eneo fulani kuingizwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu.
- Maelezo ya umuhimu, sehemu ya eneo na kupendeza kwa eneo hilo ambalo limeshaandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu.
- Nukuu kutoka kwa mashairi yanayorejelea eneo la Urithi wa Ulimwengu.
- Muziki na sauti (za kiasilia, wanyama, kengele, dialojia kuhusu taratibu za kidini, nyimbo za dini) ambazo zinamkumbusha mtu kuhusu maeneo ya Urithi wa Ulimwengu.



✓ Kutokana na mawasilisho ya darasa, mkubaliane kuhusu wazo bora zaidi la kipindi na muendeleze mawazo haya zaidi. Gawanya kazi baina ya makundi ya wanafunzi. Rekodi kipindi na ukitumie kituo cha radio cha eneo la karibu, cha kijimbo au cha kitaifa.

7

## ▲ Hazina ya Urithi wa Ulimwengu




Mojawapo ya mambo muhimu ambayo *Mapatano* yameweza kutekeleza ni utoaji msaada wa kifedha kutoka kwa Hazina ya Urithi wa Ulimwengu kufadhili miradi ya kuhifadhi urithi huo.

Hazina hii inatoa msaada na ushirikiano wa kiufundi, kama vile uchunguzi wa wataalamu kutambua au kuzuia kuchakaa kwa eneo la urithi, kupanga hatua za

uhifadhi, kutoa mafunzo kwa wataalamu wa eneo fulani katika uhifadhi au mbinu za uundaji upya, kusambaza vifaa vya kulinda mbuga za wanyama au kukarabati majengo ya kumbukumbu. Hazina hii pia huunga mkono juhudi za kitaifa za kutayarisha orodha za muda za maeneo ya asilia na kimazingira na uteuzi wa maeneo kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Kutegemea aina na kiasi cha usaidizi unaohitajika, kamati au mwenyekiti anaweza kupendekeza usaidizi utolewe kwa mojawapo wa taifa mwanachama.

Hatua za kidharura za uhifadhi na kuhifadhi maeneo yaliyo kwenye orodha ya maeneo yaliyo hatarini ndizo zinazopewa kipaumbele kwa msaada wa kifedha.

Hazina ya Urithi wa Ulimwengu iliyobuniwa 1972 na *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* hupata mapato yake makubwa kutokana na mchango wa lazima kutoka mataifa wanachama–kiasi cha asili mmoja cha mapato ya UNESCO—na misaada ya kujitolea.

Njia nyingine za kupata fedha ni kama vile hela zinazotolewa kwa amana za shughuli maalum na faida kutokana na uuzaji wa chapisho za Urithi wa Ulimwengu.

Jumla ya kiasi kinachopatikana kila mwaka inakaribia dola za marekani milioni tatu nukta tano, ambacho ni kiasi kidogo kikilinganishwa na majukumu makubwa yanayolikabili shirika hili.



Mali za hazina hii bado ni za kiwango cha chini iwapo itaweza kutimiza maombi yanayotolewa kwa Kamati ya Urithi wa Ulimwengu. Hata hivyo hazina hii tayari imetoa mamilioni ya madola kwa miradi muhimu ya kuhifadhi maeneo ya kitamaduni na asilia yaliyoko Afrika, Bara Hindi na Pasifiki, mataifa ya Kiarabu, Marekani ya Kusini na Karibea, na Uropa.

Kama wewe au wanafunzi wako mngependa kushiriki katika uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu kwa kutoa msaada kwa Hazina ya Urithi wa Ulimwengu, tafadhali tuma agizo la fedha au uhamishe fedha kutoka benki kwa akaunti zifuatazo.




Iwapo uhamishi ni wa dola za kimarekani maelezo ya benki ni kama yafuatayo:

**UNESCO Account N° 949-1-191558**
**CHASE JP MORGAN BANK**
**International Money Transfer Division**
**4 Metrotech Center, Brooklyn**
**NEW YORK**
**NY 11245, United States of America**
**SWIFT Code: CHASUS 33 - ABA N° 0210-0002-1**

Iwapo pesa ni Euro zinastahili kuhamishwa kwa akaunti ya benki ya UNESCO ifuatayo:

**UNESCO A/C No. 30003-03301-00037291909-97**
**SOCIETE GENERALE**
**Paris Seine Amont**
**10 rue Thénard**
**75005 PARIS, France**
**SWIFT code : SOGEFRPPAFS**

Tafadhali andika jina lako na anwani ya shule yako na ueleze unatuma mchango kwa hazina ya Urithi wa Ulimwengu.



## Harakati za wanafunzi za 15

### KUZUSHA UFAHAMU

**Lengo: Kuhimiza umoja na ushiriki kivitendo miongoni mwa wanafunzi katika shughuli za kuunga mkono uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu**



**Majadiliano** | **Harakati darasani au harakati nje ya darasa** | **Vipindi kadhaa** | **Lugha** | **Ramani ya Urithi wa Ulimwengu, Maelezo kwa ufupi**


✓Jadiliana jinsi wanafunzi wanavyoweza kuifanya jamii zao kuelewa kuhusu urithi wa maeneo ya kwao, ya kitaifa, na ya ulimwengu. Orodhesha mapendekezo yao. Je, pendekezo yao moja au zaidi yaweza kutekelezwa?

✓Jadilianeni malengo ya hazina ya Urithi wa Ulimwengu. Jadilianeni iwapo inawezekana kuwa na shughuli za kuchangisha pesa za kuunga mkono juhudi za uhifadhi wa urithi za eneo la kwenu au za ulimwengu.





© UNESCO 2004



# Kupitia kwa mitaala: *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu*

## Sanaa

**Tumia** picha na habari kutoka kwa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu kufunza historia. Tengeneza kielelezo chenye vipimo cha maeneo ya Urithi wa Ulimwengu.
**Tayarisha** kampeini ya matangazo ya kupalilia kuzusha ufahamu kuhusu maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na uhifadhi.
**Tembelea** maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na mchore au mpige picha mtakayoyaona.
**Tumia** maeneo ya Urithi wa Ulimwengu kufunza kuhusu mitindo ya usanifu-mijengo.

## Lugha ya kigeni

**Soma** vikaratasai kuhusu urithi wa asilia na kitamaduni wa nchi nyingine.
**Soma** kuhusu maeneo ya Urithi wa Ulimwengu kama chanzo cha habari kuhusu historia na hali ya sasa ya nchi zingine.
**Andika** makala kuhusu haja ya kuhifadhi maeneo ya urithi.

## Historia

**Temebelea** maeneo ya urithi wa ulimwengu au maeneo ya urithi yaliyo karibu nawe, ambayo yana uhusiano na vipindi vya kihistoria.
**Jifunze** kuhusu maeneo ya Urithi wa Ulimwengu kwa kuchunguza kipindi mahsusi (cha kihistoria).

## Lugha na fasihi

**Andikia** darasa lako au gazeti makala juu ya *Mapatano* au juu ya eneo mahsusi la Urithi wa Ulimwengu.
**Wahoji** watu wanaoishi karibu na eneo la urithi na udadisi eneo hilo lina maana gani kwao.
**Andika** vijikaratasi vya habari kuhusu eneo fulani.
**Tayarisha** tamthilia ya kihistoria.
**Soma** riwaya au hadithi fupi ambazo zinagusia eneo fulani la urithi.

## Hesabu

**Kagua** sifa za asilia (idadi ya spishi, ukubwa wa nyumba) za eneo la urithi wa ulimwengu na utumie grafu, pai chati, na takwimu kuwasilisha matokeo kimchoro.
**Chunguza** ukubwa wa majengo ya kumbukumbu na nyumba zingine maarufu na uzitayarishe mchoro wa kielelezo.

## Masomo ya kidini

Onyesha picha za maeneo ya Urithi wa Ulimwengu yanayohusiana na dini tofauti na mifumo mbalimbali ya imani. (Picha nyingi za maeneo zimeambatanishwa na kifaa hiki)

## Mtandao wa mdahalishi

Chunguza kurasa-tovuti la UNESCO (http://www.unesco.org/whc) na tovuti la Mradi wa Shirikisho la Mashule (ASPnet) kwenye mdahalishi ufuatao: http://www.unesco.org/education/asp.



© UNESCO 2004



**'Singetaka nyumba yangu izingirwe kwa kuta kila upande, na madirisha yangu kuthibitiwa. Napandelea tamaduni za mataifa yote zivume huru nyumbani kwangu. Hata hivyo, sitakubali kutekwa na tamaduni yoyote.'**

**Mahatma Gandhi**

# Urithi wa Ulimwengu na kujitambulisha


Ukurasa

**Malengo** **85**

Maarifa 85
Mielekeo 85
Ujuzi 85

**Urithi wa Ulimwengu: Msingi wa kujitambulisha** **86**

Kitambulishi: Mimi ni nani? Sisi ni nani? 86
Harakati za wanafunzi za 16: Majina kama vielelezo vya kujitambulisha 87
Kitambulishi katika ulimwengu unaobadilika kwa kasi 87

**Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na kitambulishi** **88**

**Harakati za wanafunzi za 17:** Maeneo ya ulimwengu na kitambulishi 89

**Mitindo tofauti ya ujenzi kama njia ya kujitambulisha** **90**


**Harakati za wanafunzi za 18:** Mitindo *tofauti ya ujenzi kama* njia ya kujitambulisha 91
**Harakati za wanafunzi za 19:** Baraza linaamua kuhusu siku zijazo za eneo la kihistoria la mji 92
**Harakati za wanafunzi za 20:** Kujifunza kupitia kwa tamaduni tofauti 93

**Kitambulishi na wenyeji** **93**

Harakati za wanafunzi za 21: Majengo na *kumbukumbu* la kitaifa la Zimbabwe Kuu, Zimbabwe 94
Harakati za wanafunzi za 22: Mbuga ya kitaifa ya wanyama ya Uluru-Kata Tjuta, Australia 96

**Kupitia kwa mitaala: Urithi wa Ulimwengu na kujitambulisha** **99**

# Malengo



## Maarifa

Kuwasaidia wanafunzi kukuza maarifa na ufahamu kuhusu:

- Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu ya kitamaduni na kiasilia kama viwakilishi vya udhabiti katika ulimwengu unaobadilika kwa haraka
- Umahususi wa kila utamaduni na wazo kuwa tamaduni zote ni sehemu ya ustaarabu wa mwanadamu
- Mwingiliano na utegemeanaji wa asilia na utamaduni, na baina ya tamaduni.

## Mielekeo

Kuwahimiza wanafunzi:

- Kuonea fahari utamaduni wao, historia ya nchi na mazingira yao
- Kutambua mambo yanayodhaminiwa na jamii zao na chanzo cha kuchukuliwa mambo hivyo
- Kukuza heshima kwa watu wote na tamaduni zao na kwa njia hiyo kuchangia uelewano na heshima ya kimataifa
- Kukuza hali ya ushirikiano katika utunzaji wa tamaduni na asilia za ulimwengu.

## Ujuzi

Kuwasaidia wanafunzi kukuza uwezo wao wa:

- Kutafiti zaidi kuhusu asili yao (ya kijamii na ya kitaifa)
- Kujadiliana mambo kwa njia wazi na ya kidemokrasia
- Kuwa viongozi katika kuunga mkono uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu.

# Urithi wa Ulimwengu: msingi wa kujitambulisha

Ufahamu wa Urithi wa Ulimwengu unaweza kutusaidia kuelewa zaidi asili yetu na kitambulishi chetu cha kitamaduni na kijamii. Uchunguzi wa kimakini wa maeneo yoyote yaliyo kwenye orodha ya Urithi wa Ulimwengu utatusaidia kufahamu kuhusu mila na desturi, mambo yanayothaminiwa na habari za watu na utamaduni uliowapatia sifa zao (urithi wa kitamaduni) au ustaarabu walioingiliana nao (wa kiasilia na ule wenye sifa za kiasilia na kitamaduni), na mandhari ya kitamaduni. Hii pia inahusisha nafasi ya kujifunza kuhusu urithi unaonekana na ule ambao usioonekana.

Maeneo ya kitamaduni na kiasilia ndiyo mazingira ambayo wanadamu wanategemea kisaikolojia, kidini, kielimu na kiuchumi. Kuharibika kwake au kuchakaa kwake kutakuwa tisho kwa kitambulishi chetu, mataifa yetu na hata sayari yetu. Tuna jukumu la kulinda maeneo haya kwa faida ya vizazi vijavyo.

Ahadi ya wanafunzi, Muungano wa Vijana wanaohusika na Urithi wa Ulimwengu, Bergen, Norway

## ▲ Kitambulishi: Mimi ni nani? Sisi ni nani?


Kitambulishi

1. Ubora au hali ya kuwa vile vile, kufanana kwa hali ya juu
2. Ubinafsi, mtu binafsi... uhai wa mtu
3. Hali ya kutambuliwa kutokana na hisia zako, mapendeleo yako, n.k.

*Shorter Oxford Dictionary*

Tangu kuzaliwa kwetu, kila mmoja anatofautiana na wengine kutokana na sifa-binafsi zetu za kuzaliwa na sifa zetu za kiasilia ambazo tunazirithi kutoka kwa wazazi na mababu zetu. Alama zinazofanyizwa na vidole vyetu, kwa mfano, zinawasilisha sehemu ya utambulishi wetu usiyofutika. Jina la familia yetu, ambalo tunalirithi, na jina ambalo tunapewa, zinaweza kubadilishwa maishani, lakini pia ni sifa muhimu ya kitambulishi chetu.

Kitambulishi hata hivyo si jambo la binafsi. Swali la 'Mimi ni nani?' lina uhusiano mkubwa na 'Sisi ni nani?' – 'sisi' kwa mfano, itakuwa kabila letu, taifa au imani yetu ya kidini. Kama wanachama wa kikundi tunaunganishwa pamoja kupitia kwa lugha, mila na desturi, kaida za kidini, sheria za kiadili, mila, chakula, mavazi, n.k. Kitambulishi cha taifa aghalabu huelezwa kupitia kwa ishara kama vile lugha, mavazi ya kitaifa, bendera, nembo au wimbo wa taifa.



*Young people in traditional costumes at the Bergen World Heritage Youth Forum, Norway.*
*© UNESCO*



ESCO 2004



■ **Harakati za wanafunzi za 16**

## MAJINA KAMA VIELELEZO VYA KUJITAMBULISHA

### Lengo: Kuwazia kuhusu kitambulishi chetu na cha jamii zetu



**Utafiti** | **Harakati darasani** | **Harakati nje ya darasa** | ***Vipindi* viwili au masaa nje ya darasa** | **Lugha**

✓ Waulize wanafunzi kuchunguza maana ya majina yao ya kifamilia wakisaidiwa wa wazazi na watu wa jamii zao. Pia, waulize waeleze jinsi majina yao (la kwanza na la pili) yalivyochaguliwa. Je, kila mwanafunzi anaonaje kuhusu jina lake? Ni jina ambalo limesambaa katika eneo hilo? Jina hilo lina uhusiano na jina la eneo muhimu la kitamaduni au kiasilia? Ni jina lisilo la kawaida? Je, jina hilo lilitumiwa kama kumbukumbu ya mtu fulani kama babu au nyanya au mtu wa jamii yenu, au mtu mashuhuri kihistoria au katika sinema, na kadhalika? Jina hilo linaathiri kitambulishi cha mtu? Kama ni kweli, hali hii inajitokezaje?

## ▲ Kitambulishi katika ulimwengu unaobadilika kwa haraka

Dunia inasonga haraka na watu wengi wanaingia katika karne ya ishirini na moja huku wakisahau kitambulishi chao. Hiki ni kinaya. Tunastahili kuonea fahari asili na utamaduni wetu na kuuhifadhi kama msingi. Tunastahili kujenga hali yetu ya siku za baadaye.
Mapendekezo ya mwanafunzi katika Muungano wa Vijana wa Urithi wa Ulimwengu, Beijing, Uchina.

Kama watu binafsi, jamii (makabila na mataifa tofauti) ambayo sisi tunajijulisha hubadilika kulingana na wakati, kutokana na muingiliano na mazingira ya kiasilia na pia na jamii zingine na tamaduni tofauti. Ingawaje hali imekuwa hivi, namna na mkazo wa mabadaliko umeongezeka sana katika karne ya ishirini hasa kuhusu njia za kisasa za usafiri, mawasiliano ya simu na habari (tarakilishi, simu, kipepesi, mtandao, satelaiti za mawasiliano, n.k.) na hali ya utandawazi (globalization).

Utandawazi kwa jumla ni swala la kiuchumi lakini lina athari za kijamii na za kitamaduni. Mojawapo ni mwelekeo karibu katika sehemu zote za ulimwengu kwa watu, hasa vijana, kupendelea bidhaa fulani zinazotumiwa kwa wingi ambazo hutangazwa kote ulimwenguni pamoja na muziki maarufu, sinema na vipindi vya televisheni, mavazi na chakula cha hotelini.

Utandawazi wa utamaduni umetajwa katika hati mbili muhimu za UNESCO:
*...utamaduni hutandazwa kwa hatua na adhari za utandawazi haujafikia tamaduni zote. Hatuwezi kusahau ahadi za wema wa utandawazi au hatari zake, mojawapo ambayo ni kusahau upekee wa ubinafsi wao. Binadamu wana uwezo wa kujichagulia*

*maisha yao na kujenga hali zao za baadaye kufikia kipeo cha uwezo wao katika hali ya utajiri na tamaduni zilizotunzwa kwa makini ambazo tusipotahadhari, zitahatarishwa na maendeleo ya kisasa.*
*Learning: the treasure within*, Report of the International Commission on Education for the Twenty-first Century, uk. 17, Paris, UNESCO Publishing. 1996.

Watu na jamii ambazo zinaishi katika ulimwengu unaobadilika kwa kasi nao pia wapaswa kubadili bila kupuza vipengele muhimu vya tamaduni zao.

Imani za Kiafrika, kwa mfano, zimefungamana na dini za kitamaduni, husisitiza umuhimu wa uhusino baina ya wanadamu na asilia, baina ya vitu vinavyoonekana na visivyoonekana bayana, mambo yanayoeleweka na ya kuhisi, na baina ya vizazi vya kale nad vya sasa. Hazina *hii ya maarifa na thamani* za kijamii inaweza kutumika kutatua shida za enzi hii kama vile kuokoa mazingira au kupatanisha makundi yanayozozona.
Our Creative Diversity, Report of the World Commission on Culture and *Development*, uk. 166, Paris, UNESCO Publishing, 1996

# Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na kitambulishi

Watu wengi wanajitambulisha na maeneo yaliyoandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Magofu ya Zimbabwe kabla ya uhuru yanatukumbusha kuhusu asili ya Zimbabwe kabla ya ukoloni; Muungano wa Urusi huhusishwa na Kremlin na Red Square zilizo Moscow; Italia na Venice na wangwa yake, *pamoja* na Mnara wa Pisa na mji wa Florence, Lebanon na Baalbek na Byblos; India na Taj Mahal, iliyo Agra; Guatemala na Antigua, Guatemala, Uzbekistan na makao ya kihistoria ya Bukhara—kwa kutoa mifano michache.



Baadhi ya maeneo ya kiasilia kama vile Mbuga ya wanyama ya Everglades, na Mbuga ya wanyama ya Grand Canyons iliyo Marekani, Mbuga ya wanyama ya Serengeti iliyo katika Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Mbuga ya wanyama ya *Sagarmatha* (Mlima Everest) Nepal, Los Glacieres iliyo Argentina, pia humulika vitambulishi vya makundi au vya kitaifa.





*I Sassi di Matera, Italia.*
*© UNESCO/M.Moldaveanu*



## ■ Harakati za wanafunzi za 17

# MAENEO YA URITHI WA ULIMWENGU NA KITAMBULISHI

## Lengo: Kuelewa thamani ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu

|  |  |  |  |  |
|---|---|---|---|---|
| **Majadiliano** | **Harakati za darasani** | **Kipindi kimoja cha darasani na muda nje ya darasa** | **Historia, elimu ya jamii** | **Ramani ya Urithi wa Ulimwengu na Maelezo kwa ufupi** |

✓Tumia picha zinazoambatanishwa na kifaa hiki na chochote kingine kitakachopatikana kuwajulisha wanafunzi baadhi ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu ambayo yamechukua nafasi muhimu katika historia ya mwanadamu na uhifadhi wa kiasilia kama vile:

- Maeneo ambayo watu wanajihusisha nayo (ya kitamaduni, na ya kiasilia).
- Maeneo ambayo yanarejelea matukio ya historia ya kisiasa ya ulimwengu.
- Maeneo yanayohusiana na dini za ulimwengu na mifumo ya imani.
- Maeneo ambayo yanatoa mifano kuhusu kuchuma riziki.

Matriki iliyo hapa chini inapendekeza mawazo ya kujadiliana.

| | **Asili ya binadamu** | **Jamii ya uwindaji na ukusanayaji** | **Jamii ya kitamaduni** | **Jamii ya wakulima** | **Jamii ya ufanyi biashara** | **Jamii ya kiviwanda** | **Jamii baada ya Usasa (Postmodern society)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bara Hindi na eneo la Bahari ya Pacifik** | Peking Man Site, Uchina | | | Matuta ya mkingamo ya Mpunga, Cordilleras (Ufilipi) | | | |
| **Mataifa ya Kiarabu** | | Rock-Art Sites Tadrart Acacus (Libya Arab Jamahiriya) | | | | | |
| **Afrika** | | | | | Kisiwa cha Mozambique (Mozambique) | | |
| **Uropa na Marekani ya Kaskazini** | | | I Sassi di Matera (Italia) | | Mji wa Hanseatic wa Lubeck (Ujerumani) | Ironbridge Gorge (Uingereza) | Bauhus na maeneo yake (Ujerumani) |
| **Marekani ya Kusini na Karibea** | | | | | | Mji wa historia wa Ouro Preto, Brazil | Brasilia (Brazil) |



© UNESCO 2004

# Mitindo tofauti ya ujenzi kama njia ya kujitambulisha

Mitindo ya ujenzi ambayo inapatikana katika baadhi ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu yanadhihirisha maingiliano baina ya watu na mazingira yao ya kiasilia. Mfano mojawapo ni eneo la Urithi wa Ulimwengu la Wilaya ya Bryggen, Bergen nchini Norway, ambalo linadhihirisha jinsi mbao za Norway, zimekuwa kitu kinachochangia kitambulishi cha kitamaduni cha watu wa Norway.



Bryggen, Norway.
© UNESCO/D. Roger



## Jinsi mbao za miti ya Norway zilivyoathiri utamaduni wao

Je, kuna uhusiano baina ya vifaa vya ujenzi vya Norway na utamaduni wao?
Stephen Tschudi-Masden, aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Ukurugenzi wa Urithi wa Kitamaduni nchini Norway ameandika:

*Kwanza... tufikirie kuhusu miti. Jambo kubwa linalouwekea mipaka ni urefu. Hakuna mojawapo wa miti hii yenye matawi mapana inayokuwa mirefu au minyoofu vya kutosha ili kuandaa mbao mwafaka za kujengea nyumba ya kawaida bila magogo kushikanishwa pamoja.*

*Vipande vya mbao virefu zaidi ambavyo vimetumika kwa ujenzi vinatuonyesha urefu wa mti huu ('Pine' au msonobari ambao ndio unatumika sana kwa ujenzi Norway): vilipatikana 1861 wakati wa ubomoaji wa kanisa la Hof, na vilikuwa na urefu wa mita 15. Huu ndiyo ulikuwa urefu wa juu kabisa—nusu ya urefu huu ndio urefu wa kawaida uliotumika kwa ujenzi wa nyumba.*

*Si mfalme wala yeyote aliye na cheo kikubwa anayeweza kukiuka vipimo na uwiano huu kwa sababu mti ndio uliamua. Nyumba zote zinatawaliwa na sheria sawa kwa kila mtu, ingawaje unene na pambo la umbo wa magogo hutofautiana.*

*Swali litazuka iwapo hali hizi za ujenzi zimekuza demokrasia katika jamii. Utahisi sifa ya kiutu ndani ya majumba haya madogo inayotuliza na kufariji. Mapambo ya mirava kwenye magogo hayo yaliyotimiwa kujengea kuta yanatuliza na kupoza na ni ya kawaida. Hata mbao zenyewe zina umuhimu wake, sio tu kinga muhimu dhidi ya baridi, lakini pia inafurahisha unapoigusa.*

*Mwenendo wa kujenga kwa mbao bado unaendelea na hata leo asilimia 80 ya nyumba zote mpya Norway zimejengwa kwa mbao. Kuhusu haya tunaweza kuwa katika eneo dhabiti tunapotaka kujadiliana kuhusu kilicho maalum kuhusu urithi wa kitamaduni wa Norway, pengine kuzidi njia nyingine yeyote ya kujieleza kitamaduni na mti wenyewe umeathiri maendeleo pamoja na mipaka yake na ubora wake.*
Norway: A cultural heritage. *Monuments and Sites. Universitetsforlaget.*

UNESCO 2004



■ **Harakati za wanafunzi za 18**


## MITINDO TOFAUTI YA UJENZI KAMA NJIA YA KUJITAMBULISHA

### Lengo: Kuwazia zaidi kuhusu kitambulishi kwa kujifunza kuhusu urithi wa vitu vinavyoonekana (k.m., maeneo mbalimbali, nyumba, majengo ya kumbukumbu, mbuga za wanyama)



Utafiti — Harakati za darasani — Vipindi viwili vya darasani — Lugha, jiografia — Picha

✓ Waulize wanafunzi waandike insha ya kueleza hali ya maeneo, majengo ya kumbukumbu na hata mbuga za wanyama kwenye eneo au nchi wanamoishi. Je, baadhi yake ni maeneo ya Urithi wa Ulimwengu? Upo uhusiano wa utamaduni na vifaa vya ujenzi, na mwelekeo wa ujenzi (jinsi nyumba zilivyopangwa, mjini, kijijini) mali asilia (k.m. mawe ya kuchimbwa) na asilia ya mandhari (k.m. mji ambao umejengwa kando ya ziwa)? Je kitambulishi chako cha kitamaduni kinamulikwa na jinsi nyumba zilivyojengwa na vifaa vilivyotumika?




*Timbuktu, Mali.*
*© UNESCO/M. Kone*

## ■ Harakati za wanafunzi za 19

## BARAZA LINAAMUA KUHUSU SIKU ZIJAZO ZA SEHEMU YA KIHISTORIA YA MJI

### Lengo: Kuelewa vyema athari ya maendeleo juu ya uhifadhi wa urithi




Uigizaji | Harakati darasani | Shughuli za nje ya darasa | Vipindi kadhaa | Masomo ya jamii, hesabu | Picha



Mitazamo ya Kielimu kuhusu Urithi wa Ulimwengu



✓Panga uigizaji darasani kwa kuzingatia hali ifuatayo ya kubuni.



Serikali ya wilaya imetayarisha mpango wa maendeleo unaohusu sehemu ya katikati ya mji unamoishi. Sehemu hii ya mji ni ya kale na ina baadhi ya majengo za kienyeji yaliyostawi. Kwa sababu hii, majengo haya ni muhimu kama kumbukumbu ya kitambulishi cha eneo lenu. Hata hivyo, majengo haya hali yao imezoroteka sana na eneo hili limeachwa nyuma na harakati za usasa. Mifereji ya maji na vyoo haviwezi kutengenezwa. Iwapo mpango wa maendeleo utatekelezwa itamaanisha ya kuwa sehemu ya kale ya mji itabomolewa na badala yake kutajengwa nyumba za gorofa. Baadhi ya wanachama wa serikali ya wilaya wanaunga mkono mpango wa maendeleo, wanasiasa wengine wa eneo hilo wanaupinga. Leo, makundi yanayohusika yamekutana kujadiliana na kuamua iwapo mpango huu utatekelezwa.

✓Wapange wanafunzi katika makundi matano:

1. Kikundi cha serikali ya wilaya kinachopendelea mpango huu
2. Kikundi cha serikali ya wilaya kinachopinga mpango huu
3. Wananchi wanaoishi katika sehemu ya kale ya mji
4. Watalaamu (wasanifu-mijengo, wapangaji wa miji n.k.)
5. Wawakilishi wa vyombo vya habari

✓Pia, chagua mwenyekiti mmoja na manaibu wawili kuongoza mjadala, na waandishi wawili kuandika ripoti juu ya mkutano.

✓Wazieni na mjadili vitisho vya aina hii vinavyoikabili miji au maeneo yaliyo kwenye Orodha ya Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu yaliyo Hatarini.

© UNESCO 2004

## ■ Harakati za wanafunzi za 20

### KUJIFUNZA KUPITIA KWA TAMADUNI TOFAUTI

### Lengo: Kuelewa vyema uhusiano baina ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na kitambulishi

| Utafiti | Harakati darasani na harakati za nje ya darasa | Vipindi kadhaa vya *darasani* | Lugha, masomo ya jamii | Ramani ya Urithi wa ulimwengu, Maelezo kwa ufupi | Mdahalishi |
|---|---|---|---|---|---|

✓ Wapange wanafunzi katika makundi. Uliza kila kikundi kuandika wasilisho fupi juu ya mada zifuatazo:

- shule yao
- darasa lao
- maeneo ya Urithi wa Ulimwengu katika nchi yao

✓Badilisheni mawasilisho haya na shule moja au zaidi ng'ambo (kupitia kwa barua, kipepesi au mdahalishi). Ni nini ulichojifunza kutoka kwa wenzako? Ilichukua muda gani? Majibu yanalingana au kutofautiana kwa njia gani?

✓Jadilianeni jinsi njia mpya za mawasiliano zinavyowaleta watu pamoja kutoka sehemu zote za ulimwengu kwa njia ambayo haingewezekana wakati wazazi wa wanafunzi walikuwa wachanga.



# Kitambulishi na wenyeji

Kujifunza njia mbali ambazo wenyeji wa maeneo tofauti wanavyohusiana na asilia na urithi wa kitamaduni husaidia katika uelewaji wa umuhimu wa kitambulishi cha kibinafsi, cha makundi na hata cha taifa, na jinsi kitambulishi hiki kinavyoweza *kutambuliwa* na kudumishwa, kwa mfano, kupitia kwa uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu. Mifano ifuatayo inayowasilishwaa kama harakati za wanafunzi itaeleweka kwa urahisi. Pengine itakuchochea kutafuta mifano mingine kutoka sehemu yenu ya ulimwengu au kwengineko na kukuza harakati kama hizo.





*UNESCO Word Heritage Youth Fora ilikuwa ni nafasi ya kujifunza tamaduni kadhaa huko Victoria Falls.* © UNESCO



## ■ Harakati za wanafunzi za 21

# MAJENGO YA KUMBUKUMBU YA KITAIFA YA ZIMBABWE KUU, ZIMBABWE

## Lengo: Kuelewa vyema asili ya kihistoria ya eneo

|  |  |  |  |  |  |
|---|---|---|---|---|---|
| **Ziara katika *eneo la Urithi* wa Ulimwengu** | **Harakati darasani** | **Vipindi kadhaa** | **Historia, jiografia, *masomo ya* jamii, masomo kuhusu uraia na serikali** | **Ramani ya Urithi wa Ulimwengu, Maelezo kwa ufupi** | **Mdahalishi** |

✓Simuliza hadithi ya Zimbabwe Kuu (Greater Zimbabwe) ili kutoa mfano wa mzozo kuhusu asili ya kihistoria ya eneo muhimu na la kuvutia. Uchunguzi wa kiakiolojia wa Zimbabwe Kuu sasa umeshathibitisha chimbuko la Kiafrika la eneo hili.

Zimbabwe Kuu inathamaniwa sana na inatambuliwa kama ishara ya taifa. Hata jina la nchi linatokana na magofu haya ya kuvutia, yanayoonewa fahari (Zimbabwe inamaanisha majumba ya mawe).

Zimbabwe Kuu iko karibu na sehemu tambarare yenye miti na ndiyo ujenzi mkubwa kabisa wa kale katika kusini mwa Sahara barani Afrika. Ina maeneo mawili yaliyojaa magofu yaliyo milimani, ngome, kasri dhabiti yenye kuta zinazofungana na majabali ya matale. Vizazi tofauti vya wakaazi walishikanisha majabali na kuta za mawe na kujenga maeneo madogo yaliyozungushiwa kuta na njia nyembamba. Pia kuna magofu ya bonde, eneo kubwa sana lililozingirwa kwa mawe, ni jengo la kumbukumbu la kufurahisha sana: kuta inayozingira eneo lililozingirwa lina urefu wa mita 250 na limetumia tani 15,000 za majabali yaliyochongwa kwa maakini (ndiyo jengo kubwa kabisa la kale).

Juhudi za kudhibitisha chimbuko la Kiafrika la magofu hayo na utamaduni wa wakazi uliotia fora, haukuwafurahisha masetla weupe katika nchi hiyo ambayo awali iliitwa Rhodesia. Ili kubatilisha historia kwa kuiandika upya, wanasiasa na wanapropaganda walishindilia kuwa kulikuwa na uwezekano wa athari za Wafenisi, Waarabu, Wahindi, au hata Wayahudi. Katika mijadala mikali bungeni ilisemekana ya kuwa Zimbabwe Kuu haikuwa na asili ya Kiafrika.

Hata hivyo, wana-akiolojia Randall MacIver na Getrude Caton-Thompson ambao walihusika katika uchimbaji huko Zimbabwe Kuu, walifikia uamuzi kuwa magofu haya kwa hakika ni ya Kiafrika. Karibu kila chombo cha kutengenezwa kilichopatikana kilikuwa na asili ya Kishona, na rekodi ya uchimbaji katika viwango vyote ilionyesha maisha ya awali Kiafrika.

Kazi hii na utafiti mgumu uliofanywa na wanaakiolojia wengine, wanaisimu, na wanaanthropolojia, unatoa msingi wa kugawanya historia ya Zimbabwe Kuu katika maeneo matatu ya kihistoria.

Idadi ya watu iliongezeka sana katika eneo hili katika karne ya kumi na moja wakati vijumba vya nguzo na udongo vilipojengwa kwenye mlima. Karne mbili baadaye, vijumba hivi viliondolewa na mahali pake kujengwa nyumba kubwa za udongo na kuta za kwanza za mawe. Wakati wa karne iliyofuata, jamii iliendelea kutokana na biashara na watu waliokuwa katika pwani ya Afrika mashariki, hasa wafanyi biashara Waislamu. Lakini, kufikia karne ya kumi na tano Zimbabwe Kuu haingeweza kuendelea kujikimu na mji mkuu ukaanza kufifia pole pole.


Mabaki yanayothibitisha biashara hii pana pamoja na mitindo ya ujenzi na muundo wa uashi wa Zimbabwe Kuu ndio uliosababisha ubishi kuhusu asili yake ya Kiafrika.

Miaka ya kuandika upya historia ya kweli na kitambulishi cha Zimbabwe ya kale sasa imekwisha. Hivi leo, magofu ya Zimbabwe Kuu yanawakilisha uhai wa taifa, almasi ya urithi wa Kiafrika.

✓Waulize wanafunzi wako waandike insha fupi kuhusu hali kama hii. Linganisha na jadili insha hizi darasani.



*Majengo ya kumbukumbu ya Zimbabwe Kuu, Zimbabwe.*
© Patrimoine 2001/C. Lepetit



© UNESCO 2004



■ **Harakati za wanafunzi za 22**

## MBUGA YA KITAIFA WANYAMA YA ULURA-KATA TJUTA, AUSTRALIA

### Lengo: Kuelewa vizuri wazo la mandhari ya kitamaduni na nafasi ya wenyeji katika uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu



| Ziara katika maeneo ya Urithi wa Ulimwengu | Harakati darasani | Vipindi viwili vya darasani | Jiografia, historia, masomo ya jamii | Maelezo kwa ufupi, Ramani ya Urithi wa Ulimwengu |
|---|---|---|---|---|

Mfano wa pili ni Mbuga ya wanyama ya Uluru-Kata Tjuta iliyo Australia, unadhirisha jinsi uandikishaji kwenye Orodha ya *Urithi* wa Ulimwengu kunaweza kuimarisha kutambuliwa na ulinzi wa kitambulishi na tamaduni za eneo.

Vile vile, mbuga hii ni mfano wa usimamizi bora wa eneo kutokana na ushirikaian kati ya wenyeji na makala ya uhifadhi ya serikali.

Eneo hili liliandikishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1987 kama eneo la kiasilia. Katika mwaka wa 1994 liliteuliwa tena kama eneo la mandhari ya kitamaduni—mahali panapowakilisha kazi za watu na miundo asilia. Mbuga ya wanyama ya Uluru-Kata Tjuta ilikuwa mandhari ya kitamaduni ya kwanza kuandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu.

*Mbuga ya wanyama ya Uluru-Kata Tjuta inasamba ardhi ya wa-Aborijino ambapo wangali wanaishi na lugha ya ki-Aborijino bado inazungumzwa kama lugha ya mama. Katika mwaka wa 1985, serikali ya Australia 'ilirejeshea' wa-Anangu umiliki wa ardhi hii. Wa-Anangu ni wenyeji wa Jangwa Magharibi la Australia. Baada ya kupatiwa mamalaka ya kumiliki ardhi hii, wa-Anangu waliikopesha mbuga hii ya wanyama Halmashauri ya Kuhifadhi Asilia ya Australia (Australian Nature Conservation Agency, au ANCA). Wa-Anangu na ANCA sasa wanahifadhi na kusimamia mbuga hii kwa pamoja. 'Urejeshaji' huu na usimamiaji wa mbuga hii unachukuliwa kama nguzo muhimu katika historia ya wanaharakati wa ki-Aborijino wanaotetea haki za ardhi na pia katika historia ya uhifadhi wa urithi nchini Australia.*

*Maarifa ya Wa-Anangu, maisha, kitambulishi na muundo wa jamii, mfumo wao wa imani za kiadili na mandhari ya ardhi wanamoishi, inapewa umbo na kuelezwa na Tjukurpa. Tjukurpa, ambaye wakati mwingine inatafsiriwa kimakosa kama 'wakati wa ndoto', huongoza jinsi wa-Ananga walivyounda jamii yao na wanavyotunzana na kutunza ardhi. Huongoza tabia zote. Wakati wa-Anangu wanapitia mahala Uluru na Kata Tjutu waliposimama, wanahisi uhai wa, na kuelewa safari na harakati za mababu zao ambao walivuka ardhi wakati dunia haikuwa na maumbile. Mababu zao (wanaojitolea katika sura za watu, mimea na wanyama) walipatia mandhari umbo waliposafiri kutoka eneo moja hadi lingine wakisafiri. Leo kama vile hapo zamani, elimu hii inasimuliwa, kudumishwa na kupitishwa kwa wengine kupitia kwa sherehe, nyimbo dansi, sanaa na ufundi-sanii. Kwa hivyo, mandhari ya ardhi ambayo kwa wageni itaonekana kuwa ya asilia kwa hakika ina maana kamili ya kitamaduni iliyobuniwa na taratibu za kitamaduni.*

*World Heritage Newsletter, Nambari 10, Machi 1996.*



© UNESCO 2004



*Mbuga ya wanyama ya kitaifa Uluru-Kata Tjuta, Australia.*
*© S. Titchen*

*Kila mara tumekuwa tukisema ya kuwa ardhi ni muhimu kwetu kwa sababu ya Tjukurpa, sasa watu wengine kutoka ng'ambo na pia wale wasio wenyeji wanatambua hivyo na jambo hili lina maana kitamaduni—linanifurahisha kwani hali hii hatimaye imetambuliwa. Hapo awali watu wengine walitucheka na kusema tunaota lakini Tjukurpa ni halisi, ni sheria yetu, lugha yetu, ardhi yetu na jamii yetu pamoja.*

Yami Lester, Mwenyekiti, Halmashauri ya Usimamizi wa Uluru-Kata Tjuta.



© UNESCO 2004

Kutia sahihi kwa *Mapatano* hakuelezi kwa mara moja jinsi kitambulishi na asili za tamduni zetu zinavyoingiliana na ulimwengu. Tunaweza kuelewa umuhimu wa kuhifadhi urithi wetu wa kitaifa na wa kikabila, lakini itakuwa vigumu kuelewa ya kuwa tunahusiana na wengine. Njia moja ya kutulinganisha ni kuutazama ulimwengu kama bahari ya visiwa vya kitamaduni, au bahari ya mwamba tumbawe (coral reef).

*Mbuga ya majini ya ya mwambu tumbawe Tubbataha, Ufilipino.*
*© IUCN/J. Thorsell*




*Mwamba tumbawe hujengwa na safu nyingi za wanyama wa marijani (coral), lakini ni safu ya juu tu ambayo ina uhai. Baada ya miaka michache wanyama hawa hufa na safu nyingine ya wanyama inapaa juu yao. Kwa kila safu ya wanyama waliohai, mwamba tumbawe unabadilika kidogo, unakuwa mrefu, mkubwa kidogo. Inaonekana kama kwamba kila mnyama anasonga kivyake, lakini kwa hakika amekwama kwenye vizazi vya kale na hawezi kujitoa. Kila mnyama aliye hai anaonekana kama hajashikanishwa na wengine walio hai. Lakini, wanyama wachache wa mwamba tumbawe chini ya bahari wanaonekana kuwa sehemu ya mwamba huo huo. Kwa hivyo, safu fulani za mwamba huo zikiangamizwa—kwa hujuma au uchafuzi wa mazingira, unaweza kuwazia kitakachotendekea sehemu nyingine ya mwamba tumbawe. Dunia yetu ni kama mwamba tumbawe. Imejengwa na maelfu ya vizazi kabla yetu—mawazo yao, vitendo vyao na walioyatekeleza. Hii ni sehemu yetu inayotupatia nafsi yetu. Kitambulishi chetu na urithi wetu.*

Thomas Hyllard Erikson, Profesa wa Anthropolojia, Chuo Kikuu cha Oslo, Norway



© UNESCO 2004



# Kupitia kwa mitaala: Urithi wa Ulimwengu na kitambulishi

## Sanaa

Chora maeneo ya Urithi wa Ulimwengu ambayo ni mifano ya hali ya juu ya werevu na ubunifu wa binadamu na uwazie kuhusu vitambulisho tofauti vya wajenzi wake na kwa mandhari ya kitamaduni watunzaji wake.

## Lugha za Kigeni

Soma makala katika lugha nyingine na uchunguze maneno ambayo yanapatikana katika lugha yako na mjadiliane ni kwa nini maneno haya yanafanana na hali hii inavyodokeza kuhusu mwingiliano wa tamaduni katika nchi yako.

Tafsiri kwa lugha nyingine gazeti lenye habari juu ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu katika nchi yako. Tafuta maneno au dhana ambazo zinahitaji kuelezwa ambazo hazitiliwi maanani katika makala ya kwanza na ujadili yanayodokeza kuhusu kitambulishi cha watu.

## Jiografia na sayansi

Chunguza Orodha ya Urithi wa Ulimwengu na ueleze uhusiano baina ya watu na maeneo ya kijiografia. Jadilianeni nafasi ya asilia katika harakati ya kubuni kitambulishi cha watu katika hali tendaji, kwa mfano, kama umuhimu wa miti nchini Norway.



## Historia

Tumia uigizaji, katika eneo la Urithi wa Ulimwengu au eneo la kitamaduni au asilia, ili kuwahimiza wanafunzi kujihusisha na hali za watu waliotengeneza maeneo hayo au wanaoishi hapo sasa.

## Lugha/fasihi

**Andika** insha juu ya umuhimu wa kuhifadhi kitambulishi cha utamaduni na uyaendeleze baadhi ya mawazo haya yawe katika tamthilia fupi.

**Shiriki** katika mashindano ambapo wanafunzi watawasilisha hotuba za dakika tano kutetea ulindaji wa eneo mahsusi la asilia au kitamaduni.

**Soma** na jadiliana riwaya na hadithi fupi zinazomulika utambulisho na zinazohusiana na eneo la Urithi wa Ulimwengu na uwaulize wanafunzi kuandika hadithi zao wenyewe.

**Chunguza** iwapo kuna tamthilia mwafaka ambazo zinajadili dhana ya kitambulishi kwa kuihusisha na maeneo ya asilia na kitamaduni katika eneo lenu.

## Filosofia na masomo ya dini

**Tumia** michoro na picha za majengo ya kumbukumbu ya kidini au majengo kama nyenzo ya kueleza mfumo wa imani.

**Zingatia** na uelewe ishara tofauti unapotembelea eneo la kidini (kanisa, msikiti, hekalu au hata mandhari ya kidini).



**'Watalii 500,000,000 wazuru maeneo 552 ya Urithi wa Ulimwengu mwaka wa 1998'**

# Urithi wa Ulimwengu na Utalii


**Ukurasa**

**Malengo** **103**

Maarifa 103
Mielekeo 103
Ujuzi 103

**Utalii: Finomena ya ulimwengu kote na biashara kubwa** **104**

**Harakati za wanafunzi za 23:** Kukisia mielekeo ya utalii 105
**Ukurasa wa harakati za wanafunzi:** Takrimu za utalii wa ulimwengu Chati ya I 106
**Ukurasa wa harakati za wanafunzi:** Takrimu za utalii wa ulimwengu Chati ya II 107
**Ukurasa wa harakati za wanafunzi:** Takrimu za utalii wa ulimwengu Chati ya III 108
Faida na uwezekano wa tisho kutoka kwa utalii kwa uhifadhi wa maeneo ya urithi 109
**Harakati za wanafunzi za 24:** Faida na uwezekano wa tisho la utalii kwa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu 110
Umuhimu wa mfumo mpya wa utalii 110

**Urithi wa Ulimwengu, utalii na maendeleo yanayohifadhi mazingira** **111**

**Harakati za wanafunzi za 25:** Urithi wa Ulimwengu na mchezo kuhusu utalii 112
**Ukurasa wa harakati za wanafunzi:** Urithi wa Ulimwengu na mchezo kuhusu utalii 113
**Harakati za wanafunzi za 26:** Watalii wenye nidhamu na waliokosa nidhamu
Mwongozo wa kijumla wa nidhamu ya utalii 114

**Maeneo zaidi ya Urithi wa Ulimwengu ya kutembelewa** 115

**Harakati za wanafunzi za 27:** Kuchunguza huduma na vifaa katika maeneo ya urithi 116
**Ukurasa wa harakati za wanafunzi:** Kuchunguza hudum na vifaa vya kutumiwa na watalii katika meneo ya urithi 117


**Utalii kupitia kwa mdahalishi na Urithi wa Ulimwengu** **118**

**Usimamizi wa utalii katika maeneo ya Urithi wa Ulimwengu** **119**

**Harakati za wanafunzi za 28:** Ujenzi wa barabara kuu kupitia eneo la Urithi wa Ulimwengu 120
**Ukurasa wa harakati za wanafunzi:** Ujenzi wa barabara kuu kupitia eneo la Urithi wa Uilmwengu 121

**Kupitia kwa mitaala: Urithi wa Ulimwengu na utalii** **122**

# Malengo



## Maarifa

Kuwasaidia wanafunzi kukuza elimu na uelewaji wa

- Mielekeo katika utalii na athari inayoweza kutokea kwenye maeneo ya Urithi wa Ulimwengu
- Jinsi utalii unavyoweza kutusaidia kujifunza zaidi kuhusu urithi, tamaduni zingine, thamani na mila zingine
- Haja ya usimamizi wa maeneo kuhusisha usimamizi wa wageni

## Mielekeo

Kuwahimiza wanafunzi :

- Kuelewa haja ya kuanzisha mfano mpya wa utalii unaojali na kutilia maanani uhifadhi
- Kuwazia na kuheshimu hatua zilizochukuliwa za kulinda maeneo ya Urithi wa Ulimwengu dhidi ya utalii halaiki.

## Ujuzi

Kuwasaidia wanafunzi kukuza ujuzi wao wa:

- Kujifunza jinsi ya kufasiri na kuchambua takwimu ili waelewe vyema uhusiano baina ya mielekeo ya utalii na uhifadhi wa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu
- Kimsingi wa kuwawezesha kuwa waongoza-afari katika maeneo ya Urithi wa Ulimwengu
- Kuzuru maeneo ya kitamaduni na asilia kwa heshima na kwa kuwajibika
- Kukuza ufikiriaji wa kibunifu kuwasilishaji maeneo ya Urithi wa Ulimwengu wafurahie watalii wakinzingatia uhifadhi wa maeneo hayo.



Awwani

# Utalii: Finomena ya ulimwengu wote na biashara kubwa

*Hakuna mtu yeyote au utamaduni yowote ambao unaweza kuendelea bila harakati za kuingiliana na watu na tamaduni zingine. Lazima tujifunze kutambua kuwa kila utamaduni unakopa kwa tamaduni zingine. Tunahitajika kutambua kuwa utalii wa kitamaduni unaweza kuwa njia mojawapo zalishi na ambayo inaweza kuleta masikilizano baina ya ustaarabu mbali mbali. Kukutana na wengine pia husaidia watu kuthamini utamaduni na urithi wao na kuelewa mazingira yao ya asilia.*
Koichiro Matsuura, Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO katika Muungano Mkuu wa Mawaziri wa Mazingira, Nairobi, Februari 8, 2001.

Mojawapo wa *shughuli* kubwa ulimwenguni katika miaka arobaini iliyopita imekuwa ni ongezeko la utalii wa *halaiki*. Utalii huu umeathiri sana idadi ya watu wanaotembelea maeneo ya Urithi wa Ulimwengu.

Kwa sababu ya maendeleo ya haraka ya teknolojia ya usafiri, hali ya maisha kuboreka, mapumziko yaliyogharamiwa na muda wa kustarehe, watu wanasafiri sana leo kuliko hapo kale. Kwa mfano, katika mwaka wa 1950, Shirika la Utalii la Ulimwengu (World Tourism Organization, au WTO) lilikisia kuwa utalii ulimwenguni kote ulihusisha watu milioni 25 wakilinganishwa na watu milioini 664 katika 1999. Hii inamaanisha zaidi ya mara 25 ya idadi ya watalii waliozuru miaka hamsini baadaye. Shirika la WTO linabashiri kuwa watalii bilioni moja kufikia mwaka wa 2010 na takribani billoni 1.6 kufikia mwaka wa 2020.

Watu wengi wanahamu ya kuvumbua sehemu mpya zinazovutia na kwa kuwa maeneo yaliyoandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu yana thamani ya juu ya kiulimwengu watu wengi wanaamua kuyatembelea. Kwa kuwa watu wengi huishi katika miji mikubwa, huwa na hamu ya kutembelea maeneo yanayojulikana kwa uzuri wa maeneo ya urithi wa kiasilia. Matembezi ya aina hii mara nyingine hujulikana kama utalii wa kimazingira, ilhali utalii wa kitamaduni hurejelea utalii katika maeneo ya kitamaduni.

**Mtalii**

Anayefanya ziara, hasa anayefanya hivi kwa kujipumzisha; anayetembea kwa kujifurahisha au utamaduni, kutembelea mahali fulani kwa sababu ya vitu vinavyovutia kama mandhari na kadhalika.
*Shorter Oxford Dictionary*

**Utalii**

Nadharia na hali ya utendaji ya kuzuru; kusafiri kwa kufariji.
*Shorter Oxford Dictionary*



*Watalii wanazuru Mont-St-Michel na bandari yake, Ufaransa.*
*© Patrimoine 2001/D. Chenot*

© UNESCO 2004

Utalii mara nyingi huhusishwa na maendeleo kwa kuwa hutoa kazi na huleta pesa za kigeni ambazo huhitajika sana. Kwa mfano, katika mwaka wa 1950 ilikisiwa ya kuwa watalii walitumia dola za marekani milioni 2.1 ikilinganishwa na dola za marekani bilioni 486 katika mwaka wa 2002.

Kwa habari zaidi juu ya mielekeo ya utalii unaweza kurejelea tovuti la Shirika la Utalii la Ulimwengu (http://www.world-tourism.org)


*Utalii hauwezi kuwepo bila utamaduni, kwa kuwa utamaduni ni mojawapo wa mambo yanayowamotisha watu kutembea.*
*Proceedings of a Round Table on Culture, Tourism and Development: Crucial Issues for the Twnty-firt Century, uk. 7, UNESCO Juni 26–27 1996.*



## ■ Harakati za wanafunzi za 23

## KUKISIA MIELEKEO YA UTALII

### Lengo: Kujifunza kuhusu mielekeo ya utalii ya ulimwengu na yanayodokezwa na idadi ya watalii wanaotembelea maeneo ya uhifadhi wa urithi wa ulimwengu.



**Utafiti** | **Harakati darasani** | **Kipindi kimoja au zaidi** | **Hesabu, masomo ya jamii** | **Kurasa za harakati za wanafunzi, tawkimu juu ya utafiti wa ulimwengu, kikotoo (calculator), Ramani ya Urithi wa Ulimwengu, picha**

✓Waonyeshe wanafunzi wako chati ya 1 ya Ukurasa wa harakati za wanafunzi (wakilisha nakala kwa kila mwanafunzi). Eleza data kwa wanafunzi na uandae habari kuhusu kukusanya, kufasiri na kutumia takwimu. Waulize wanafunzi watumie Ramani ya Urithi wa Ulimwengu kuchunguza idadi ya maeneo ya urithi katika nchi 15 zinazotembelewa sana. Wambie wachunguze uhusiano huo (yaani iwapo idadi ya maeneo haya katika nchi tofauti inaweza kueleza idadi kubwa ya watalii) na kasha uwaulize waziweke nchi kumi zinazotembelewa sana katika maeneo ya kijiografia: Afrika, Bara la Marekani na Karibea, Bara Hindi na eneo la Pasifiki, mataifa ya Kiarabu na Uropa.

✓Wasilisha chati ya 2 kwa wanafunzi na uwaulize wayaweke mataifa hayo kumi na tano katika orodha mbili: mataifa yaliyostawi na mataifa ambayo hayajastawi sana. Je, kuna uhusiano baina ya mataifa yaliyostawi na uchumaji wa juu kutoka kwa utalii na maeneo ya Urithi wa Ulimwengu? Jadiliana matokeo. Ni mataifa mangapi yaliyo na mapato ya juu kutoka kwa utalii yaliyo na maeneo ya Urithi wa Ulimwengu?

✓Onyesha chati ya 3 kwa wanafunzi na mjadiliane kinachomaanishwa na kasi ya ukuaji wa uchumi na kwa nini kasi ya ukuaji ni tofauti katika miongo tofauti.

✓Jaribu kupata takwimu kuhusu utalii na idadi ya watalii wanaotembelea maeneo ya urithi katika nchi yako na uwaulize wanafunzi kuwasilisha data hiyo.

## Mataifa 15 yanayotembelewa zaidi na watalii

Idadi ya watalii wanaowasili

**Chati 1**

| Nr. | Nchi | Mapato kutoka utalii wa kimataifa (mabilioni) 1999 | 2000 | Mabadiliko asilimia 2000/1999 | Magao wa soko 2000 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ufaransa | 73.0 | 75.5 | 3.4 | 10.8 |
| 2 | Marekani | 48.5 | 50.9 | 4.9 | 7.3 |
| 3 | Uhispania | 46.8 | 48.2 | 3.0 | 6.9 |
| 4 | Italia | 36.5 | 41.2 | 12.8 | 5.9 |
| 5 | Uchina | 27.0 | 31.2 | 15.5 | 4.5 |
| 6 | Uingereza | 25.4 | 25.2 | −0.8 | 3.6 |
| 7 | Shirikisho la Urusi | 18.5 | 21.2 | 14.5 | 3.0 |
| 8 | Mexico | 19.0 | 20.6 | 8.4 | 3.0 |
| 9 | Canada | 19.5 | 20.4 | 4.9 | 2.9 |
| 10 | Ujerumani | 17.1 | 19.0 | 10.9 | 2.7 |
| 11 | Austria | 17.5 | 18.0 | 2.9 | 2.6 |
| 12 | Poland | 18.0 | 17.4 | −3.1 | 2.5 |
| 13 | Hungary | 14.4 | 15.6 | 8.1 | 2.2 |
| 14 | Hong Kong (Uchina) | 11.3 | 13.1 | 15.3 | 1.9 |
| 15 | Ugiriki | 12.2 | 12.5 | 2.8 | 1.8 |

Takwimu kutoka: Shirika la Utalii la Ulimwengu (WTO), data *imekusanywa mpaka* Agosti 2001

## Mataifa kumi yanayonufaika zaidi kutokana na utalii

**Chati II**

Idadi ya watalii wa kimataifa

| Nr. | Nchi | Mapato kutoka utalii wa kimataifa (US$ bilioni) 1999 | Mapato kutoka utalii wa kimataifa (US$ bilioni) 2000 | Mabadiliko (asilimia) 2000/1999 | Mgao wa soko 2000 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Marekani | 74.9 | 85.2 | 13.7 | 17.9 |
| 2 | Uhispania | 32.4 | 31.0 | –4.3 | 6.5 |
| 3 | Ufaransa | 31.5 | 29.9 | –5.1 | 6.3 |
| 4 | Italia | 28.4 | 27.4 | –3.2 | 5.8 |
| 5 | Uingereza | 20.2 | 19.5 | –3.4 | 4.1 |
| 6 | Ujerumani | 16.7 | 17.8 | 6.5 | 3.7 |
| 7 | Uchina | 14.1 | 16.2 | 15.1 | 3.4 |
| 8 | Austria | 12.5 | 11.4 | –8.7 | 2.4 |
| 9 | Canada | 10.2 | 10.8 | 5.9 | 2.3 |
| 10 | Ugiriki | 8.8 | 9.2 | 5.0 | 1.9 |
| 11 | Australia | 8.0 | 8.4 | 5.3 | 1.8 |
| 12 | Mexico | 7.2 | 8.3 | 14.8 | 1.7 |
| 13 | Hong Kong (Uchina) | 7.2 | 7.9 | 9.4 | 1.7 |
| 14 | Uturuki | 5.2 | 7.6 | 46.8 | 1.6 |
| 15 | Shirikisho la Urusi | 7.5 | – | | |

Takwimu kutoka: Shirika la Utalii la Ulimwengu (WTO), data imekusanywa mpaka Agosti 2001

## Utabiri wa utalii wa kipindi kirefu wa WTO, Vision 2020 — Chati III

Utabiri wa utalii wa maeneo

Watalii wa kimataifa watakaofika katika maeneo mbali mbali (mamilioni)

| | Kuanzia mwaka | Utabiri | | Ukuaji wa wastani katika kwa mwaka (asilimia) | Asilimia ya mgao wa soko (%) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1995 | 2010 | 2020 | 1995–2020 | 1995 | 2020 |
| Afrika | 20.2 | 47.0 | 77.3 | 5.5 | 3.6 | 5.0 |
| Bara za *Marekani* | 108.9 | 190.4 | 282.3 | 3.9 | 19.3 | 18.1 |
| Bara *Hindi* Mashariki na Pacifik | 81.4 | 195.2 | 397.2 | 6.5 | 14.4 | 25.4 |
| Uropa | 338.4 | 527.3 | 717.0 | 3.0 | 59.8 | 45.9 |
| Guba la Kati | 12.4 | 35.9 | 68.5 | 7.1 | 2.2 | 4.4 |
| Bara Hindi Kusini | 4.2 | 10.6 | 18.8 | 6.2 | 0.7 | 1.2 |
| Baina ya nchi | 464.1 | 790.9 | 1,183.3 | 3.8 | 82.1 | 75.8 |
| Usafiri wa mbali | 101.3 | 215.5 | 377.9 | 5.4 | 17.9 | 24.2 |

Takwimu kutoka: *Shirika la Utalii la Ulimwengu* (WTO), data zilizohifadhiwa na WTO za Julai 2000.


1. Kwa usafiri baina ya nchi, inamaanisha pale ambapo nchi watalii wanakotoka haijatajwa.
2. Usafiri wa mbali ni usafiri wowote ambao hauhusisha usafiri ndani ya eneo hilo *hilo*.

## ▲ Faida na uwezekano wa tisho la utalii kwa uhifadhi wa maeneo yenye urithi




Utalii una faida nyingi zilizo wazi: kwa mataifa wenyeji miji na maeneo ya urithi, utalii husababisha kuwepo kwa vibarua huleta pesa za kigeni, mara nyingi husababisha kuimarishwa kwa huduma za eneo fulani kama vile barabara, mawasiliano, vifaa muhimu, na huduma za afya. Watalii wanaweza kufurahia maajabu ya ulimwengu na kujifunza kuhusu nchi zingine, mazingira yao, utamaduni, thamani zao, na njia za maisha na kwa kufanya hivi waendeleze uelewano na umoja wa kimataifa. Binadamu hujifunza mengi yanayomhusu kwa kujifunza kuhusu watu wengine.

Hata hivyo utalii unaweza kuwa na athari mbaya. Kwa mfano, mamilioni ya watalii hutembelea eneo la Urithi wa Ulimwengu la Hekalu ya Borobudur nchini Indonesia, eneo lenye joto sana na unyevunyevu. Ili kuhakikisha starehe ya watalii madereva wa mabasi ya utalii huacha magari yakiguruma na kisafisha hewa kikifanya kazi wanapowasuburi watalii kurudi kutoka ziara zao za eneo hili. Gasi ya *carbon* monoxide inayotolewa na gari inaweza kuharibu *hekalu* za mawe.



Hekalu ya Barobudur, Indonesia. © *UNESCO/ A. Voronzoff*



Misafara ya magari mengi ni hatari kuu kwa maeneo mengi ya urithi. Barabara iliyopo karibu na Stonehenge huko Uingereza imetisha hali ya eneo hili kuendelea kuwa imara. Mapendekezo ya kujenga barabara kuu karibu na viwanja vya piramidi kutoka Giza hadi Dahshur huko Misri ulisimamishwa na serikali ya Misri kutokana na pendekezo la **UNESCO.**

***Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu*** yanaporejelea maeneo yaliyo hatarini, hutaja tisho kubwa kutokana na ukuaji haraka wa mji au miradi mikubwa ya utalii (*Sehemu 11*, aya 4).

Stonehenge, Avebury na maeneo mengine Uingereza. © *UNESCO/ A. Lacoudre*

Utalii una athari nzuri na mbaya kwa maeneo ya urithi na kuna haja ya kuhakikisha kuwa athari mbaya zinaondolewa na zile njema zinapaliliwa.

Ahadi ya wanafunzi World Heritage Youth Forum, Bergen, Norway,



## ■ Harakati za wanafunzi za 24

## FAIDA NA UWEZEKANO WA TISHO LA UTALII KWA MAENEO YA URITHI WA ULIMWENGU

### Lengo: Kuelewa vizuri faida na uwezekano wa tisho la utalii kwa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu



**Majadilian o** | **Harakati darasani** | **Kipindi kimoja** | **Lugha, Masomo ya jamii** | **Makaratas i mawili makubwa**

Wapange wanafunzi katika makundi mawili makubwa na uulize kundi moja kutayarisha orodha ya faida ya utalii kwa eneo la karibu au kwa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu. Mualike mwanafunzi mmoja kutoka kila kikundi awasilishe orodha ya kikundi chake na wajadiliane pamoka jinsi tisho la utalii linavyoweza kupunguzwa.

## ▲ Umuhimu wa mfumo mpya wa utalii



Utalii huwafanya watu kuthamini tofauti za kitamaduni, desturi tofauti za maisha na mazingira ya kiasilia. Inatoa nafasi muhimu za watu wachanga kuingiliana kitamaduni.

*Utalii unaweza … kuandaa funzo la kuvumiliana pale ambapo kila mmoja anaweza kukumbana na ulimwengu wa kipekee na wenye tofauti.*
Maoni haya yametokwa kwa Proceedings of a Round Table on Culture, Tourism and Development: Crucial issues for the 21st century. uk. 7. Paris, UNESCO 26–27 June 1996.

Hata hivyo utalii unaweza kusababisha tofauti za kiuchumi na kijamii iwapo huduma za kimsingi (hoteli, mabwawa ya kuogelea, n.k.) zitajengewa watalii na kukwamiza juhudi za ujengaji wa shule au mahospitali kwa faida ya wenyeji.

Mfumo mpya wa utalii unahitajika ambao utaunga mkono maendeleo yatakayodumisha hali ya ikolojia na kutia moyo nchi husika kushikilia vitambulishi vya kitamaduni ili kufanya mazingira yao yatunzwe vyema zaidi na kuthaminiwa na wageni. Na vile vile mazungumzo baina ya watu wa tamaduni tofauti, hali ya kuheshimiana na umoja unahitaji kudumishwa. Kwa mataifa ambayo yana upungufu wa maji watalii wanaweza kuonyesha moyo wa kushirikiana kwa kutumia maji kwa uangalifu, kwa mfano, kutotarajia taulo na matandiko ya vitanda kufuliwa kila siku.

© UNESCO 2004

# Urithi wa Ulimwengu, utalii na maendeleo yanayohifadhi mazingira

Urithi wa Ulimwengu na mazingira

*Utalii unaweza kuchangia maendeleo ya hali ya juu kama yatawahusisha na kushirikisha wenyeji wa eneo husika, ambao wanastahili kuhusishwa wakati wa kupanga na kutekeleza maendeleo hayo, na iwapo rasilmali na tamaduni ambayo ndiyo msingi wa utalii zinahifadhiwa kwa mda mrefu.*
*Maoni kutoka kwa Proceedings of a Roundtable on Culture, Tourism and Development: Crucial issues for the 21st centry. p 7. Paris, UNESCO. 26–27 June 1996.*

Utalii wa halaiki unaweza kuwa na athari kubwa kwa utunzaji na uhifadhi wa maeneo ya kitamaduni (kuchakaa kutokana na idadi kubwa ya wageni) na maeneo ya *kiasilia* (kwa mfano, kuletwa kwa spishi geni na watalii, kujenga hoteli kwenye maeneo hafifu ya pwani, uchafuzi kutokana na taka za utalii). Kila eneo la urithi, hasa eneo la urithi wa kiulimwengu, lazima lisimamiwe vizuri. Ni muhimu kwa watu wachanga kuwazia juu ya mchango wao wa baadaye kwa usimamizi wa maeneo kama wamiliki wa siku za baadaye.

Tunaweza kudhamini na kuona maeneo haya yote kwa sababu mababu zetu waliyahifadhi tuyaone. Kwa upande wetu ni jukumu letu kuyahifadhi ili watoto wetu nao pia wayadhamini maeneo haya.
Mapendekezo ya Wanafunzi, Muungano wa Vijana wanaohusika na Urithi wa Ulimwengu, Beijing, Uchina.

III

*Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu yanastahili kuwa kielezo cha usimamizi na uhifadhi imara. Hata hivyo kwa bahati mbaya, hali ya juu inayotarajiwa kwa maeneo haya haipatikani katika hali za sasa. Lakini ziara na utalii uliosimamiwa vyema wenye kujali mazingira kwa muda mrefu huyaletea maeneo haya fedha na kuchangia uhifadhi wa muda mrefu.*
*Tourism, Eco-tourism and Protected Areas*
*H. Ceballos-Lascurair (mhariri.), IUCN 1996.*


© UNESCO 2004



## ■ Harakati za wanafunzi za 25

# URITHI WA ULIMWENGU NA MCHEZO KUHUSU UTALII

## Lengo: Kufurahia wakati wa kuelewa maswala muhimu yanayohusika katika usimamizi wa maeneo na *utalii*



| Uigizaji | Harakati darasani na nje ya darasa | Vipindi kadhaa | Lugha, masomo ya jamii | Ramani ya Urithi wa Ulimwengu Maelezo kwa ufupi, picha | Vifaa vya uigizaji |
|---|---|---|---|---|---|

Rules:

✓ Wapange wanafunzi katika *timu za wanafunzi* wawili au wane

✓ Katika kipindi cha kwanza cha darasa patia kila timu habari kuhusu eneo la Urithi wa Ulimwengu (data, picha, mahali lilipo, sifa zake, n.k.). Kila timu itawakilisha eneo lake wakati wa mchezo kwa usaidizi wa mwalimu. Kila timu itatayarisha mpango wa 'usimamizi wa *utalii*' wa *eneo* walilopewa.

✓ Katika kipindi cha pili darasani, wanafunzi wanaweza kuanza mchezo. Kila timu itatupa 'dice' na kusonga hadi mahali panapoonyeshwa. Wakati kila timu imesonga, itapatiwa muda (dakika 10 had 30) kutayarisha waliyoonyeshwa kwenye miraba. Iwapo timu itashindwa *kukamilisha jukumu*, haiwezi kusonga mbele. Wakati timu iko ndani ya mraba wenye MABANGO, itatumia wakati huo kutayarisha bango inayoeleza sifa za eneo hilo. Timu ya kwanza kufika eneo la KUMALIZA, baada ya maagizo na mabango ndiyo mshindi.

Wakati wa *kipindi cha* tatu, wanafunzi wanaweza kujadiliana matokeo yao na wawasilishe mabango yao.





*Wasimamizi wa Victoria Falls wanawafundisha wageni na wanafunzi wanaohudhuria Mungano wa vijana wa kwanza wa Eneo la Afrika wa Urithi w Ulimwengu, Zambia na Zimbabwe*
© UNESCO

© UNESCO 2004

# Urithi wa Ulimwengu na mchezo kuhusu utalii





| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| KUANZA<br>Eneo lako liko kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Andaa mpango wa usimamizi wa utalii kwa timu zingine. 1 | BANGO 2 | BANGO 3 | Eneo linapatwa na janga la kiasilia. Eleza kilichotokea (ukitilia maanani sifa la eneo lako, na uharibifu uliotokea)<br>Rudia sehemu ya KUANZA 4 | BANGO 5 | Kuna takataka nyingi kwenye eneo lako. Andika njia tano za kukabiliana na hali hii.<br>Songa *mbele* miraba minne 6 |
| BANGO 7 | BANGO 8 | BANGO 9 | Kituo cha kutoa habari cha eneo lako kimeingiliwa kwa kukosa maeneo ya huduma muhimu. Andikia wageni barua kwa wageni *ukiomba* michango ya kurekebisha kituo hicho.<br>Rudi nyuma miraba 5 10 | BANGO 11 | Rekodi kubwa ya watalii wanatembelea eneo lako. Pesa zinazopatikana zinakuwezesha kuanzisha mradi wa kukarabati mpya. Ni nini utakachopatia kipaumbele na kwa nini. Eleza haya kupitia kwa *mchoro* bila maneno.<br>Songa mbele miraba 5 12 |
| Sehemu ya eneo imeporomoka kutokana na kutotunzwa vyema. Andika orodha ya shida (angalau tano) na utatuzi utakaotolewa.<br>Rudia sehemu ya KWANZA 13 | Ombi la pesa za uhifadhi limefaulu. Andika ombi hili, na utaje sababu za kueleza ka nini unstahili kuzipata.<br>*Songa* mbele miraba tano 14 | Hoteli mpya *ya kitalii* imejengwa msimamizi anaelewaumuhimu wa uhifadhi wa urithi wa ulimwengu. Andika tangazo ya hoteli hii, lichapishwe kwenye jarida.<br>Songa mbele miraba mine. 15 | Ukaguzi wa mipango wa ICOMOS *wa* miaka mitano unapinga rekodi yako ya uhifadhi.<br>Rudi nyuma miraba tisa 16 | BANGO 17 | Eneo lako lilionyeshwa kwenye televisheni.<br>Songa mbele miraba mitatu. 18 |
| BANGO 19 | Watalii wengi kupindukia walitembelea eneo lako na kusababisha mmonyoko mkuu. Andika faida tano na hasara tano za utalii katika eneo lako.<br>Rudi nyuma miraba kumi na moja. 20 | BANGO 21 | Hoteli yako ililazimika kufungwa kwa sababu paa linavuja.<br>Rudi nyuma miraba tano. 22 | BANGO 23 | KUMALIZA<br>Una eneo lililohifadhiwa vizuri linalo mpango mzuri wa usimamizi. Andika ripoti juu ya mpango wa usimamizi, shida mnazokabiliana nazo na utatuzi unaotumika 24 |



## ■ Harakati za wanafunzi za 26

# WATALII WENYE NIDHAMU NA WALIOKOSA NIDHAMU

## Malengo: Kuwa mtalii wa kuheshimika

|  |  |  |  |  |  |
|---|---|---|---|---|---|
| **Uigizaji** | **Harakati darasani na nje ya darasa** | **Vipindi kadhaa** | **Lugha, masomo ya jamii** | Ramani ya Urithi wa Ulimwengu Maelezo kwa ufupi, picha | **Vifaa vya uigizaji** |

✓Waagize wanafunzi waandike na waigize tamthilia juu ya mtalii mwenye tabia mbaya, asiyeheshimu maeneo, anayesambaza takataka, mara nyingine anaharibu eneo kwa kuchora michoro isiyo na maana, anapuzi utamaduni na mila za eneo hilo na ambaye anajali tu starehe yake. Mtalii mwenye heshima ana haja ya kujifunza kuhusu utamaduni na mila za eneo fulani (historia ya eneo, ufundi-sanii na kazi za kisanaa, muziki, chakula, mavazi, n.k.). Baada ya tamthilia kuandikwa na kuigizwa na wanafunzi, wajadili jinsi mtalii wa aina hii anavyoweza kubadilishwa na kuwa mtu anaependelea kutembelea maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na kuyaheshimu kwa kufuata mwongozo uliopo hapa chini.

✓Waagize wanafunzi wachague eneo la urithi la sehemu wanapoishi, la kitaifa au la kiulimwengu na utayarishe orodha ya mapendekezo ya kampeini ambayo itawaongoza watalii wanapozuru eneo. Jadilianane mapendekezo na muyapitie pamoja na shirika la utalii la eneo hilo au jumuiya ya urithi.



## Mwongozo wa kijumla wa nidhamu

Wakati wa kupanga safari watalii wanastahili:

1. Kujifunza mengi iwezekanavyo kuhusu eneo la ziara
2. Kutembelea watoa huduma (mashirika ya ndege, wapangaji safari na hoteli) ambao wanadhihirisha kujali mazingira
3. Kupanga mapumziko na ziara wakati kilele cha safari kimeshuka
4 Kutembelea maeneo ambayo kwa kawaida hayatembelewi sana.

Baada ya kufika watalii wanastahili:

1. Kuheshimu tamaduni na mila za wenyeji
2. Kufikiria kuhusu uhuru wa kutoingiliwa, utamaduni, tabia, mila za jamii wenyeji
3. Kuunga mkono uchumi wa eneo hilo kwa kununua bidhaa za hapo na kutumia huduma zao
4. Kuchangia juhudi za uhifadhi
5. Kuhifadhi na kutunza mazingira ya kiasilia, mfumo-ikolojia na wanyama pori
6. kutoharibu maeneo ya kitamaduni na majengo ya kumbukumbu
7. Kutumia kawi na maji kwa uangalifu na kuondoa taka kwa njia mwafaka
8. Kutahadhari kuhusu moto
9. Kutopiga kelele bila sababu
10. Kutumia barabara na vibarabara vilivyoruhusiwa kutumiwa.

Mwongozo wa *General Behaviour Guidelines for Tourists, Environmental Codes of Conduct for Tourism*, United Nations Environment Programme

© UNESCO 2004


## Maeneo zaidi ya Urithi wa Ulimwengu ya kutembelea

Katika mwaka wa 1978 maeneo 12 ya kwanza yaliandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Kufikia mwaka wa 1987 tayari kulikuwa na maeneo 289 kwenye orodha na miaka 17 baadaye, mwaka 2004, orodha ilikuwa na maeneo 754. Kila mwaka kamati ya Urithi wa Ulimwengu inaongezea maeneo zaidi kwenye orodha. Watu wachanga waliohudhuria mkutano wa vijana wa Urithi wa Ulimwengu wa UNESCO walieleza rai yao ya kutaka kutembelea maeneo mengi ya Urithi wa Ulimwengu iwezekanavyo. Hata hivyo shule nyingi ziko mbali na maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na ni ghali kuyatembelea. Wanafunzi kwa hivyo wakapendekeza waondolewe ada ya kuingia au ipunguzwe kwa makundi ya wanafunzi na kuwa wafanyi biashara wa maeneo husika wanaweza kusaidia kufadhili usafiri wa wanafunzi wanaotembelea maeneo ya Urithi wa Ulimwengu. Kufikia lengo hili shule zingine zinafanya shughuli mbali mbali za uchangishaji wa pesa (uuzaji wa keki na peremende, kuosha magari, kupanga sherehe za nyimbo na uigizaji unaolipishwa ada ya kuingia, n.k.) ili kugharamia matembezi ya shule zao katika maeneo ya Urithi wa Ulimwengu.

Upangaji wa kimakini unahitajika ili kuhakikisha ziara za wanafunzi kwa maeneo ya kiasilia na kitamaduni yanawafurahisha. Ingawaje ziara kwa hakika zinaweza kuchangia kuchakaa kwa maeneo, zikipangwa vizuri zinaweza kuwachochea wanafunzi kujitolea kwa shughuli za muda mrefu za kuyalinda na kuyahifadhi.




*Mji wa kihistoria wa Sukhothai na miji majirani ya kihistoria, Thailand.*
*© Patrimoine 2001/P. Aventurier*



© UNESCO 2004

## ■ Harakati za wanafunzi za 27



# KUCHUNGUZA HUDUMA NA VIFAA KATIKA MAENEO YA URITHI

## Lengo: Kupata stadi za kuchunguza vifaa katika maeneo ya urithi ili kuviboresha



**Utafiti**



**Harakati darasani**




**Harakati nje ya darasa**



**Vipindi viwili vya darasani na muda baada ya masomo**



**Lugha, jiografia, masomo ya jamii.,**



***Kurasa* za harakati za wanafunzi kuchunguza huduma na *vifaa* katika maeneo ya urithi**

✓Panga ziara ya *eneo* la *urithi lililo* karibu ambalo ni maarufu kwa watalii.

✓Toa nakala za harakati za wanafunzi na umpatie kila mwanafunzi nakala moja.

✓Wapatie wanafunzi habari kuhusu eneo ambalo watazuru na uwaeleze umuhimu wa kukamilisha fomu na kuandika ripoti.

✓Wanafunzi wanapokupatia ripoti zao wakabidhi muhtasari wa waliyoyaona na mujadiliane jinsi huduma na vifaa katika eneo hili vinavyoweza kuboreshwa.



Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu yanastahili:

- Kuchunguza idadi ya watalii wanaozuru eneo fulani ili kuzuia uharibifu wa maeneo dhaifu.
- Yawe na vinjia vya kutembelea vya wazee na walemavu.
- Yasiwe na maeneo ya kibiashara nje ya eneo kuu la urithi.

Mapendekezo ya wanafunzi, Muungano wa Wanafunzi Wanaohusika na Urithi wa Ulimwengu, Beijing, Uchina

© UNESCO 2004

■ Wanafunzi wanahitajika kutathmini hali ya vifaa kwa kuweka alama katika eneo mwafako

| [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] |
|---|---|---|---|---|
| [illegible] | | | | |
| [illegible] | | | | |
| [illegible] | | | | |
| [illegible] | | | | |
| [illegible] | | | | |
| [illegible] | | | | |
| [illegible] | | | | |
| Usafi | | | | |
| Viongozi wa [illegible] | | | | |
| Viburudisho | | | | |
| Na mengine | | | | |

**Ripoti kwa msimamizi wa eneo la urithi**

Kwa Bibi/Bwana

Nimetembelea eneo lako hivi karibuni na kufikia uamuzi kuwa.

❑ Vifaa na huduma katika eneo lako vinatosha

❑ Vifaa na huduma katika eneo hilo havitoshi na vinastahili kuboreshwa kwa njia ifuatayo:

. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

Natarajia ripoti hii itakuwa ya manufaa kwa maendeleo ya baadaye ya eneo lako. Wako mwaminifu,

**Jina:** **Sahihi:** **Tarehe:**

*Wanafunzi wanastahil kukamilisha ripoti zao na kumpatia mwalimu*

# Utalii kupitia kwa mdahalishi na Urithi wa Ulimwengu

Kwa kupitia teknolojia mpya ni rahisi 'kutembelea' eneo la Urithi wa Ulimwengu na maeneo mengine bila kusafiri hadi kwenye eneo lenyewe. Kwa mfano mabustani ya starehe na makavazi katika nchi zingine yamebuni vielelezo vya vijiji fulani au hata sehemu za miji. Huko York, Uingereza watalii wanaweza kutembelea kijiji cha Vikings cha Jorvik, ambacho kimebuniwa upya chini ya ardhi na wasafiri hutumia gari-moshi. Kwa kutumia skrini za kuonyesha picha zilizo *'three-dimensional'* pamoja na *kiini macho* ama 'special effects', watalii wanavuitwa sana na viwanja au *'amusement parks'* ambapo watu huweze kusafiri mahali tofauti kutumia *'simulated rides'*, hata nje ya sayari yetu, kama wameshikanishwa kwa kiti maalum kinachosonga! Hii ni aina mpya ya utalii. Walimu wanaweza kujadili na wanafunzi wao faida na hasara za aina hii ya utalii, hasa kwa kuwazia kuhusu siku za baadaye.




Orodha ya marejeleo


*Mimi ni msafiri. Wewe ni mgeni. Wao ni watalii.*
*Sentensi hii inaeleza kugaflika (au paradoksia) ketu: Tunapenda kusafiri hadi maeneo pori na ya kupendeza lakini tunatishwa na athari ya idadi kubwa ya binadamu wanaosafiri kama sisi. Kila mtu anfuatilia harakati halali ya kutumia muda wake wa starehe. Hata hivyo kwa pamoja tunatisha mahali ambapo tunapapenda. Kwa hakika tumo katika hatari ya kuzipenda mbuga za wanyama za ulimwengu na mahali pengine panapolindwa hadi kupaangamiza kabisa.*

Adrian Philllips, IUCN, 1996






CD-ROM nyingi zinazidi kutolewa kuhusu maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na sasa inawezekana kutembelea, kwa mfano, zaidi ya maeneo 100 ya Urithi wa Ulimwengu yaliyo katika sehemu zote za ulimwengu. Utembezi huu hutokana na CD-ROM za UNESCO zenye miji ya Urithi wa Ulimwengu na tovuti (web site) zinazoonyesha miji kama Angkor, Kambodia. Maonyesho yaliyopangwa vizuri na kurasa-tovuti zinawapatia wanafunzi nafasi ya 'kuzuru' maeneo ya Urithi wa Ulimwengu. Iwapo unajua kutumia mdahalishi (Internet) unaweza 'kuzuru' eneo la tovuti la UNESCO linalohusu makao ya Urithi wa Ulimwengu ili ujifunze kuhusu maeneo 754 yaliyo kwenye Orodha ya ya Urithi wa Ulimwengu.



*Wanafunzi waliohudhuria Muungano wa Wanafunzi wa Urithi wa Ulimwengu huko Victoria Falls, wanajionea wanyama na mimea walipouabiri Mto Zambezi.*
© UNESCO

© UNESCO 2004

# Usimamizi wa utalii katika maeneo ya Urithi wa Ulimwengu

Tatizo kubwa la uhifadhi wa maeneo ya urithi ni kuwakubalia watu kuyatembelea bila kusababisha athari mbaya. Maeneo ambayo yamedumisha urembo wao na kutunzwa vyema kwa kutofikiwa kwa urahisi sasa yamekuwa lengo la wapangaji wa safari za watalii. Kwa hivyo kila eneo la Urithi wa Ulimwengu linahitaji usimamizi bora.

Ukuta Mkuu wa Uchina uliandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu mnamo 1987. Sehemu ya ukuta huu mkuu inayotembelewa na mamilioni ya watalii kila mwaka ni eneo lililojengwa kwa tofali na mawe karibu na Beijing wakati wa utawala wa kifamilia wa Ming Dynasty. Mabaki ya kuvutia, mengine ya miaka 2000 yanaweza kuonekana katika Jangwa la Gobi liliko Gansu. Hali ya ukame ya jangwa hili imehifadhi vitu hivi dhaifu. Mabaki ni kama vile ngome za matope na hata mafungu ya matete yaliyowekwa tayari kuwashwa kama ishara ya mashambulizi, kutoka kwa wahamahamaji wa kaskazini. Eneo hili la ukuta limetembelewa na watalii wachache, na kuna hofu ya kuwa uongezekaji wa wageni unaweza kuhatarisha mabaki dhaifu ya eneo hili.

Ramani ya Urithi wa Ulimwengu

Mojawapo wa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu ya kiasilia ya kupendeza na kushangaza sana ni Te Wahipounamu iliyopo Kisiwa Magharibi mwa New Zealand. Uzuri wake wa kiasilia umehifadhiwa vizuri. Umbali wa New Zealand na nchi zingine umesaidia uhifadhi viumbe vingi na vya kipekee. Hata hivyo uongezekaji mkubwa wa idadi ya watalii na uimarishaji wa usafiri umewasaidia watalii wengi kufika New Zealand. Kumekuwa na majadiliano mengi katika miaka ya hivi karibu kuhusu ujenzi wa barabara kuu kupitia eneo hilo na kuunganisha miji miwili ya Haast na Milford, kurahisisha usafiri wa watalii. Ujenzi huu utasababisha faida na hasara pia, ambazo zitachunguzwa zaidi katika harakati za wanafunzi za 28.

Urithi wa Ulimwengu na mazingira



*Te Wahipounamu, New Zealand.*
*© UNESCO / F. Dondou*



© UNESCO 2004



## ■ Harakati za wanafunzi za 28

# UJENZI WA BARABARA KUU KUPITIA ENEO LA URITHI WA ULIMWENGU

### Malengo: Kuelewa maslahi na maoni tofauti kuhusiana na maendeleo, utalii na Urithi wa Ulimwengu



**Uigizaji**



**Harakati darasani**




**Harakati nje ya darasa**



**Vipindi kadhaa na muda baada ya masomo**



**Jiografia, hesabu, sayansi, lugha**



***Kurasa za* harakati za wanafunzi: kujenga barabara kuu kupitia ndani ya eneo la Urithi wa Ulimwengu, Maelezo kwa ufupi, Ramani ya Urithi wa Ulimwengu**

✓ Wapange wanafunzi katika makundi na usambaze nakala ya ukurasa wa harakati za wanafunzi kwa kila kikundi. Waulize wanafunzi waoanisha taarifa zilizoandaliwa na picha inayoelezwa na taarifa hizo. Kisha kila picha ipewe nambari na *kila kikundi kipewe nambari* (1 hadi 5). Uliza kila kikundi kukuza taarifa ya nambari waliyopewa.

✓ Iwapo wanafunzi wamekamilisha kutayarisha taarifa zao, kila kikundi kitamkabithi mmoja wao wadhifa wa *kushiriki katika mjadala* utakaopangwa darasani ili kutetea maoni ya picha ya mhusika wao. Kila kikundi kitateua mwanachama mmoja kama mojawapo wa waamuzi watakao amua baada ya mjadala iwapo barabara itakubaliwa kupitia hapo au la.




© UNESCO 2004



*1. Jambo la mwisho ambalo New Zealand inahitaji ni barabara zinazoelekea mwituni. Itakuwa na athari mbaya sana katika eneo ambalo ni la kiasilia na haina maana kiuchumi. Inabadilisha tu njia inayotumiwa na watalii kufika New Zealand bila hata kuwavutia kwa wingi na hata hatuwahitaji wengi. Haitatendeka.*

Mkurugenzi, Shirika la Ulinzi wa Misitu na ndege.



*2. La muhimu, tunachukulia hatua hii kama jibu la kuongezea utalii katika sehemu ya pwani. Barabara hii itachukua nafasi ya kila kitu ambacho tumepoteza. Iwapo asilimia kumi ya basi zinazokwenda Milford zinaweza kuja hadi pwani ya magharibi itaongeza biashara yetu ya utalii maradufu.*


Msimamizi Mkuu, Westland Country Council



*3. Barabara katika sakafu ya Bonde itasababisha utatizi wa mfumo ikolojia wa kinamasi ulio hafifu na barabara itakayopita kando kando ya vilima itaharibu mandhari.*


Mhifadhi wa misitu





*4. Sura ya nchi na mandhari ni ya kupendeza sana. Itafanya New Zealand kufikia kiwango kipya na hata kuendeleza utalii wa kimataifa. Sehemu ya faida itakayopatikana ni kutumia safari ya gari kutoka Haast hadi Milford.*

Waziri wa Usafiri




*5. Tukisawazisha mambo hatuoni dhara lolote katika pendekezo hasa kama uchunguzi wa uwezekano wa maendeleo hauonyeshi gharama ya kupindukia kwa taifa. Inaweza kufaidi utalii na jamii za kusini ya Westland na Fiordland ambazo mapato yao makubwa hutokana na utalii.*

Mhariri wa gazeti la *Otango Daily Times*

Habari kutoka: Shule ya Upili ya Greymouth, New Zealand

# Ujengaji wa barabara kuu kupitia eneo la Urithi wa Ulimwengu



# Kupitia kwa mitaala: Urithi wa Ulimwengu na utalii

## Sanaa

**Panga** kampeini ya utalii ukihusisha mabango ya kuwavutia watalii katika eneo.

**Buni** na ikiwezekana tolesha makaratasi ya habari kuhusu maeneo ya utalii. Chora kwa kalamu au kwa rangi au hata tembelea eneo la utalii. Tayarisha picha zilizochorwa kwenye eneo za uzuri wa kisanaa au michoro ya mapambo kwenye mavazi.

**Chora** bango linaloonyesha haja ya kuhifadhi maeneo ya urithi ya eneo la karibu na la kitaifa; fanya utafiti kuhusu taswira ya eneo hilo, na sababu ya kulibuni na iwapo hali ya utalii imebadilika.

## Jiografia/Historia

**Jadili** iwapo *na kwa* nini (au si kwa nini) eneo fulani limekuwa likiwavutia watalii kwa muda mrefu.

**Jadili** iwapo historia ya eneo hilo inaifanya kuwa na maana kwa utalii wa kijimbo, kitaifa, kijimbo au kiulimwengu.

**Pendekeza** jinsi ya kueleza historia ya eneo hilo kidhahiri kwa watalii.

**Chunguza** mmonyoko kwenye eneo hilo unaosababishwa na wageni na ujadili suluhisho, kama vile njia tofauti za kuelekea hapo.



## Mtandao wa mdahalishi

**Tafiti** kwenye mdahalishi kwa kutumia maneno ya kiini 'World Heritage' na 'tourism' ili upate habari kuhusu urithi wa ulimwengu na utalii katika mataifa mahsusi au majimbo.

## Lugha/Fasihi

**Andika** makaratasi ya habari kwa watalii, umma kwa jumla, wageni, walemavu, wageni kutoka ngambo, watu wachanga, n.k.

**Andika** wito wa kiutangazaji wa eneo.

**Andika** na urekodi ziara za eneo kwenye kinasa sauti.

**Jadili** au igizeni kuhusu thamani ya eneo la urithi na uwezekano wa tisho kutoka kwa utalii. Tafsiri habari kuhusu eneo katika lugha zingine.

**Chunguza** makaratasi ya matangazo kuhusu eneo la kimataifa, na la kitaifa.

**Tafiti** kuhusu eneo lolote ambalo limetajwa kwenye riwaya na hadithi na ujadili jinsi nukuu kutoka kwenye vitabu vya kifasihi zinavyoweza kuhusishwa kwenye brocha na hati au savei.

## Hesabu

**Tumia** grafu, chati yenye kuonyesha vigao au takwimu kujadili mielekeo ya utalii na yanayodokezwa na hali hii kwa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu, hesabu na urekodi matokeo ya hojaji au savei.

## Sayansi ya jamii

**Fanya** savei ya wageni kwa kuwapatia hojaji.

**Wahoji** wasimamizi wa maeneo ili kujifunza kuhusu athari nzuri na mbaya zinazotokana na utalii kwenye maeneo ya urithi.

# Urithi wa




**'Asilia inaweza kufasiriwa kwa njia nyingi—kama msingi wa biashara za kisayansi; kama rasilimali; kitu cha kutazamwa na kufurahiwa; au kama sanaa ya kusisimua.'**

**Rais Nelson Mandela, Oktoba 1994**

# Urithi wa Ulimwengu na Mazingira


| | Ukurasa |
|---|---|
| **Malengo** | **125** |
| Maarifa | 125 |
| Mielekezo | 124 |
| Ujuzi | 125 |
| **Watu wachanga na uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu** | **126** |
| **Harakati za wanfunzi za 29:** Mfumo wa kiikolojia na mandari ya ardhi | 127 |
| **Uhifadhi wa mazingira wa kimataifa** | **127** |
| **Harakati za wanafunzi za 30:** Uharibifu wa mazingira | 131 |
| **Uhifadhi wa bayo-anuwai kupitia kwa uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu** | **132** |
| **Harakati za wanafunzi za 31:** Uharibifu wa anuwai ya kibayolojia | 133 |
| Anuwai ya kitamaduni na ya kibayolojia | 133 |
| Mabadiliko ya spishi na kuangamia kwa spishi | 133 |
| Hifadhi ya *kiasilia* ya *Valee de Mai, Seychelles* | 135 |
| Hifadhi ya wanyama pori ya Manas, India | 136 |
| Te Wahipunamu, New Zealand | 136 |
| **Harakati za wanafunzi za 32:** Mchezo fumbo kuhusu Gondwanaland | 137 |
| *Ukurasa* wa *harakati* za wanafunzi: Mchezo fumbo kuhusu Gondwanaland | 138 |
| **Harakati za wanafunzi za 33:** Kuoanisha maeneo ya kiasilia ya Urithi wa Ulimwengu na vigezo vinavyoambatana na maeneo hayo | *140* |
| **Maendeleo yanayoweza kudhibitiwa ya kiikolojia na ya kitamaduni** | **140** |
| Mbuga ya wanyama ya Banc d'Arguin, Mauritania | 141 |
| **Harakati za wanafunzi za 34:** Kulinda mazingira | 142 |
| **Harakati za wanafunzi za 35:** Harakati zinazoendeleza *udumishaji* wa ikolojia | 142 |
| Wenyeji waunga mkono udumishaji wa mazingira 143 | |
| **Harakati za wanafunzi za 36:** Ziara za maeneo ya urithi 143 | |
| **Hali ya baadaye ya sayari** | **144** |
| **Kupitia *kwa mitaala:* Urithi wa Ulimwengu na mazingira** | **145** |

# Malengo



## Maarifa

**Kuwasaidia wanafunzi kukuza maarifa yao na uelewaji wa:**

- *Mazingira* ya kiasilia na kitamaduni na uhusiano wa watu na mazingira
- Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu kama maeneo yanayolindwa yaliyo muhimu kwa *uhifadhi wa* anuwai ya kibayolojia na spishi za mimea na wanyama zinazokabiliwa na tisho
- *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* kama mchango muhimu kwa hatua za uhifadhi wa pamoja wa mazingira.

## Mielekeo

**Kuwahimiza wanafunzi:**

- Kukuza maadili dhabiti ya uhifadhi na kujitolea kuhifadhi mazingira
- Kuishi maisha yao kwa njia ambayo italinda spishi na anuwai za kibayolojia na kuhakikisha kuwa uwezo wa vizazi vya baadaye wa kujitafutia mahitaji yao hautahatarishwa.



## Ujuzi

**Kuwasaidia wanafunzi kukuza uwezo wao wa:**

- Kushiriki katika ulinzi wa mazingira, hasa ulinzi wa Urithi wa Ulimwengu
- Kushiriki katika hatua za kimaendeleo za kustawi kwa mazingira na kuhakikisha afya ya sayari na watu wake
- Kujitolea kama viongozi wa uhifadhi wa Urithi wa *Ulimwengu*.

# Watu wachanga na uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu

Uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu unaweza kuchangia ulinzi wa mazingira, anuwai ya kiasilia na ya kitamaduni, na uhusiano baina ya watu na mazingira.

Urithi wa Ulimwengu unasaidia kumulika baadhi ya mambo ya kimazingira ambayo watu wanayafikiria, hasa idadi inayoongezeka ya mimea na spishi za wanyama adimu wanatoweka, na kusababisha upungufu wa anuwai ya kibayolojia au bayo-anuwai (bioligical diversity). Uhifadhi wa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu unatekelezwa katika mpango wa kimataifa wa kuhakikisha kuendelea kustawi kwa kolojia, ambapo, kwa mfano, hadhi ya eneo fulani kuwa katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu inasawazishwa na mahitaji ya wenyeji wa eneo hilo ya kutumia rasilmali na kujikimu kiuchumi. Na pamoja na haya *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* yanatambua urithi wa kitamaduni na kiasilia na maingiliano baina ya aina hizi mbili za urithi.

Kwa sababu hii, *Mapatano* yanatoa nafasi ya kipekee ya mtazamo mkamilifu wa uhifadhi wa mazingira unaohusisha ulindaji wa anuwai ya kiasilia na thamani ya kitamaduni ya eneo fulani.

Maeneo 149 ya kiasilia yaliyo kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu ya mwaka 2004, yanalinda spishi za mimea na wanyama, mifumo ya kiikolojia, maeneo ya kijiolojia, taratibu za kiikolojia na kibayolojia na makao ya kiasilia, na vile vile maeneo yanayovutia na ya umuhimu wa kiujumi. Maeneo haya ni karibu asilimia 10 ya dunia (nchi kavu na bahari) ambayo kwa sasa inatunzwa na kusimamiwa kama maeneo yanayolindwa.

Ili watu wachanga washiriki *kikamilifu* katika uhifadhi wa mazingira, wanahitaji kuelewa maswala na hali tatizi zinazokabili harakati hii, na wawe na uwezo wa kutenda ipasavyo. Kujifahimisha umuhimu wa *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* juu ya uhifadhi wa mazingira kunaweza kusaidia kutekeleza jukumu hili. Baadhi ya maswala muhimu katika uhifadhi wa mazingira yamewasilishwa katika sehemu hii ya kifaa hiki.

Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu



Wanafunzi wa shule ya upili ya Greymouth wanazuru mto wa barafu (glacier) huko Te Wahipounamu, kusini-magharibi New Zealand.
© UNESCO



© UNESCO 2004

■ **Harakati za wanafunzi za 29**

## MIFUMO YA KIIKOLOJIA NA MANDHARI YA ARDHI

**Lengo: Kuongeza ufahamu zaidi kuhusu aina tofauti za mifumo ya kiikolojia na maeneo ya kiasilia ya Urithi wa Ulimwengu**



**Mazoezi** | **Harakati darasani** | **Vipindi viwili** | **Jiografia, sayansi** | **Ramani ya Urithi wa Ulimwengu, Maelezo kwa ufupi**

✓Kuna mifano ya aina hii ya mifumo ya kiikolojia au maumbile ya ardhi katika eneo lenu? Je, sifa kuu na sura ya nchi ikoje? (kwa mfano, *kinamasi, maziwa* katika maeneo nyevu) na ni spishi za aina gani za mimea na wanyama zilizopo, kwa mfano, ndege wa majini katika sehemu za mvua nyingi?

✓Waulize wanafunzi kuchunguza Maelezo kwa ufupi na kuchagua na kuainisha maeneo ishirini ya kiasilia ya Urithi wa Ulimwengu *ya aina zifuatazo*:

- misitu
- pwani
- milima

✓Jadilianeni matokeo yaliyopatikana na wanafunzi na uwaulize watambue maeneo katika nchi zao ambayo yanaingia katika kategoria hizi tatu.

✓Waulize wanafunzi watambue mifano kutoka kwa Orodha ya Urithi wa Ulimwengu ya:

- mwamba marijani
- misitu
- visiwa
- jangwa
- maeneo ya mvua nyingi

na mjadiliane matokeo.

# Uhifadhi wa mazingira wa kimataifa

Kwa kuwa tumekabaliwa na uharibifu mkubwa wa mazingira—uchafuzi wa hewa, maji na mchanga, upataji joto wa ulimwengu usio wa kawaida, kuangamizwa kwa safu la 'ozone' na rasilmali za kiasilia zisizoweza kuhuishwa tena, kutoweka kwa *spishi*, na upungufu wa namna mbali mbali za uhai—lazima sote tuchukuwe hatua ya dharura ili kurekebisha uharibifu ambao tayari umefanywa ili kuhifadhi anuwai ya kiasilia na kitamaduni na kuhakikisha maendeleo ambayo yanaweza kudumishwa kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vya baadaye.



Anwani

Uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu, hasa wa maeneo ya kiasilia, unaweza *kuchangia* kuboresha na kulinda mazingira. Pamoja na *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu*, kuna mapatano kadha ya kimataifa kuhusu uhifadhi wa *mazingira*. Habari zaidi kuhusu mikataba hii na ofisi za wahusika zinaweza kupatikana kupitia kwa tovuti (website) ya makao ya **Urithi wa Ulimwengu ya UNESCO** kwenye anwani ifuatayo (http://unesco.org/whc)

*Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* yalitiwa sahihi miezi miwili baada ya kongamano la kwanza la Umoja wa Mataifa juu ya mazingira lililofanyika Stockholm, Uswidi, mnamo Septemba 1972. Miaka ishirini baadaye, viongozi wa ulimwengu walikutana Juni 1992 katika kongomano la Umoja wa Mataifa la Mazingira na Maendeleo huko Rio de Janeiro (Brazil). Mkutano wa Rio de Janeiro (Earth Summit), uliitishwa kukadiria kuchakaa *kulikothiri* kwa mazingira na kufafanua mikakati ya kuiboresha. Mkutano huu mkuu ulipelekea kupitishwa kwa Agenda 21, mapendekezo kadha ya kusaidia kuokoa ulimwengu, ambayo sura yake ya 36 inasisitiza nafasi muhimu ya elimu na watu wachanga.

Pamoja na haya, mataifa 181 na Jumuiya ya *Uropa walitia* sahihi mkataba juu ya anuwai ya kibayolojia, ambayo unasisitiza bidii za pamoja za kuhifadhi aina tofauti za uhai. Mapatano mawili zaidi ya kimataifa pamoja na taarifa juu ya uhifadhi wa misitu yalitokana na mkutano huu mkubwa wa Rio.

*Mapatano ya Mabadiliko ya Hali ya Anga (Convention on Climate Change)* yalianza kutekelezwa mnamo Machi 21, 1994 na yameratibiwa na mataifa 186 kufikia sasa. Yanalenga kudhibiti utoaji wa gesi zinazosababisha joto kwenye anga na kwa hivyo kupambana na shida ya uongezekaji wa joto lililokithiri ulimwenguni.




*Mapatano ya Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Majangwa (Convention on Desertification) katika nchi ambazo zinapatwa na shida ya ukame mkubwa na au ukuaji wa majangwa hasa katika Afrika*, yalianza kazi Desemba 26, 1996. Yanalenga kumaliza tisho la kutaabika kwa binadamu na maafa ya kimazingira kutokana na ukame na ukuaji wa jangwa.

Taarifa isiyo ya kisheria ya mwongozo kuhusu kukabaliana kijumla juu ya usimamizi, uhifadhi na maendeleo yanayoweza kukabilianwa nayo ya aina zote za misitu *(Non-Legally Binding Authoritative Statement of Principles for a General Consensus on the Management, Conservation, and Sustainable Development of all Types of Forests)* pia ilipitishwa katika mkutano wa Rio. Huu mkataba unalenga kuhimiza mataifa yote yafanye bidii kurejesha ulimwengu katika hali ya kimisitu kwa upandaji upya wa misitu na uhifadhi wa rasilmali.

Pamoja na haya, *Mapatano juu ya Biashara ya Kimataifa ya Spishi Zinazohatarishwa za Wanyama na Mimea ya Porini* (CITES) yalikubaliwa 1975. CITES inapanga usimamiaji wa biashara ya kimataifa ya spishi zilizo katika hatari ya kutoweka, CITES inakataza kabisa biashara juu ya spishi hizi za mwituni.

*Mapatano ya Ransar juu ya maeneo nyevu* yenye umuhimu wa kimataifa *(Ramsar Convention on Wetlands)* ni mapatano baina ya serikali kadhaa ambayo yanashirikisha mataifa kuhifadhi na kutumia kwa busara maeneo nyevu na rasilmali zake.



*Mbuga ya kitaifa ya wanyama ya Ichkeul, Tunisia.* *© INCAFO*

© UNESCO 2004

Kwa sasa kuna maeneo nyevu 1,094 yakienea hekta milioni 87, ambayo yamepangiwa kuandikwa katika Orodha ya Ransar ya maeneo nyevu na ya umuhimu wa kimataifa.

Maeneo 25 yaliyoko kwenye Orodha ya Ramsar ya maeneo nyevui yenye umuhimu wa kimataifa pia ni maeneo ya Urithi wa Ulimwengu. Maeneo haya ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Algeria | La Valee d'Iherir (Inayohusishwa na eneo la Urithi wa Ulimwengu la Tassili r'Ajjer | Phillipines | Mbuga ya mwamba wa marijani ya Tubbataha |
| Australia | Mlango mkuu wa Bahari wa Strait (unaohusishwa na eneo la Urithi wa Ulimwengu wa kisiwa cha Fraser)<br>Mbuga ya wanayama ya kitaifa ya Kakadu | Romania | Delata ya Danube |
| Bangladesh | Sundarbans | Shirikisho la Urusi | Delta ya Selenga (Sehemu ya urithi wa ulimwengu ya ziwa Baikal) |
| Bulgaria | Hifadhi ya kiasilia ya Srebarna | Senegal | Hifadhi maalum ya kitaifa ya ndege Djoudj, Senegal |
| Canada | Delta ya Peace -Athabusca, Whooping Crane, Summer Range. (zote mbili ni sehemu ya eneo la Urithi wa ulimwengu la mbuga ya wanyama ya kitaifa ya Wood Buffalo) | Slovenia | Mapango ya Skocjan |
| Costa Rica | Mbuga ya wanyama ya kisiwa cha Cocos, ya | Uhispania | Mbuga ya wanyama ya kitaifa ya Donana |
| Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo | Mbuga ya wanyama ya kitaifa ya Virunga | | |
| Ufaransa | Mont St Michael, na Kisiwa cha Ghuba | | |
| Hungary, Jamhuri ya Slovak | Mapango ya Aggtelek Karst na Slovak Karst | Sweden | Sjaunja (sehemu ya eneo la urithi wa ulimwengu la Laponian) |
| Hungary | Mbuga ya wanyama ya Hortobagy | Tunisia | Mbuga ya wanyama ya Ichkeul |
| India | Mbuga ya wanyama ya Keoladeo | Marekani | Mbuga ya wanyama ya kitaifa ya Everglades |
| Lebanon | Tyre | | |
| Mauritania | Mbuga ya wanyama ya Banc d'Arguin | | |
| Niger | Mbuga ya wanyama ya 'W' | | |



Ziwa Baikal, Shirikisho la Urusi. © UNESCO



Mbuga ya Wanyama ya Kitaifa ya 'W' ya Niger. © UNESCO



Pamoja na haya mpango wa UNESCO wa Man and the Biosphere (MAB) unalenga kumulika mgongano baina ya maswala ya mazingira na maendeleo ambayo yanahusu rasilmali za kiasilia, uchunguzaji wa athari ya harakati za watu juu ya mazingira na jinsi binadamu wanavyokabiliana na matokeo hayo. Mbuga za 'biosphere' husaidia kuhifadhi anuwai za kibayolojia (au bayo-anuwai), kudumisha ikolojia na kutusaidia tujifunze kuhusu matumizi ya kitamaduniya ardhi, kusambaza habari kuhusu usimamizi unaoweza kudumishwa wa rasilmali na ushirikiano katika kukabiliana na shida zinazohusu rasilmali.

Anuwai

© UNESCO 2004

## ▲ Anwani za tovuti za mapatano mengine

### ▶ *Natural heritage*

| | |
|---|---|
| *Mapatano ya Anuwai ya kibayolojia* | *http://www.biodiv.org* |
| *Mapatano ya Biashara ya Kitaifa ya Spishi za Maua na Wanyama Pori Zilizo Hatarini (CITES)* | *http://www.cites.org* |
| *Mapatano ya spishi za kuhamahama* | *http://unep-wcmc.org/cms* |
| *Mapatano ya Ramsar juu ya maeneo yenye mvua nyingi* | *http://www.ramsar.org* |
| *Mfumo wa Mapatano ya Umoja wa Mataifa juu ya mabadiliko ya hali ya anga* | *http://www.unfccc.de* |
| *Mapatano ya Umoja wa mataifa ya kupambana na ueneaji wa majangwa* | *http://unccd.int* |

### ▶ *Urithi tamaduni*

*Ulinzi wa mali-tamaduni wakati wa vita za kisilaha (Mapatano ya Hague):*
*http://www.unesco.org/culture/legalprotection/war/html_eng/index_shtml*

*Uzuiaji wa biashara haramu ya uingizaji, au utumiaji katika mataifa mengine au uhamishaji wa umilki wa mali-tamaduni:*
*http://www.unesco.org/culture/legalprotection/theft/html_eng/index_en.shtml*

*Mapatano ya mda juu ya ulinzi wa urithi wa ulimwengu wa kitamaduni ulio chini ya maji:*
*http://www.unesco.org/culture/legalprotection/water/html_eng/index_en.shtml*

*Mapatano ya Unidroit juu ya vifaa vya kitamaduni vilivyoibiwa au kutumwa kwa mataifa ya nje kwa njia isiyo halali:*
*http://www.unidroit.org/english/conventions/c-cult.htm*

*Mapatano mengine ya urithi wa kitamaduni: http://fletcher.tufts.edu/multi/cultural.html*

### ▶ *Vifaa vya kitamaduni vya Uropa*

Nchi wanachama wa Baraza la Mataifa ya Uropa pia wamebuni makubaliano ya kimataifa ya sheria. Ambayo yanahusu::

*Mapatano ya kitamaduni ya Uropa:*
*http://conventions.coe.int/Treaty/en/Treaties/Html/018.htm*

*Mapatano ya Uropa juu ya ulinzi wa Urithi wa Kiakolojia:*
*http://conventions.coe.int/Treaty/en/Treaties/Html/066.htm*

*Mapatano ya ulinzi wa urithi wa usanifu-mijengo wa Uropa*
*http://conventions.coe.int/Treaty/en/Treaties/Html/121.htm*

*Mapatano ya Uropa ya Ulinzi wa Urithi wa Kiakiolojia: (Revised)*
*http://conventions.coe.int/Treaty/en/Treaties/Html/143.htm*

*Mapatano ya Uropa ya mandhari-nchi:*
*http://www.nature.coe.int/english/main/landscape/conv.htm*

*Orodha kamili ya Mapatano ya Baraza la Uropa yanaweza kupatikana:*
*http://conventions.coe.int/Treaty/EN/CadreListeTraites.htm*



© UNESCO 2004



## ■ Harakati za wanafunzi za 30

### UHARIBIFU WA MAZINGIRA

**Lengo: Kutambua maswala yaliyopo ya kimazingira na yale yanayoweza kutokea katika nchi yako na yanavyohusiana na maeneo ya kiasilia ya Urithi wa Ulimwengu**



**Utafiti** | **Harakati darasani** | **Vipindi vitatu** | **Jiografia, sayansi** | **Ramani ya Urithi wa Ulimwengu, Maelezo kwa ufupi** | **Vitabu vya sayansi, habari fupi zilizotolewa magazetini, makala ya magazeti**

✓Waulize wanafunzi kuorodhesha maswala muhimu ya kimazingira au shida zinazoweza kutokea katika nchi yao au jimbo (kama vile mmomonyoko, mabadiliko ya hali ya anga, maji kupwa sana, uongezekaji wa majangwa, ukataji wa miti zaidi). Waulize iwapo kuna maeneo ya Urithi wa Ulimwengu ya hapo karibu, taifa au eneo kubwa la ulimwengu yanayokabiliwa na shida hizi.

✓Je shida za kimazingira katika nchi yako au eneo la kwenu zinatatuliwa kwa njia gani? Kwa vitendo vya watu wa nchi yako au kwa hatua za kimataifa?

✓Waulize wanafunzi wakusanye makala juu ya maswala ya kimazingira na wachambue matokeo yao darasani.



### Ishara zinazoonyesha uharibifu wa mazingira

▶ Zaidi ya thuluthi mbili za spishi za ndege wa ulimwengu wanapungua, wamo hatarini au wanatishwa na uwezekano wa kutoweka.



▶ Katika miaka mia mbili iliyopita, robo moja ya spishi za ndege wametoweka hasa katika visiwa vilivyo kwenye bahari.



▶ Idadi ya vyura inaelekea kupungua ingawaje si wazi kwa nini jambo hili linatokea.

▶ Miamba ya marijani inaonekana kupungua kwa ukubwa.

© UNESCO 2004

# Uhifadhi wa bayo-anuwai kupitia uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu

Anuwai ya kibayolojia au bayo-anuwai (biological diversity) ni istilahi inayotumika kurejelea aina zote za uhai na pia inahusu mimea aina mbali mbali, wanyama na vijiumbile, jeni zao na mifumo-ikolojia (ecosystems) ambayo wao ni sehemu yake.


Uhifadhi wa bayo-anuwai ya ulimwengu ni jukumu kubwa ambalo linahusisha uhifadhi wa uhai wa dunia. Hii inahusisha uhifadhi wa mazingira ya majini, baharini na vijiumbe.

Uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu ni sehemu muhimu sana ya juhudi za ulimwengu za uhifadhi anuwai ya uhai na inategemea sana hatua za pamoja za kimataifa.

Hifadhi maalum ya wanyama pori ya Okapi iliyo katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo iko katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu kwa kuwa ina mojawapo ya makao muhimu ulimwenguni ya kiasilia ya uhifadhi wa bayo-anuwai, ambayo pia yana spishi ambazo zinakabiliwa na tisho la kuangamia. Hifadhi hii ina spishi zilizo hatarini kama vile mamalia wa hali ya juu, ndege na karibu Okapi 5000 kati ya 30, 000 ambao bado wamebakia ulimwenguni.

*Bustani ya Wanyama ya Okapi, jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. . © IUCN/J. Thorsell*





Uhifadhi wa mfumo wa kiikolojia (ecological conservation) pia ni sehemu muhimu ya uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu kwa mfano, mfumo wa uhifadhi wa mwamba wa marijani wa Belize (Belize Barrier Reef Resere System) ambao uliandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu mnamo mwaka wa 1996, unalinda mfumo wa kiasilia wa maana sana, ambao una 'attols' zilizo kando ya ufuo, mchanga ulio ufuoni, misitu ya mikoko, wangwa na milango ya mito, katika sehemu linanoloenea kwa hektari 93,400. Maeneo mengine makubwa ya Urithi wa Ulimwengu yanalinda mifumo ya kiikolojia ya misitu (kwa mfano Hifadhi maalum ya msitu wa Sinharaja, Sri Lanka) na maeneo nyevu (kwa mfano, Mbuga ya wanyama ya kitaifa ya Doñana iliyoko Uhispania).

Kuangamia kwa bayo-anuwai hasa kwa mifumo ya kiikolojia iliyo hatarani (kwa mfano visiwa na maeneo nyevu) kwa kawaida haiwezi kupinduliwa kwa hivyo kuna sababu za kutosha za kujihusisha na vitisho dhidi ya anuwai na kuchukua hatua mara moja kupunguza vitisho hivi. Pamoja na kulinda spishi mahsusi zinazokabiliwa na tisho ni muhimu zaidi kuhakikisha uhifadhi wa muda mrefu wa mifumo ya kiikolojia, jumuia ya mimea na wanyama na mandhari ya ardhi kwa ujumla.

© UNESCO 2004



## ■ Harakati za wanafunzi za 31

## UHARIBIFU WA ANUWAI YA KIBAYOLOJIA

### Lengo: Kutambua hatari zinazoweza kutisha bayo-anuwai


**Utafiti**


**Harakati darasani**


**Harakati nje ya darasa**


***Vipindi* vinne na ziara za kielimu**


**Sayansi, biolojia**


**Mafungu ya kuandikia, pensili, darubini, kamera**

✓Waulize wanafunzi kueleza mkazo juu ya anuwai ya kibayolojia unaodhihirika katika maeneo yao miongoni mwa haya yaliorodheshwa:

- ubadilishaji wa makaazi (kwa mfano, ufyekakaji miti ili kuanzisha mashamba)
- spishi zilizoletwa katika eneo fulani (ambazo zinaweza kuila mimea asilia na wanyama na kushindania makao na spishi asilia)
- uchafuaji: hewa, maji, mchanga na kelele
- uchimbaji wa migodi
- mengine

✓Waulize wanafunzi kama wanajua kuhusu kupungua kwa idadi ya ndege, wanyama na mimea asilia katika eneo la kwao.

✓Je kuna hatua za kuhifadhi ambazo zinachukuliwa ili kusimamisha upunguaji huu wa bayo-anuwai.

✓Panga na uendeleze ziara ya *kielemu* katika mbuga ya wanyama ya karibu, msitu au hifadhi ya ndege, ili mfanye savei ya bayo-anuwai ya eneo hilo (sensa ya mimea na wanyama). Waalike wazazi kwenye darasa ili wanafunzi wapate nafasi ya kuwasilisha matokeo yao. Waulize wazazi iwapo bayo-anuwai imepungua au kuongezeka sasa ikilinganishwa na wakati walipokuwa wachanga.

13

## ▲ Anuwai ya kitamaduni na ya kibayolojia

Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu ya kitamaduni na kiasilia aghalabu huwa dhihirishoo la anuwai ya kitamaduni na ya kibayolojia.

*Anuwai ya kitamaduni na kibayolojia huhitaji kuhifadhiwa pamoja iwapo moja yao itastawi; maarifa ya watu fulani kuhusu rasilmali na jinsi inavyostahili kusimamiwa ni rasilmali muhimu kwa wanadamu wote.*
Jeffrey A. McNeeley, IUCN, Nature and Resource, Vol 28, No. 3, 1992.

## ▲ Mabadiliko na kuangamia kwa spishi

Mabadiliko ya spishi ni utaratibu unaoendelea pole pole. Spishi mpya zinatokea kupitia kwa mabadiliko ya jeni na kusababisha bayo-anuwai.

© UNESCO 2004

Lengo mojawapo la *uhifadhi* wa Urithi wa Ulimwengu ni kulinda maeneo ya kiasilia ambayo huandaa rekodi ya mabadiliko ya spishi. Kigezo cha *urithi* wa kiasilia (i), kigezo mojawapo kati ya vinne vinavyotumika katika uchaguaji wa maeneo ya kiasilia ili yaingizwe kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu hurejelea:

*Mifano ya kipekee inayowakilisha hatua muhimu za historia ya dunia, pamoja na rekodi ya maisha, mifanyiko muhimu inayoendelea katika ukuaji wa miundo ya ardhi au sura muhimu za ulimwengu.*

Eneo la Urithi wa Ulimwengu la Messel Pit Fossil, Ujerumani ni mfano wa eneo lililoandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu katika misingi ya kigezo cha urithi wa kiasilia (i). Shimo kuu la Messel lina visukuku vingi kutoka enzi ya Eocene baina ya miaka milioni 57 na 36 kabla ya kuzaliwa nabii Kristo. Inatoa habari za kipekee kuhusu hatua za kale za mabadiliko ya mamalia.

Katika *eneo* la Australia la Riversleigh na Naracoorte, hatua za utaratibu wa mabadiliko ya wanyama waliyongamia kitambo (kwa mfano, wanyama waliyoumbwa na mifuko ya kubebea watoto) bado zingali zimehifadhiwa vizuri. Eneo hili liliandikwa kwenye Orodha la Urithi wa Ulimwengu kupitia vigezo (i) na (ii).





*Maeneo ya Australia visikuku vya mamalia (Riversleigh na Naracoorte)*
*© UNESCO*

## Uvumbuaji wa spishi mpya: Msonobari wa Wollemi—kizuka kutoka miaka ya dinosari

*Katika Desemba mwaka wa 1994, spishi mpya ya mti ilivumbuliwa karibu na Sydney, Australia. Msonobari wa Wollemi (Wollemi nobilis) unaokua hadi mita 35. shina lake kuu lina ukubwa wa mzunguko wa mita moja. Uvumbuaji wa spishi ya mti ambao unakua hadi urefu mkubwa kama huo ni jambo nadra sana. Mazingara ya msonobari wa aina ya Wollemi ni korongo huko Sydney lenye ncha kali ambalo lilikuwa kinga ya mioto ya mara kwa mara iliyochoma eneo la karibu. Eneo hili limesaidia uhai wa miti hii. Ugunduzi wa spishi hii mpya ya miti inaonyesha wazi ya kuwa urithi wetu mwingine wa kibayolojia bado haujajulikana.*

State of the Environment, Australia, 1996, Executive Summary, Commonwealth of Australia

© UNESCO 2004

Bayo-anuwai hupotea wakati aina fulani ya mmea au mnyama ambao hawajazoea hali mpya za kimazingira (kama vile mvua au mabadiliko ya hali joto) wanapokuwa hawafanikiwi katika uzaanaji na kuendelea kudumu. Kwa hivyo wanatoweka. Rekodi ya visukuku inaonyesha kuwa mimea na wanyama wengi hatimaye watakuja kutoweka. Hata hivyo siku hizi inafikiriwa kuwa, kwa ujumla utowekaji wa spishi unafanyika kwa haraka kuliko utokeaji wa spishi mpya. Hii inawasilisha hali ya dunia ambayo haiwezi kubadilishwa.

**Kwa sasa,**

- **Asilimia 11 ya ndege waliobakia**
- **Asilimia 11 ya mamalia**
- **Asilimia 5 ya samaki**
- **Asilimia 8 ya spishi za mimea**

→ **zinatishiwa na utowekaji**

- **Idadi ya mamalia impungua sana kutokana na na uwindaji**

- **Uvuaji samaki na nyangumi umesababisha upungufu mkubwa wa idadi ya spishi za majini**

Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu yamestawishwa ili kuhakikisha ulinzi wa spishi za mimea na wanyama wanaokabiliwa na tisho la utowekaji.

13

## ▲ Hifadhi ya kiasilia ya Vallée de Mai, Ushelisheli



*Hifadhi ya Kiasilia ya Vallée de Mai, Ushelisheli. © National Geographic Society/W. Curtsinger*

Hifadhi ya Vallée de Mai iliyo katikati ya kisiwa kidogo cha Praslin, Ushelisheli, iliingizwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu mnamo mwaka wa 1983. Bonde hili linatunza msitu wa minazi ulio karibu katika hali yake ya kiasilia. Hapo ndipo pakuwapo nazi kubwa kabisa ulimwenguni baadhi ni za kilo ishirini. Hapo mbeleni kisiwa chote kilikuwa kimejaa aina mbalimbali za minazi, lakini ukataji uliokithiri umepunguza eneo minazi hii hupatikana, na minazi inapatikana tu katika hilo bonde ndogo. Bonde hili na msitu wake wa minazi unatishwa na spishi za kigeni zinazoletwa kutoka mahali kwingineko pamoja na uvunaji wa nazi, na pia uwashaji mioto.

## ▲ Hifadhi ya wanyama pori ya Manas, India

Hifadhi maalum ya wanyama pori ya Manas nchini India, iiko katika safu ya Mlima Himalaya, ambapo vilima vyenye misitu, vinapungua na mahali pake kuchukuliwa na vilima vyenye nyasi nyingi na misitu ya tropiki ambayo ni makao ya spishi nyingi zilizo hatarini. Eneo hili liliingizwa kwenye Orodha la Urithi wa Ulimwengu katika mwaka wa 1985, na kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu ulio hatarini katika mwaka wa 1992. Manas pia inahusisha makundi ya wanyama *walio hatarini* kama 'tiger', nguruwe-mbilikimo, kifaru na ndovu wa India. Tisho kubwa kwa wanyama hawa ni uwindaji haramu. Kulingana na ripoti ya 1997 vifaru ishirini na wawili wameuawa na walioasilia ni kumi hadi kumi na watano.



Ramani ya Urithi wa ulimwengu

## Te Wahipounamu, New Zealand

Te Wahipounamu iko katika South *Island*, New Zealand. Ni eneo kubwa la ardhi (hektari milioni 2.6 au asilimia 10 ya New Zealand). Te Wahipounamu ni kinamisi nyevu sana chenye milima mirefu ya majabali yenye miteremko inayo-tumbukia baharini. Eneo hili linaonyesha ishara ya mito barafu (glaciers) ambayo ilichonga mabonde na njia za mito na mikono ya bahari na sura ya nchi wakati wa enzi iitwayo Ice Age. Kwa sababu ya kutengwa kijiografia na nchi zingine New Zealand inayo spishi za *kipekee* za ndege, wanyama na mimea. Pia ndege wengi wakawa hawapai na miti na mimea ikazoea mvua ya maeneo hayo kwa njia ya ajabu. Kwa mfano 'giant Kahikatea' (msonobari mweupe) unakuwa hadi mita 30. Misitu kama hii mara nyingi huitwa 'misitu ya disonaria' kwa sababu inaonekana kama ilivyokuwa wakati wa dinosoria miaka milioni 65 iliyopita.

*Wakati masetla* wa Uropa walipofika, kukatokea wanyama wengi na magonjwa yaliyosababisha mimea na wanyama kuwa hatarini na hata wengine *kutoweka*.




Kutengeka kwa eneo hili, mabadiliko ya kijiolojia na hali ya anga imesababisha kuwepo kwa spishi za mimea na wanyama nchini New Zealand ambao hawapatikani mahali popote penginepo. Hata hivyo sababu hizo hizo zilizoyafanya mazingira, mimea na wanyama na New Zealand kuwa *maalum ndiyo* zimesababisha viumbe hivi kukosa usalama. Wapolinesia ambao ndiyo walikuwa wahamiaji wa kwanza New Zealand walifika huko miaka 1000 iliyopita. Walianzisha uharibifu wa kiwango kikubwa wa spishi na makao ya viumbe. Wakati wazungu walifika na kuanzisha ukoloni wa New Zealand nchi hii *ilikuwa tayari im*epoteza asilimia 23 ya misitu yake, na asilimia 30 ya ndege. Hasara kubwa ilimuangukia moa (ndege mkubwa asiyepaa) kutokana na watu wengi zaidi waliofika pamoja na wanyama wauaji. Sasa kuna aina ya mimea na pamoja na wanyama 503 walio hatarini pamoja *na* 43 ambao wanachukuliwa kuwa wametoweka.

Habari kutoka: Greymouth High School, New Zealand.



© UNESCO 2004

## ■ Harakati za wanafunzi za 32



# MCHEZO FUMO KUUSU GONDWANALAND


### Lengo: Kujifunza kuhusu uundaji wa bara na jinsi utengaji unavyoweza kulinda urithi wa kiasilia


Mazoezi


Harakati darasani


Vipindi viwili vya darasani


Jiografia, historia, sayansi


Ramani ya Urithi wa Ulimwengu, kurasa za harakati za wanafunzi, mchezo fumbo wa Gondowanala d


Makasi, gundi, ramani ya ulimwengu

✓Waeleze wanafunzi wako kuhusu Gondwanaland ya kale.

Kwa kuchunguza ushahidi wa miundo ya aina za majabali na visukuku, wanasayansi wanaamini ya kuwa New Zealand zamani ilikuwa sehemu ya bara kubwa Gondwanaland ambayo pia ilihusisha Australia, Afrika, Marekani ya kusini, India, Antarctica, n.k. New Zealand inawezekana kuwa ndiyo kiungo muhimu sana cha Gondwanaland kwa sababu imejitenga tangu wakati ule ilipojitoa kutoka kwa Antarctica na Australia miaka milioni themanini iliyopita. Kwa kuwa imezingirwa na kilomita 1, 600 za maji watu walifika huKo miaka 1000 iliyopita tu. Mimea mwitu ya New Zealand ilistawi bila kusumbuliwa kwa mamiliioni ya miaka. Hata sasa New Zealand bado ndiyo mahali palipojitenga sana duniani.






Ramani ya Urithi wa ulimwengu

✓Wapange wanafunzi katika makundi madogo. Patia kila kikundi nakala ya ukurasa wa harakati za wanafunzi. Waulize wakate vijisehemu kupitia kwenye maeneo yaliyo na nukta nukta, vipange na uvibandike kwenye bara ya Gondwanaland. Jadiliana na wanafunzi jinsi mgawanyiko wa Gondwanaland ulivyoitenga New Zealand kutoka sehemu zingine za ulimwengu na kulinda maua na wanyama wake wa pori.

✓Linganisha Gondwanaland na bara za sasa.


Chanzo cha habari: Greymouth High School, New Zealand

© UNESCO 2004






Mchezo fumbo wa Gondwanaland






Mchezo fumbo wa Gondwanaland



**■ Harakati za wanafunzi za 33**

## KUOANISHA MAENEO YA KIASILIA YA URITHI WA ULIMWENGU NA VIGEZO VINAVYOAMBATANA NA MAENEO HUSIKA

**Lengo: Kuelewa vyema vigezo vinavyotumika katika uchaguzi wa maeneo ya kiasilia ya Urithi wa Ulimwengu**



**Utafiti** | **Harakati darasani** | **Vipindi vitatu** | **Sayansi ya maumbile, sanaa** | **Picha, Ramani ya Urithi wa Ulimwengu , Maelezo kwa ufupi**

✓Chagua maeneo ya kiasilia 25 katika sehemu tofauti za ulimwengu kwa kutumia Maelezo kwa ufupi (wakilisha kurasa husika au uziandike kwa kalamu, na uache sehemu ya vigezo vilivyotumika).

✓ Waweke wanafunzi *katika makundi matano* na upatie kila kundi maelezo ya maeneo tano ambayo yamechaguliwa, watahitajika kuonyesha maeneo hayo yalipo katika ramani ya Urithi wa Ulimwengu. Uliza kila kikundi kuteua mwanafunzi mmoja kuwasilisha mapendekezo yao kwa darasa. Linganisha majibu yao na vigezo ambavyo vilitumika kama Maelezo kwa ufupi yanaeleza.



✓Kwa kutilia maanani vigezo vinne vinavyotumiwa kuchagua maeneo ya Urithi wa Ulimwengu ya *kiasilia waulize wanafunzi* wapendekeze vigezo kwa kila maeneo ya urithi ya karibu ya kitaifa au eneo la mataifa mengi. Na uwaambie waangalie kama maeneo hayo yako kwenye ramani ya Urithi wa Ulimwengu na mjadiliane vilivyo. Wanafunzi watatayarisha mabango yaliyo na wito wa kutetea uhifadhi katika maeneo ya urithi waliyoyapendekeza.

# Maendeleo yanayoweza kudhibitiwa ya kiikolojia na ya kitamaduni

*Maendeleo lazima yaweze kudhibitiwa ili kuhakikisha ya kuwa yanatosheleza mahitaji ya kizazi cha sasa bila kupunguzia uwezo vizazi vijavyo kukabiliana na matatizo yake.*
Environment and *Sustainable* Development, UNESCO, 1997

Haja ya kudumisha usawa baina ya mwanadamu na mazingira ni hali inayomulikwa na *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu*. Maelezo ya Urithi wa Ulimwengu yanayochukuliwa kama ya kiutamaduni na kiasilia, hukumbusha jumuiya ya kimataifa muingiliano baina ya watu na mazingira ya *kiasilia* ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo na ikolojia yanayoweza kudhibitiwa .

Katika taratibu za maendeleo nafasiitngew lazima itengwe ambayo, kwa hakika, huridhisha kiroho na kwa njia tendaji sana ndiyo msingi wa maisha yetu.
Jeffrey A. McNeeley, IUCN, Nature and Resources, Vol no. 28, No 3, 1992.

UNESCO 2004

Vitisho vingi dhidi ya mazingira (kama vile ukataji wa miti kwa sababu ya ukulima, uvuvi, uchafuaji wa mazingira) vinavyosababishwa na maendeleo ya sasa, na uongezekaji wa watu *lazima* usimamiwe ili kuhifadhi anuwai ya ulimwengu ya kibayalojia na kitamaduni. Uhifadhi na matumizi ya rasilmali (kwa mfano ya kizaraa, uchimbaji migodi, misitu) huchukuliwa kama kwamba hazihusiani. Kwa sababu hii utumizi wa rasilmali hukatazwa katika maeneo ambayo ni ya Urithi wa Ulimwengu. Hata hivyo katika maeneo fulani yaliyo na usimamizi mzuri njia bora zaidi ni kusawazisha uhifadhi wa urithi wa kiasilia na kitamaduni na usimamiaji wa matumizi ambao unahusika na nafasi ya utumiaji au shughuli zingine za kiuchumi ili watu wa eneo hilo wawe na hamu wenyewe ya kuchangia juhudi za uhifadhi.

## ▲ Mbuga ya wanyama ya Banc d'Argun, Mauritania

Mbuga hii iliyo sehemu ya magharibi ya Afrika ni makao ya mamilioni wa ndege, ina mandhari yanayohusisha matuta ya mchanga, vinamasi vya pwani, visiwa vidogo, maji ya *kina* kifupi yanayosababisha mandhari ya nchi na bahari ya kuvutia na sifa zikiwemo za kibayolojia. Mbuga hii ni mwenyeji wa ndege wanaohamahama na spishi kadha za kasa (turtle) na pomboo (dolphin).


Banc d'Arguin ina umuhimu mkubwa wa kiuchumi kwa eneo hilo: vijiji saba vya biashara ya uvuvi vinategemea utajiri wake mkubwa wa rasilmali za kiasilia na inatoa msingi wa utalii unaozingatia hali ya ikolojia. Mbinu za uvuvi za kienyeji zinazotumiwa na wenyeji hazikusababisha athari mbaya kwa rasilmali za mbuga. Hata hivyo motoboti zikitumika na uvuvi uendelezwe sana inawezekana maisha ya ndege wa pale yaathiriwe vibaya.



*Mbuga ya wanyama ya Banc d'Arguin, Mauritania.*
© UNESCO/IUCN/J. Thorsell



© UNESCO 2004



## ■ Harakati za wanafunzi za 34

## ULINZI WA MAZINGIRA

### Lengo: Kuelewa umuhimu wa usimamizi mzuri wa maeneo ya kiasilia ya Urithi wa Ulimwengu



**Uigizaji** | **Harakari darasani** | **Vipindi kadhaa** | **Lugha, jiografia, sayansi, biolojia** | **Ramani ya Urithi wa Ulimwengu, Maelezo kwa ufupi**

✓Waelezee wanafunzi wako hali katika Mbuga ya wanyama ya Banc d'Arguin Mauritania, upange uigizaji wa kubuni katika *eneo la Urithi wa* Ulimwengu. Wapange wanafunzi katika makundi yanayotetea maslahi tofauti.

✓*Kundi la wafanyi biashara* wanataka kuendeleza biashara ya uvuvi na tayari wamepata wawekezaji wa kigeni wa kugharamia mradi wao. Hata hivyo msimamizi wa mbuga ya wanyama na wanamazingira wa eneo hilo wanahofia kuwa uvuvi ukiendelezwa sana utahitilafiana na maisha ya ndege wa hapo. Serikali ingependelea kuongezea mapato ya *wakaazi wa eneo hilo* lakini hawataki kutatiza hali ya kiikolojia ambayo imesawazika vyema. Je ni maamuzi gani yatakayochukuliwa ya kuwaridisha wote?





## ■ Harakati ya wanafunzi za 35

## HARAKATI ZINAZOENDELEZA UDUMISHAJI WA KIIKOLOJIA

### Lengo: Kuwahimiza wanafunzi kuwazia maswala yanayohusu taka



**Mazoezi** | **Harakati darasani na nje ya darasa** | **Vipindi vichache** | **Vyombo vya kuwekea vitu ambavyo vinaweza kujengwa upya kama** | **mikebe ya alumini na bati, katoni za maziwa, n.k.**

✓Uchafuzi hutokana na kutumia kitu kupindukia au utumizi mbaya. Matumizi ya kipimo razini ya rasilmali kwa njia ambayo *inaweza kudhibitiwa*, pamoja na kutumia upya (recycling) unaweza kuwa suluhisho. Tunastahili sote kufikiria jinsi tunavyoweza kuchangia utumiaji upya na matumizi ya hali ya juu ya rasilmali. Mwalike mwanamazingira darasani kuzungumzia umuhimu wa utumiaji upya na jinsi ya kuutekeleza. Waulize wanafunzi kutayarisha *kampeini ya utumiaji* upya (kwa mafano makaratasi, alumini na mikebe ya bati, chupa) kwa shule na jamii (na pamoja na wanafunzi na wazazi). Amua ni bidhaa zipi zitakusanywa kwa utumiaji mpya. Husisha darasa la sanaa katika utayarishi wa mabango ya kampeini. Chunguza pamoja na wanafunzi matokeo ya *kampeini ya utumiaji* upya.

✓Jadili uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu na udhibiti wake. Je, kuna umuhimu kutumia upya rasilmali na kuitumia tena badala ya kuifuja?


✓Washauri wanafunzi wahusike katika kazi ya kuweka mazingira yao na *maeneo* ya urithi katika hali ya usafi kwa kukusanya taka na kuichoma, kuiondoa au kwa kuijenga upya kwa busara.

UNESCO 2004

## ▲ Wenyeji waunga mikono uhifadhi wa mazingira

Uungaji mkono wa shughuli za uhifadhi unaweza kuongezeka iwapo watu wanaweza kutumia maeneo yanayolindwa kama vile maeneo ya Urithi wa Ulimwengu kwa njia inayoweza kudhibitiwa. Miradi ya uhifadhi na maendeleo inaendelea kuunganishwa na kuungwa mikono katika maeneo yanayolindwa au karibu na maeneo hayo.

Kushirikishwa kwa watu wa eneo fulani katika upangaji wa shughuli za uhifadhi na usimamizi wake ni muhimu iwapo maeneo haya yatatumika kwa njia inayoweza kudhibitiwa.



## ■ Harakati za wanafunzi za 36

## ZIARA ZA MAENEO YA URITHI

### Lengo: Kuwapatia wanafunzi nafasi ya kuwa na ujasiri, ubunifu na kuwa macho kuhusu mazingira yao



**Mazoezi** | **Harakati darasani** | **Harakati za nje ya darasa** | **Vipindi kadhaa vya darasani na muda baada ya darasa** | **Masomo ya jamii, sayansi, biolojia** | **Ramani**

✓Wanafunzi hufurahia harakati za kijasiri na uvumbuzi. Kwa hivyo pendekeza wapange safari maalum ya eneo la urithi. Fikirieni pamoja itakuwa safari ya aina gani, kama vile ya kuelekea kwenye urithi wa kiasilia, kuelekea kwenye urithi wa kitamaduni, kuelekea kwenye urithi wa kimiji, ya kuelekea kwenye urithi wa maua, ya kuelekea kwenye urithi wa picha au video. Baada ya kuamua kuhusu maudhui ya ziara yenu ya eneo la urithi leta ramani kadhaa darasani ili mzitazame pamoja. Waulize wanafunzi wapange safari yao na wachunguze baadhi ya maeneo muhimu kwenye ramani wakipata fursa. Baada ya safari kupangwa waulize wanafunzi kutayarisha kijitabu kuihusu ili maeneo muhimu yamulikwe.

*Ziara kufika eneo la urithi Head-Smashed-In-Buffalo Jump complex, Canada. 142¡142© S. Titchen*



✓Panga siku maalum ya ziara hiyo. Tumia ziara hii kuwahimiza wanafunzi watumie hisia zao (kunusa, kusikiza, kutazama)

✓Kutokana na matokeo na athari ya ziara hii kwa wanafunzi, fikiria kuhusu ziara nyingine ambayo wanafunzi wanaweza kuwakaribisha wengine kuungana nao (madarasa mengine katika shule yao au kutoka shule zingine katika jamii hiyo, wazazi na wanajamii).



© UNESCO 2004

## Hali ya baadaye ya sayari yetu


Tangu mkutano wa Rio wa 1992 (Earth Summit) jumla ya maeneo 333 ya kiasilia, kitamaduni na yanayo husisha sifa hizi mbili za kitamaduni asilia, yamesha andkishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Maeneo 58 kati ya haya ni ya kiasilia (kufikia Desemba mwaka wa 2000).

*Katika mataifa yalito stawi bila shaka kumekuwa na mabadiliko katika matumizi ya rasilmali—matumizi bora ya kawi, ardhi, maji... Uchafuzi wa hewa, maji na udongo umepungua. Hata hivyo katika mataifa yanayoendelea, uchafuzi unaendelea kuongezeka. Jambo la maana ni kuwa mataifa haya yameanza kujionea kuwa hali hii hii imezorata mno na ni vigumu kutenganisha maendeleo ya kiuchumi na kuamu kwa upande mmoja na ulindaji wa mazingira.*
UNESCO Sources no 92, July –August 1997

Mawazo haya yamechangia kwa wingi katika uhifadhi wa mazingira ya ulimwengu.

## Rasilmali zilizoandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu

### Habari kufikia Desemba 2001





Habari kutoka Makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu, Paris 2001

Kwa kuwa maeneo ya *Urithi wa* Ulimwengu yanatambuliwa kuwa yenye thamani ya kiulimwengu ha hali ya juu, yanastahili kuwa mifano ya usimamizi bora.
Bernd von Droste, Mkurugenzi, Makay makuu ya *UNESCO ya Urithi* wa Ulimwengu, Paris, na
Jeffrey A. McNeely, IUCN, World Heritage, Twenty Years Later, IUCN, 1992



UNESCO 2004



# Kupitia kwa mitaala Urithi wa Ulimwengu na mazingira

### Sanaa
Chagua eneo la Urithi wa Ulimwengu la kiasilia linalopendelewa na wanfunzi na uwaambie *walichore*.

### Bayolojia
Chagua eneo la Urithi wa Ulimwengu la kiasilia katika jimbo la kwenu na utayarishe orodha ya mimea, miti, wanyama, n.k.
Linganisha orodha hii na orodha ya mimea, miti na wanyama katika mtaa wenu.
Tekeleza uchunguzi katika mtaa wenu wa mimea, wanyama na sifa za kijiolojia.

### Lugha ya kigeni
Anzisha uhusiano na shule moja iliyo ng'ambo (ikiwezekana kupitia kwa mradi wa ASPnet) na mbadilishane mawazo kuhusu maswala ya kimazingira yanayo wahusu nyote na athari kwenye juhudi za uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu.

### Historia
Chagua eneo la kiasilia na uwaulize wanafunzi kufikiria kuhusu miundo *ya kale ya* ardhi ya eneo hilo na vile ilivyo hivi sasa, na tisho la siku za baadaye za uhifadhi wake.

### Jiografia
Chagua eneo la kiasilia, kama vile moja lenye mito barafu (tazama Los Glaciares, Argentina, Maelezo kwa ufupi) na mjadiliane *kuhusu uongezekanaji* wa joto ulimwenguni na adhara zake.

### Lugha
Chagua eneo la Urithi wa Ulimwengu ambalo wanafunzi wanafikiria kuwa tayari limeshakabiliwa au linatishwa kukabiliwa na uchafuzi na watayarishe kampeni ya kuzuia au kuangamiza *uchafuzi na* kuanzisha au kutilia nguvu hatua za uhifadhi.

### Hesabu
Tekeleza savei ya spishi kadhaa (mimea, miti, wanyama, ndege, samaki) ambazo idadi yao imepungua au ziko karibu kuangamia katika eneo mnakoishi na na uhesabu asilimia ya spishi hizi.

### Sayansi
Chukua sampuli za maji kutoka maziwa au mito ya karibu na uchunguze hali ya uchafuzi ya maji haya.



© UNESCO 2004



**‘Kwa kuwa vita huanzia katika mawazo ya watu, ni katika mawazo yao ambamo ulindaji wa amani unaweza kujengwa.’**

**Dibaji ya katiba ya UNESCO**

# Urithi wa Ulimwengu na amani


Ukurasa

**Malengo** **149**

Maarifa 149
Mielekeo 149
Ujuzi 149

**Urithi wa Ulimwengu na amani** **150**

**Harakati za wanafunzi za 37:** Kueleza maana ya amani na Urithi wa Ulimwengu 151

**Maeneo ambayo ni ishara ya amani** **151**

***Harakati za wanafunzi* za 38:** Urithi wa Ulimwengu na amani katika eneo lenu 154

**Ulinzi wa Urithi wa Ulimwengu wakati wa vita** **154**


**Harakati za wanafunzi za 39:** Kujenga upya urithi ulioharibiwa na vita 155
*Mapatano ya Hague* yanalinda urithi wa *kitamaduni* 155
**Harakati za wanafunzi za 40:** Ulinzi wa Urithi wa kitamaduni na kiasilia wakati wa vita 157
Ulinzi wa urithi wa kiasilia wakati wa vita 157

***Urithi* wa *Ulimwengu na haki* za binadamu** **158**

**Harakati za wanafunzi za 41:** Ubaguzi—tisho kwa amani 159
**Harakati za wanafunzi za 42:** Buni mchezo-fumbo wa maeneo kuhusu *Urithi* wa Ulimwengu na amani 160
***Ukurasa* wa *harakati* za wanafunzi:** Buni mchezo-fumbo wa maneno kuhusu Urithi wa Ulimwengu na amani 161

**Kupitia kwa mitaala: Urithi wa Ulimwengu na amani** **162**

# Lengo



## Maarifa

Kuwasaidia wanafunzi kukuza maarifa na ufahamu kuhusu :

- Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu kama ushahidi wa amani, haki za binadamu na demokrasia
- Ujumbe wa kiadili wa UNESCO na *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu*
- Umuhimu wa kutobaguana katika misingi ya mataifa, uvumilivu na heshima kwa watu wote na utamaduni

## Mielekezo

Kuwapatia wanafunzi moyo kuhusu:

- Kuwaheshimu watu na utamaduni wao na kuwapatia moyo
- Kutafuta mbinu za amani za kutatua migogoro katika maisha yao.
- Kushirikiana katika moyo wa umoja katika kuunga mkono uhifadhi wa urithi.



## Ujuzi

Kuwasaidia wanafunzi kukuza uwezo wao wa:

- Kufanay kazi kwa vikundi
- Kutatua mizozo kwa amani baina yao na kuwasaidia wengine kujifunza kuhusu utatuzi wa mizozo kwa amani
- Kushiriki kidemokrasia kwa mambo ya kisiasa na kiraia
- Kuchangia juhudi za UNESCO za uifadhi wa Urithi wa Ulimwengu

# Urithi wa Ulimwengu na utamaduni wa amani

Amani huhitaji mahusiano yasiyo ya kivita sio tu baina ya nchi lakini pia baina ya watu, baina ya makundi ya kijamii, baina ya nchi na watu wake na baina ya watu na *mazingira* yao. Kujifunza kuhusu maeneo ya kitamaduni na kiasilia yaliyoandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu, hutusaidia kuelewa sura nyingi za amani kwa kutukumbusha maumbile ya ajabu ya kiasilia na ya binadamu, mengi ambayo yanamulika hamu yetu ya kupata uhuru, haki, kuelewana na heshima, upendo na urafiki. Haya yanahusisha haki zetu za kibinadamu za kimsingi na ni vipengele muhimu ambavyo haviwezi kupuuzwa, vya amani na maendeleo kwa kila mtu binafsi, jamii na dunia kwa jumla.

**Amani**

1.(a) Amani kutoka au kusitishwa kwa vita, uadui; hali ya nchi au jamii ambapo haiko vitani na nyingine.
(b) Kuidhinishwa kwa mkataba wa amani baina ya mataifa mawili ambayo yalikuwa vitani.
2. Uhuru usio na ghasia ya raia au vurugu, na usalama wa raia.
3. Uhuru usio wa kusumbuliwa au kutiwa wasiwasi.

*Shorter Oxford Dictionary*

*Mapatano kuhusu ulinzi wa Urithi wa Kitamaduni wa kiasilia* na *Hazina ya Urithi* hutegemea vitendo vya pamoja vya kimataifa vya kulinda sehemu za ulimwengu zenye umuhimu sana.




Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu

*Kutofahamu desturi na maisha ya watu wengine kumekuwa sababu katika historia ya watu kuwashuku wengine na kutoaminiana katika ulimwengu na tofauti hizi mara nyingi zimesababisha vita kutokea;*

*Yamkini vita vikubwa na vibaya ambavyo sasa vimekwisha viliwezekana kwa sababu ya watu kukaidi kanuni za kidemokrasia, kanuni za heshima, usawa na kuheshimiana kwa watu na badala yake uenezaji wa mafundisho ya kutotoshana kwa watu na mataifa, yaliyotokana na kutofahamu na chuki;*

...

*Ya kuwa uenezaji mkubwa wa utamaduni, na uelimishaji wa binadamu juu ya haki na uhuru na amani hayawezi kupuuzwa iwapo heshima ya binadamu itazingatiwa na yanahusu jukumu tukufu ambayo mataifa yote lazima yatekeleze katika moyo wa kusaidiana na kujaliana hali na kwa hivyo amani (iwapo haitakosekana) lazima itategemea msingi wa akili na umoja wa binadamu.*

Dibaji ya Katiba ya UNESCO

*Mwendo wa utamaduni wa amani, kama mto mkubwa, hujazwa na vijito tofauti – kutoka kila desturi, lugha, dini na mielekeo ya kisiasa. Lengo lake ni dunia ambayo tamaduni tofauti, zinaishi pamoja katika mazingira yaliyo na uelewano wa kitamaduni kuvumiliana na umoja.*

Rene C. Romero, Mratibu wa Kitaifa wa ASPnet, Tume ya Kitaifa ya UNESCO, Ufilipino.


© UNESCO 2004



## ■ Harakati za wanafunzi za 37

### KUELEZA MAANA YA AMANI NA URITHI WA ULIMWENGU

### Lengo: Kuelewa vyema *uhusiano* baina ya amani na urithi



| Majadiliano | Harakati darasani | Kipindi kimoja | Historia, masomo juu ya utawala, lugha | Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu, Ramani ya urithi wa ulimwengu, Maelezo kwa ufupi | Kamusi |
|---|---|---|---|---|---|

✓Andika neno 'amani' ubaoni(au taja tu jina lenyewe) na uwaulize wanafunzi kuorodhesha istilahi ambazo wanazihusisha na neno amani. Mwalike kila mwanafunzi kusoma orodha *yake. Wakati wan*apozisoma andika kila istilahi mpya ubaoni, na uweke alama juu ya maneno yanayorudiwa. Ukifika mwisho wa harakati hii utatambua istilahi ambazo zinahusishwa sana na neno amani.

✓*Rudia mazoezi* haya na neno 'Urithi wa Ulimwengu' kwa kuanza kuwauliza wanafunzi kutazama Ramani ya Urithi wa Ulimwengu na kuchagua maeneo ambayo majina yake yana maneno yanayohusishwa na amani, upatanifu, utulivu; au na ulinzi na vita (k.m. kumbukumbu ya amani, ngome, majengo yaliyoimarishwa, kuta). Kisha uwaulize wachague moja (au kadhaa) ya maeneo yanayohusiana na amani ambayo yameelezwa *katika sehemu hii na* watafute habari zaidi kuhusu eneo hilo (kwa mfano kwenye ensaiklopidia ya maktaba ya shule kwa mfano au kwenye mtandao) na nafasi yake katika historia ya amani.

# Maeneo yanayoashiria amani

Maeneo mengi ya Urithi wa Ulimwengu humulika thamani ya kimsingi ya amani na haki za kibinadamu, na ushirikiano wa kimataifa mara nyingi huhakikisha yanahifadhiwa. Mengi hujumuisha mawazo *dhabiti kuhusu* amani. Mto barafu wa Bustani ya Amani ya Kimataifa ya Waterton (tazama picha), iliyoko kwenye mpaka baina ya Canada na Marekani, ina jina amani lililotajwa bayana kwenye anwani yake. Iliandikishwa kwenye Orodha ya *Urithi wa Ulimwengu* mwaka wa 1995. Eneo Waterton Lakes National Park iliyo Alberton (Canada) na Glacier National Park huko Montana (Marekani). Pamoja zinaunda bustani ya kwanza ya kimataifa , ambayo ina spishi nyingi za mimea na mamalia pamoja na miundo mandhari ya kimlima na ya mito barafu.

Waterton Glacier International Peace Park. Canada na Marekani. © *UNESCO*





© UNESCO 2004

Kumbukumbu ya Amani ya Hiroshima (Genbaku Dome) iliyoandikishwa kwenye orodha ya urithi mwaka 1996 kwa upande mwingine ni ishara dhabiti na bayana ya mambo yaliyotekelezwa na amani ya ulimwengu kwa zaidi ya karne moja kufuatia matumizi ya nguvu za kupindukia ambazo zimewahi kubuniwa na mwanadamu.

*Kitu cha maana sana cha Kuba hili ni kile ambacho inawasilisha mabaki yake kwa upande mmoja yanaashiria uharibifu wa hali ya juu ya mwanadamu na kwa upande mwingine yanawasilisha ujumbe wa matumaini ya kuendelea kuwepo kwa muda mrefu kwa amani ya ulimwengu kote ambayo ilianzishwa na ulipukaji wa bomu ya atomu, 1945. Wakati bomu ya kwanza ya atomu lilipolipuka juu ya Hiroshima mnamo Agosti 6 1945 na kusababisha vifo vya watu 140,000, jumba hili ndilo liloachwa limesimama karibu na eneo la katikati la mlipuko kama gofu. Liliachwa hivyo wakati ujenzi mpya wa mji ulipoanza na kujulikana kama Kuba la Genbaku (Kuba la Bomu ya Atomi). Katika mwaka wa 1991, Baraza la mji wa Hiroshima likapitisha maazimio ya kuwa kuba hilo lihifadhiwa daima. Mbuga ya kumbukumbu ya amani ambapo kuba hili ndilo alama kuu yaardhi hiyo, ilijengwa baina ya 1950 na 1964. Tangu 1952 Bustani hii imekuwa eneo la sherehe ya kumbukumbu ya Amani ya Hiroshima inayofanywa kila mwaka tarehe 6 Agosti.*

Baraza la Kimataifa la Majengo na maeneo ya kumbukumbu ya Urithi (ICOMOS)





*Kumbukumbu la Amani la Hiroshima (Kuba la Genbaku), Japan, ishara muhimu inayopendelea amani.*
*© UNESCO*

Vita vilivyofuatia mgawanyiko wa Yugoslavia ya awali vilisisitiza mji wa kale wa Dubrovnik Kroatia kama ishara ya uhuru na amani. Mji huu wa kupendeza uliyo katika pwani ya Dalmatia unaojulikana kama Lulu ya Adriatic (Pearl of the Adriatic), umekuwa *na neno* 'Libertas' (uhuru) limeandikwa kwenye bendera yake kwa miaka mingi. Mji huu ulijulikana sana katika eneo la Mediterranean, ulikuwa na meli nyingi za vita na ofisi nyingi za kibalozi na vituo vya biashara kote katika bara la Uropa. Ingawaje uliharibiwa vibaya na tetemeko la ardhi mnamo 1667, Dubrovnik iliwahi kuhifadhi, makanisa yake ya miundo ya Gothic, Renaissace na Baroque, nyumba za watawa, makasri na chemichemi, pamoja na ukuta wa mawe wa kupendeza ambao unazingira karibu mji wote wa kale. Ukuta huu ambao kwa karne nyingi ulilinda mji huu kutokana na mashambulizi ya baharini haukuwahi kuulinda mji kutokana na bomu za kisasa za miaka michache iliyopita. Uliandikishwa katika mwaka wa 1991 kwenye orodha ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu yaliyo hatarini, Dubrovnik iliweza kukarabati nyumba ambazo zilikuwa zimebomolewa kwa msaada wa UNESCO, na umekuwa ishara ya umoja wa kimataifa na kuendelea kuwa ishara ya uhuru na amani.

Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu

© UNESCO 2004

*Mji wa kale wa Dubrovnik, Croatia.*
©UNESCO/IUCN/
J. Thorsell





*Uangamizaji wa Dubrovnik mnamo mwaka wa 1991.*
*© UNESCO/D. Lefèvre*



© UNESCO 2004



## ■ Harakati za wanafunzi za 38

### URITHI WA ULIMWENGU WA AMANI KATIKA JIMBO WAKO

### Lengo: *Kufikiria* kuhusu maeneo ya urithi yanayoashiria amani



| Utafiti | Harakati darasani na nje ya darasa | Kipindi kimojas | Historia, jiografia, sanaa | Ramani ya Urithi wa Ulimwengu, Maelezo kwa ufupi | Vitabu vya historia ya kitaifa |
|---|---|---|---|---|---|

✓ Waulize wanafunzi watambue maeneo ya kitamaduni na kiasilia (ikiwezekana maeneo ya Urithi wa Ulimwengu) ambapo mikataba ya amani imepigwa sahihi au ambayo *ina thamani* ya kitaashara kuhusu matukio ya kihistoria (kwa mfano, vita vikubwa maamuzi muhimu)

✓ Waulize walete darasani habari yoyote watakayoweza kuipata kuhusu maeneo haya na kisha uwaulize kwa njia ya ubunifu (maandishi, *uchoraji*, uchoraji kwa rangi) kile ambacho wanaamini ni ujumbe wa eneo mojawapo lolote.

# Kulinda maeneo ya urithi wakati wa vita





Urithi wa Ulimwengu na Kitambulishi

Katika vita vyovyote vikubwa maeneo ya kitamaduni na ya kiasilia yanaweza kuathiriwa. Mara nyingine maeneo mahsusi ya kitamaduni huharibiwa makusudi ili kuharibu ishara inayo*thaminiwa ya kitambulisho* cha watu. Maeneo ya kiasilia (hasa wanyama na mimea yake) yanaweza kutishwa kwa njia nyingi – mabomu, magari ya majeshi kupitia katika mbuga za wanyama zinazolindwa, moto, *uwindaji* haramu, kuhamisha watu kwa wingi kutoka kwenye makao yao. Maeneo ya kitamaduni na kiasilia ambayo huleta pato kutoka kwa ut*alii* yanaendelea kuwa lengo la uharibifu wa kimaksudi wakati wa vita.



Urithi wa Ulimwengu na utalii

Katika mateso yanayosababishwa na vita, *ulinzi wa maeneo* ya kitamaduni na kiasilia unaweza kuonekana kama uharibifu wa pesa. Ingawaje inaweza kuonekana hivi mtu akitazama mambo kijuujuu, tajriba imeonyesha uokoaji wa urithi wetu *wa kitamaduni na* kiasilia ni muhimu sana, hasa wakati maeneo yaliyoshambuliwa yanahusu majengo kama maktaba za kitaifa, makanisa, makavazi, vyuo vikuu na madaraja ambayo ni ya tangu karne za kale.



Urithi wa Ulimwengu na kitambulishi

Mfano mmoja wa kusisimua ni ujenzi mpya huko Poland wa Makao ya *Kihistoria* ya Warsaw (Historic Centre of Warsaw) ya karne ya kumi na nane , ambayo yaliandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu mnamo 1980. Katika Agosti 1944, wakati wa vita vya *pili vya ulimwengu* asilimia 85 ya katikati ya mji uliharibiwa na makundi ya majeshi ya Nazi yaliyokuwa yameshikilia nchi hii. Baada ya vita, kampeini ya miaka mitano ya raia ilisababisha ukarabati upya kwa *makanisa, makasr na* soko. Ni mfano wa kipekee wa ujenzi mpya mkamilifu wa

© UNESCO 2004

kipindi cha historia cha karne ya kumi na tatu hadi ya ishirini, na inaeleza fahari na kitambulishi.

Wito wa watu wachanga la Dubrovnik unaomba:

*Juhudi zaidi na vitendo vya kutatua shida kwa amani, kwa kuwa vita huharibu urithi wetu.*



■ **Harakati za wanafunzi za 39**

## KUJENGA UPYA URITHI ULIOANGAMIZWA NA VITA

### Lengo: Kujifunza kuhusu ujenzi mpya wa Urithi wa Ulimwengu



| Utafiti | Harakati darasani | Harakati nje ya darasa | Kipindi kimoja | Historia | Vitabu vya historia ya eneo la karibu, fasihi ya eneo la karibu, mahojiano |
|---|---|---|---|---|---|

✓Waulize wanafunzi kuwahoji mababu zao, watu wa jamii yao, wazee katika ujirani wao kuhusu mambo yafuatayo:

- Iwapo waliathiriwa au wanajua kuhusu vita au mzozo wa kutumia zana, maishani mwao, je wanakumbuka, taasisi za kitamaduni, majengo au maeneo ya urithi ambayo yalibomolewa au kuangamizwa wakati wa vita?
- Je, imefanyiwa ukarabati? Je wanaonaje kuhusu ujenzi huo? Je ujenzi huo unahusu eneo lolote la Urithi wa Ulimwengu?

✓Waulize wanafunzi waandike kwa muhtasari mahojiano yao na wayatumie kwa mjadala darasani.s.

## ▲ *Mapatano ya Hague* yalinda Urithi wa kitamaduni



Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu

Baada ya kujionea uharibifu mkubwa wa urithi wetu wa kitamaduni wakati wa vita vya pili vya dunia vya 1945, Jumuiya ya kimataifa, ikakubali huko Hague (Netherlands), *Mapatano ya Kulinda Mali-tamaduni Wakati wa Mzozo wa Kisilaha*. *Mapatano ya Hague* yana sehemu za ulindaji wa rasilimali inayoweza kusogezeka na isiyoweza kusogezeka ambayo ni muhimu kwa urithi wa kitamaduni wa watu, na bila kujali asili yake au umilki wake, hufanya heshima ya rasilimali hii jukumu la wote.



© UNESCO 2004

## ■ Harakati za wanafunzi za 40

## ULINZI WA URITHI WA KITAMADUNI NA KIASILIA WAKATI WA VITA

### Lengo: kujifunza kuhusu *Mapatano ya Hague* na haja ya kulinda mazingira ya kiasilia wakati wa vita



Utafiti | Harakati za darasani | Kipindi kimoja cha darasani | Historia na masomo ya utawala | Mapatano ya Hague ya 1954



Anwani

✓Jadilianeni na wanafunzi dibaji ya *Mapatano ya Hague ya 1954* na mjaribu kupata nakala ya mapatano yote kutoka tume ya kitaifa ya UNESCO ya nchi yenu au kutoka kwa UNESCO. Jadiliana na wanafunzi wako:

- Muktadha wa kihistoria (baada ya vita vya pili vya ulimwengu) ambapo *Mapatano ya Hague* yalipoandikwa.
- Malengo ya *Mapatano ya Hague* au ya ulinzi wa urithi kwa jumla wakati wa vita.
- Ni kwa njia gani *Mapatano ya Hague* na ya Urithi wa Ulimwengu yanavyotofautiana na ni kwa njia gani yanajengana.
- Mifano ya vita au mizozo ya kisilaha ya hivi majuzi ambapo *Mapatano ya Hague* yalitumika.
- Je vita huharibu kwa njia gani mazingira ya kiasilia?

✓Jadilianeni jinsi vita huharibu mazingira ya kiasilia



## ▲ Ulinzi wa urithi wa kiasilia wakati wa vita

Uharibifu wa baadhi ya mifumo muhimu ya kiekolojia duniani kwa sababu ya vita vya hivi majuzi imedhihirisha ugumu wa kulinda urithi wa kiasilia katika hali kama hizo (kwa mfano upitaji wa magari ya jeshi, utumiaji wa moto ili kuondoa miti kwenye ardhi, mkazo juu ya ardhi kwa sababu ya watu wengi waliohamishwa makwao). Mfano ni eneo la Urithi wa Ulimwengu la Kahuzi-Biega katika Zaire ya kale inayoitwa sasa Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo. Kufuatia vita vya hivi juzi vya Rwanda kambi ya watu 50,000 ilijengwa kwenye mipaka ya mbuga, ambapo ni makao ya sokwe adimu wa milimani na aliye hatarini aliyefanyiwa utafiti na wanasayansi, George Schaller, marehemu Profesa Grzzimek na Diane Fossey. Kutokana na juhudi za UNESCO, mkuu wa umoja wa mataifa anayehusiaka na maswala ya wakimbizi, mamlaka ya nchi, Shiriko la Msaada la Ujerumani la GTZ, na kwa msaada wa kipesa wa Hazina ya Urithi wa Ulimwengu, kambi hii ya wakimbizi ilihamishwa mahali pengine mwafaka.



*Sokwe wa milimani aliye hatarini, Mbuga ya Kitaifa Ya Bwindi, Rwanda. © UNESCO*

© UNESCO 2004

# Urithi wa Ulimwengu na haki za binadamu

Mapambano ya wanadamu kuhusu kutambuliwa na kuheshimiwa kwa haki za binadamu mara nyingine huandamana na vitendo vya amani, uhuru na maendeleo. Na mara nyingi, kihistoria imekuwa ikihusishwa na kanuni za demokrasia na ushirikishi wa watu katika utawala.

Maeneo mengi ya Urithi wa Ulimwengu hujumuisha mawazo haya ingawaje yanaweza kuelezwa kwa njia tofauti, mara nyingine kwa njia ambazo haziwezi kueleweka kwa urahisi. Mifano ifuatayo inafafanua kauli hii.

Kisiwa cha Gorée nje ya pwani ya Senegal, kinaangaliana na mji mkuu wa Dakar. Katika karne ya kumi na tano hadi ya kumi na tisa kituo kikubwa kabisa cha biashara ya utumwa, katika pwani ya Afrika kilikuwa Goree. Kilitawaliwa wakati tofauti na Wareno, Waholanzi, Waingereza na Wafaransa. Usanifu wa mijengo yake unamulika tofauti baina ya makao ya watumwa yanayohuzunisha, na nyumba za kupendeza za wafanyi biashara za watumwa. Kwa sasa mahali hapo ni kumbukumbu ya unyonyaji wa binadamu na mahali maalum pa mapatanisho.

Kumbukumbu nyingine yenye kutia uchungu kuhusu haki za binadamu na kuteseka kusikoelezeka kulikofanyiwa mamilioni ya watu ambao hawakuwa na hatia ni kambi ya kizuizi ya Auschwitz huko Poland, iliyoandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu mwaka wa1979. Kuta zake za kingome, sengenge, majukwaa, makao ya majeshi, viunzi vya kunyongea watu na zaidi ya haya vyumba vya gesi na majiko ya kuchomea watu zinatoa ushuhuda kuhusu hali ambazo wakati wa vita vya pili vya dunia waNazi walivyowaua watu milioni 1.5, wakiwemo watoto, wakongwe wa mataifa ishirini na nne, wengi wao wakiwa wa asili ya kiyahudi katika eneo hilo. Eneo hili linawakilisha kipindi cha historia ya mwanadamu kinachostahili kukumbukwa ili kuepuka ukatili zaidi baadaye. Unaonyesha matokeo mabaya ya chuki ya kitaifa.


Katika eneo hili, wageni wanaweza kujionea makavazi ya kitaifa ya Auschwitz yaliyo na seli za gerezani, chemba za gesi na oveni za kuchomea watu. Makavazi haya yanatumika kama taasisi ya kihistoria na utafiti ulio na nyaraka za kipekee. Inachangia sana mapambano yanayoendelea ya amani ya ulimwengu wote na usalama kwa kuwa kila mwaka Auschwitz hutembelewa na maelfu ya watu hata madarasa mazima ya shule kutoka maeneo tofauti ya ulimwengu.



*Kizuizi cha Auschwitz, Poland.*
*© UNESCO / A. Husarska*



UNESCO 2004



## Harakati za wanafunzi za 41

## UBAGUZI—TISHO KWA AMANI

### Lengo: Kuangamiza kutovumuliana na kuendeleza kujifunza kuhusu tamaduni za kimataifa na kuheshimu mazingira ya ulimwengu


Majadiliano


Harakati darasani


Harakati nje ya darasa


Vipindi kadhaa



Historia, masomo ya utawala, lugha, fasihi


Vitabu vya historia, ensaikilopidia

✓Waulize wanafunzi kueleza hisia zao juu ya matukio makuu ya kihistoria (k.m. vita vya kwanza na vya pili vya ulimwengu) ambavyo vilichochea chuki, kutoelewana na ubaguzi, na haja ya kuhakikisha siku za baadaye za amani, kwa kuandika insha, mashairi, uchoraji, mabango, utungaji wa nyimbo au muziki.

✓Waulize wahusishe kujieleza kwao na yale ambayo wamejifunza hadi sasa kuhusu Urithi wa Ulimwengu. Je kujifunza kuhusu tamaduni zingine na desturi tofauti za maisha, na kujifunza kuhusu maeneo ya urithi, kunasaidia kuelewa kikweli na kudhamini na kuheshimu watu wengine na mazingira ya ulimwengu?

Uhuru kama thamani ya kimsingi ndiyo ujumbe wa maeneo kadhaa ya Urithi wa Ulimwengu, kwa mfano, Mnara wa Haki (Statue of Liberty) na Ukumbi wa Uhuru (Independence Hall) yote ambayo yako marekani. Ukumbi wa Haki uliingizwa kwenye orodha ya urithi mnamo mwaka wa 1984, umesimama kwenye mlango wa Bandari ya New York na umekaribisha wahamiaji wengi wa nchi hii tangu 1886 ulipozinduliwa. Mnara huu wa kumbukumbu una urefu wa sehemu za chuma wa mita 46 na ulibuniwa Paris na mchongaji wa Kifaransa Frédéric-Agusute Bartoldi, aliyesaidia katika ujenzi wa sehemu za vyuma na Gustave Eiffel (aliyetengeneza mnara wa Eiffel, Paris, Ufaransa). Ishara ya haki inawakilisha utumiaji wa kiufundi wa hali ya juu sana wa karne ya kumi na tisa. Kwa kuwa mnara huu, ambao pesa za kuujenga zilitokana na mchango wa kitaifa, ulibuniwa Uropa, na mchongaji mfaransa unatiliwa nguvu thamani ya kiishara ya eneo hili la urithi kama lenye kueleza mabadilishano ya sifa tofauti za kitamaduni.



*Independe*
*Marekan*
*© UNES*

Independence Hall ilio katikati ya mji wa Philadelphia, Pennsylvania, ni mahali ambapo Utangazaji wa Uhuru na Katiba ya Marekani zilipotiwa sahihi (uhuru 1776 na katiba 1787). Tangu wakati huo kanuni hizi za kidemokrasia zinazoendelezwa katika hati hizi za umuhimu mkubwa kwa Marekani na historia ya ulimwengu zimechochea wanasheria katika maeneo mengi ya ulimwengu. Eneo hili liliandikishwa kwenye orodha ya urithi mnamo 1979.

■ **Harakati za wanafunzi za 42**



## BUNI FUMBO KUHUSU URITHI WA ULIMWENGU NA AMANI

### Lengo: kutilia mkazo kwenye fikira za wanafunzi uhusiano uliopo baina ya uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu na amani



Mazoezi



Kipindi kimoja au viwili



Elimu kuhusu utawala



Ramani ya Urithi wa Ulimwengu




Ukurasa wa harakati za ulimwengu, buni mchezo-fumbo wa Urithi wa Ulimwengu na amani, kamusi, ensaiklopidia

✓Waulize wanafunzi wako watengeze orodha mbili, moja ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na nyingine ya dhana au maneno yanayohusishwa na amani. [k.m. visawe vya amani: mapatano ya kusimamisha vita kwa muda, makubaliano ya kusimamisha vita kwa muda (ili kuondoa majeruhi): upatanifu, itifaki, urafiki, shwari, kimya, utulivu, maneno yanayohusiana: isiyo-chokozi, isiyo-na ukali/nguvu na kinyumume cha amani: vita, uchokozi, mzozo wa kisilaha, uhasama, vita mapambano.

✓Baadaye waulize wabuni mchezo-fumbo wao kwa kutumia majina ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na maneno kutoka orodha yao.
Tumia ukurasa ufuatao wa harakati za wanafunzi kama mfano.

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | e | | | | | | |
| a | | | | c | | | | | | |
| r | | t | | n | | | | | | |
| g | o | r | e | e | | | | | | |
| a | | o | | d | e | f | e | n | c | e |
| | | f | | n | | | | a | | c |
| | | | | e | | | | i | | a |
| | | l | | p | | | | r | | e |
| p | e | a | c | e | | | | d | | p |
| | | h | | d | | | | a | | |
| | | a | | n | | | | h | | |
| | | m | | i | | | | | | |
| | | | | | | | | | | |
| | | j | | | | | | | | |
| p | e | a | c | e | | | | | | |
| | | t | | | | | | | | |



# Kupitia kwa mitaala: Urithi wa Ulimwengu na utamaduni wa amani

## Sanaa
Chagua eneo la ulimwengu linalohusiana na amani au ujumi.
Tengeneza mabango yaliyo na ujumbe maalum unaokuza amani na uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu.

## Lugha za kigeni
Tafsiri maneno ya amani na urithi katika lugha zingine ambazo wanafunzi wanazifahamu na utayarishe orodha (k.m., paix na patrimoine kwa Kifaransa, paz na patrimonio kwa Kihispania).
Tafiti zaidi, wakati wa kujifunza lugha za kigeni, maeneo ya urithi yanayohusiana na amani.

## Jiografia
Soma magazeti ya kila siku na ukate makala kuhusu mizozo na migorogoro inayotokea katika sehemu tofauti za ulimwengu na jinsi inavyoweza kuhatarisha Urithi wa Ulimwengu.

Linganisha na wasilisha makaratasi hayo baada ya mwezi mmoja kulingana na maeneo ya kijiografia (k.m., Afrika, mataifa ya Kiarabu, Bara Hindi, Pasifik, Uropa, Marekani ya Kaskazini, Marekani ya Kusini na Karibea).

Tambua eneo lolote la Urithi wa Ulimwengu karibu na maeneo ya mzozo na mjadiliane iwapo yapo kwenye hatari ya kuharibiwa au kuangamizwa.

## Historia
Tambua eneo linalohusiana au linaloashiria amani (katika nchi yako au kwengineko duniani) ambalo bado haliko kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Jadilianeni umuhimu wake wa kihistoria na uonyeshe eneo lenyewe lilipo sasa na litakapokuwa (Kihistoria) katika siku za baadaye.

## Lugha
Tengeneza orodha ya visawe vya amani kisha uchague kisawe kimoja na uandike aya moja juu yake kuhusiana na Urithi wa Ulimwengu.

## Hesabu
Chagua eneo la ulimwengu kama vile Kisiwa cha Gorée kilicho Senegal na utafiti kwa mfano, kuhusu idadi ya wafungwa ambao walitoka kisiwa hicho kwa meli wakielekea bara za Amerika, wasilisha data hii katika chati kulingana na miongo au karne. Jadili matokeo.



©UNESCO 2004

# Marejeleo





**Tunahitaji vifaa vya kielimu vya kusisimua na mwafaka ili vitusaidie kuelewa umuhimu wa urithi. Watu wachanga wastahili kushiriki katika utayarishi wa vifaa hivy.**

**Ahadi yetu, Muungano wa Kitaifa wa Kwanza wa Vijana, Bergen, Norway**

# Marejeleo

| | Ukurasa |
|---|---|
| **Istihali** | **165** |
| **Anwani** | **169** |
| Makao Makuu ya UNESCO | 169 |
| Ofisi za UNESCO | 171 |
| Mashirika muhimu | 172 |
| **Orodha ya Marejeleo** | **175** |
| Vifaa vya UNESCO vya *bure* | 175 |
| Vifaa vya UNESCO vya kulipiwa | 176 |
| Vifaa vingine vya kulipiwa | 177 |
| **Orodha ya anwani** | **178** |



# Istihali

### Mradi wa Shirikisho la Mashule (ASPnet)

Ulianzishwa na UNESCO mnamo mwaka wa 1953 ukiwa na lengo la kuyahamisha mashule kote ulimwenguni ziimarishe ya elimu katika kuendeleza utamaduni wa amani, kuvumiliana na uelewano wa kimataifa. Katika miongo mitano iliyopita zaidi ya shule 7, 000 kote ulimwenguni zimejiunga na mradi wa ASPnet katika kukuza mitazamo mipya ya elimu na vifaa vya kuendeleza lengo lililotajwa

### Bayo-anuwai

Inarejelea aina tofauti za viumbe na inahusisha mimea tofauti ya dunia, wanyama, viumbe na viji-umbe (micro-organisms), jeni zao na mifumo ikolojia ambayo wao ni sehemu yake.

### Uhifadhi

Unarejelea utaratibu wa kutunza eneo ili kudumisha thamani zake maalum. Uhifadhi unaweza kuhusisha utengenezaji, utunzaji, urejeshaji katika hali ya awali, na ukarabati.

### Kigezo (vigezo, wingi)

Vinatumiwa kuchagua maeneo yenye thamani kubwa ya kidunia ili yaingizwe kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu.

### Utamaduni wa amani

Ni dhana inayotumika katika taaluma tofauti ambayo inahusisha harakati za UNESCO za kuendeleza uzingatiaji wa desturi ambazo ziko katika kiini cha moyo wa amani.

### Urithi wa kitamaduni

Unaelezwa katika *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* kama majengo ya kumbukumbu na maeneo.

### Mandhari ya ardhi ya kitamaduni

Huonyesha mwingiliano baina ya watu na mazingira ya kiasilia.

### Kongamano Kuu la UNESCO

Wanachama wote wa UNESCO hukutana baada ya kila miaka miwili kuidhinisha utaratibu na bajeti ya shirika.

## ICCROM
Ni makao ya kimataifa ya uchunguzi wa utunzaji na urejeshaji katika hali ya awali wa mali tamaduni (International Centre for the Preservation and Restoration of Cultural Proper). ICCROM hutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu njia za kuhifadhi maeneo ya urithi wa kitamaduni na hupanga kozi za mbinu za kukarabati.

## ICOM
Ni baraza la kimataifa la makavazi (International Council of Museums). ICOM hutangaza na kukuza makavazi na taaluma ya maakava kote ulimwenguni.

## ICOMOS
Ni baraza la kimataifa la majengo na maeneo ya kumbukumbu (International Council of Munuments and Sites). ICOMOS huandaa utathmini wa kiufundi juu ya maeneo ya kitamaduni na mandhari ardhi za kitamaduni kwa ajili ya kuandikishwa katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu.

## IUCN
Ni umoja wa uhifadhi wa ulimwengu (The World Conservation Union). IUCN hushauri kamati ya Urithi wa Ulimwengu kuhusu uteuzi wa maeneo ya kiasilia kwa ajili ya kuandikishwa katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu.

## Orodha ya meaneo ya urithi yaliyo hatarini
Yanahusisha maeneo ya Urithi wa Ulimwengu ambayo kamati ya urithi wa ulimwengu imeamua kuwa yanakabiliwa na tisho kiasi ya kwamba yanahitaji hatua za pamoja za jumuiya ya kimataifa ili kuyahifadhi.



## Mataifa wanachama
Mataifa ambayo ni wanachama wa UNESCO hujulikana kama mataifa wanachama.

## Urithi wa kiasilia
Huelezwa katika *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu* kama miundo ya kiasilia kifisiografia na maeneo ya kiasilia.

## Uteuzi
Ni utaratibu ambao taifa mwanachama wa *Mapatano* hufuata iwapo taifa hilo linataka eneo fulani kuingizwa kwenye Orodha la Urithi wa Ulimwengu. Fomu maalum ya uteuzi lazima ijazwe kikamilifu na kutumiwa makao makuu ya Urithi wa Ulimwengu ya UNESCO.

## Thamani ya juu ya kiulimwengu
Kusema kuwa eneo fulani lina thamani ya juu ya kiulimwengu (outstanding universal value) inamaanisha kutoweka kwake kutakuwa hasara isiyoweza kufidiwa kwa watu wote wa ulimwengu. Thamani ya juu ya ulimwengu inaweza kuelezwa kisahili kama thamani ya Urithi wa Ulimwengu.

## Patrimonito
Ni muhusika anayeashiria mtu mchanga anayelinda urithi. Ilibuniwa na washiriki wa Muungano wa Urithi wa Kwanza wa Vijana huko Bergen, Norway, 1995.

IESCO 2004

## Taifa husika

Ni mataifa ambayo yamezingatia *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu*. Kwa hivyo yanakubali kutambua na kuteua maeneo katika mataifa yao kuandikishwa katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu. Wakati serikali husika inapoteuwa eneo, inaeleza jinsi eneo linavolindwa na mpango wa usimamizi wa kulihifadhi. Mataifa husika pia yanatarajiwa kulinda thamani ya maeneo ya urithi yaliyoandikishwa na yanahimizwa kuripoti mara kwa mara kwa UNESCO kuhusu maeneo hayo. Taifa husika hukutana mara moja kila baada ya miaka miwili katika kikao cha kawaida cha kongamano kuu la UNESCO katika Bunge kuu la mataifa wanachama. Katika bunge kuu mataifa husika huchagua kamati ya Urithi wa Ulimwengu, na kuchunguza taarifa za hesabu za Hazina ya Urithi wa Ulimwengu na kuamua juu ya sera za muhimu.

## Orodha ya muda

Kila nchi ambayo ni taifa husika wa *Mapatano* huombwa kubuni orodha ya muda, inayotaja maeneo ya kitamaduni na kiasilia ambayo inanuia kuyateua kuandikishwa katika Orodha ya Urithi wa Ulimwengu katika miaka mitano au kumi ijayo.

## Umoja wa Mataifa (UN)

Ni shirika la kimataifa ambalo lina mataifa wanachama 189 (hesabu ya 2001). Shirika hili lilianzishwa baada ya vita vya pili vya dunia ili kudumisha amani na usalama wa kimataifa, kuendeleza uhusiano wa kirafiki baina ya mataifa na kuendeleza maendeleo ya kijamii, hali ya kufana ya maisha, na haki za binadamu.

## UNESCO—Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni

Ni wakala maalum wa Umoja wa Mataifa ulio na mataifa wanachama 190 (hesabu ya 2003). Lengo la UNESCO ni kujenga ulinzi wa amani katika fikra za wanaume na wanawake kupitia kwa ushirikiano wa kimataifa wa kiusomi.

## Makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu

Yanahusika na kutekeleza maamuzi ya Kamati ya Urithi wa Ulimwengu.

## Mradi wa Elimu wa UNESCO wa watu wachanga juu ya Urithi wa Ulimwengu

Ni mradi wa kimaeneo ambao unaratibiwa na makao ya UNESCO ya Urithi wa Ulimwengu na Sekta ya Elimu ya ASPnet (UNESCO Wrld Heritage Centre and Eduction Sector ASPNet Coordination Unit) inayohusika na uratibu ikiwa na lengo la kuanzisha elimu ya Urithi wa Ulimwengu ili kuhakikisha ufahamu wa thamani ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu na uhifadhi.

## Urithi wa Ulimwengu

Urithi wa kitamaduni na kiasilia wa thamani kuu ya ulimwengu yaliyoandikishwa kwenye Orodha ya Urithi wa Ulimwengu.

## Ofisi ya Urithi wa Ulimwengu

Ofisi hii inahusisha mataifa saba wanachama wa Kamati ya Urithi wa Ulimwengu na hukutana mara mbili kwa mwaka kutayarisha kazi ya kamati.



© UNESCO 2004

## Kamati ya Urithi wa Ulimwengu

Kamati ya kiserikali ya wanachama ishirini na moja inahusika na kutekeleza *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu.*

## *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu*

*Mapatano Yanayohusu Ulinzi wa Urithi wa Ulimwengu wa Kitamaduni na Kiasilia (The Convention Concerning the Protection of the World Cutlrual and Natural Heritage)* ulikubaliwa na kikao cha kumi na sita cha Kongamano Kuu la UNESCO mwaka 1972. Lengo la *Mapatano* haya ni kulinda, kuhifadhi, kudumisha na kupitishia vizazi vijavyo thamani za kidunia za hali ya juu za Urithi wa kitamaduni na kiasilia.

## Hazina ya Urithi wa Ulimwengu

Imebuniwa na michango ya kujitolea na ya lazima na hutumika katika uhifadhi wa maeneo ya Urithi wa Ulimwengu

## Orodha ya Urithi wa Ulimwengu


Orodha ya maeneo ya kitamaduni, kiasilia na yenye sifa zote mbili (pamoja na mandhari ya kiasilia) yanayochukuliwa kuwa na thamani kuu ya kiulimwengu.

## Muungano wa Vijana juu ya Urithi wa Ulimwengu

Mikutano kumi ya muungano wa vijana juu ya Urithi wa Ulimwengu ishafanywa: Dubrovnik, Kroatia, 1996; Victorial Falls, Zimbabwe, 1996; Beijing, Uchina, 1997; Osaka, Japan, 1998; Kisiwa cha Gorée, Senegal, 1999: Ifrane, Morocco, 1999; Cairns, Australia, 2000; Lima, Peru, 2001; Karlskrona, Uwidi, 2001; Bratislava, Slovakia, 2002; Velikiy Novgorod, Urusi, 2002; Oman, Jordan, 2002; Rhodes, Ugiriki, 2003. Malengo ya muungano wa vijana ni kuendeleza uelewano baina ya tamaduni na ziara za kubadilishana miongoni mwa watu wachanga, na kuendeleza ufahamu kuhusu umuhimu wa *Mapatano ya Urithi wa Ulimwengu*, na kukuza mipango ya vitendo vya kimaeneo na vya kitaifa vya kuwahusisha katika uhifadhi wa Urithi wa Ulimwengu.



© UNESCO 2004



# Anwani

## ■ Makao Makuu ya UNESCO

### *UNESCO Headquarters*

7 place de Fontenoy
75352 Paris 07 SP
France
Simu: (33 1) 45 68 10 00
Kipepesi: (33 1) 45 67 16 90
http://www.unesco.org

### *Makao ya Urithi wa Ulimwengu*

Makao Makuu ya UNESCO
Simu: (33 1) 45 68 15 71
(33 1) 45 68 18 76
Kipepesi: (33 1) 45 68 55 70
Barua pepe: wh-info@unesco.org
http://www.unesco.org/whc
www.unesco.org/whc/education

### *Mradi wa Shirikisho la Mashule (ASPnet)*

Sekta ya Elimu
Makao Makuu ya UNESCO
Kipepesi: (33 1) 45 68 56 39
Barua pepe: aspnet@unesco.org
http://www.unesco.org/education/asp

### *Kitengo cha Urithi wa Kitamaduni cha UNESCO*

Kitengo cha utamaduni hasa kinahusika katika usimamizi wa kampeini za kitaifa, nyingi ambazo zinahusu mali za Urithi wa Ulimwengu. Pia inatekeleza miradi inayoendelezwa katika ushirikiano na makao ya Urithi wa Ulimwengu, ICCROM na ICOMOS.

### *Kitengo cha Urithi wa Utamaduni*

Sekta ya Utamaduni
1 rue Miollis
75732 Paris Cedex 15
France
Simu: (33 1) 45 68 37 56
Kipepesi: (33 1) 45 68 55 96



© UNESCO 2004

### *Sehemu ya Viwango vya Kimataifa*

Husimamia utekelezi wa *Mapatano ya Hague ya 1954 (Mapatano kuhusu ulinzi wa mali-tamaduni wakati wa mzozo wa kisilaha)* na *Mapatano ya 1970 ya kukataza na kuzuia uingizaji katika mataifa ya nje na pia ubadilishaji wa umilki wa mali-tamaduni (Convention on the Means of Prohibiting and Preventing the Illicit Import, Export and Transfer of Ownership of Cultural Property).*

International Standards Section
Kitengo cha Urithi wa Kitamaduni, Sekta ya Utamaduni
Makao makuu ya UNESCO

### *Sekta ya Sayansi, UNESCO*

Na Kitengo chake cha Sayansi ya Ikolojia, Kitengo cha Sayansi za Dunia, na Ofisi ya Uratibu wa *Mipango ya Kimazingira*, hushirikiana na makao ya Urithi wa Ulimwegu na IUCN kutekeleza miradi inayohusu mali ya kiasilia ya Urithi wa Ulimwengu, hasa kwa maeneo yaliyotengwa ka Biosphere Reserves.

Kitengo cha Sayansi za Kiekolojia
Sekta ya Sayansi
1 rue Miollis
75732 Paris Cedex 15
France
Simu: (33 1) 45 68 40 67
Kipepesi: (33 1) 45 68 58 04



Man and the Biosphere Programme:
Barua pepe: mab@unesco.org
http://www.unesco.org/mab

### *Mpango wa Utamaduni na Amani*

Ni dhana ya *taaluma nyingi* ambayo inaleta pamoja harakati ambazo UNESCO huendeleza kuhimiza kuzingatia thamani ambazo ni kiini cha amani.

Uratibu wa Utamaduni wa Amani
Makao Makuu ya UNESCO
Simu: (33 1) 45 68 12 20
Kipepesi: (33 1) 45 68 55 57
Barua pepe: cp@unesco.org
http://www.unesco.org/cp

### *Ofisi ya Uchapishaji wa UNESCO (UPO/D)*

Makao Makuu ya UNESCO
Simu: (33 1) 45 68 46 25
Kipepesi: (33 1) 45 68 57 39
http://upo.unesco.org

· UNESCO 2004

## OFISI ZA UNESCO

### *UNESCO Dakar*
12 Avenue Roume, BP 3311, Dakar, Senegal
Simu: (221) 8492323
Kipepesi: (221) 8238393
Barua pepe: Dakar@unesco.org

### *UNESCO Santiago*
Calle Enrique Delpiano 2058, Casilla 3187, Santiago, Chile
Simu: (56 2) 6551050
Kipepesi: (56 2) 6551046
Barua pepe: uhst@unesco.org

### *UNESCO Bangkok*
Sanduku la Posta ya Prakanong, 967, Bangkok, 10110, Thailand
Simu: (662) 0879/0577/0550
Kipepesi: (662) 391 0866
Barua pepe: Bangkok@unesco.org

### *UNESCO Amman*
Sanduku la Posta 2270, Wadi Saqra, Amman 11181, Jordan
Simu: (962 6) 5514234/6559
Kipepesi: (962 6) 5532183
Barua pepe: amman@unesco.org

### *UNESCO Apia*
Sanduku la Posta 5766
Matautu, UTA Post Office, Apia, Samoa
Simu: (685) 24 276
Kipepesi: (685) 22 253
Barua pepe: unesco.apia@unesco.org

### *UNESCO Harare*
Sanduku la Posta HG 435, Highlands, Harare, Zimbabwe
Simu: (263 4) 77 6114/15
Kipepesi: (263 4) 77 60 55
Barua pepe: harare@unesco.org

### *UNESCO San José*
Ap. Postal 220, San Francisco 2120, San José, Costa Rica
Simu: (506) 296 37 81/220 44 00
Kipepesi: (506) 231 22 02
Barua pepe: san-jose@unesco.org

### *UNESCO Doha*
Sanduku la Posta 3945, Doha, Qatar
Simu: (974) 86 77 07/77 08
Kipepesi: (974) 86 76 44
Barua pepe: doha@unesco.org

# ■ MASHIRIKA MUHIMU

### *Makao ya Kimataifa ya Uchunguzi wa Uhifadhi na Ujengaji Upya wa Mali-asilia*

International Centre for the Study of the Preservation and Restoration of Cutltural Property (ICCROM)
Via di San Michele 13
I-00153 Rome
Italia
Simu: (396) 585 531
Kipepesi: (396) 585 533 49
Barua pepe: iccrom@iccrom.org
http://www.icomos.org/iccrom

### *Baraza la Kimataifa juu ya Kumbukumbu na Maeneo ya Urithi wa Ulimwengu*

International Council on Monuments and Sites (ICOMOS)
49-51 rue de la Fédération
75015 Paris
Ufaransa
Simu: (33 1) 45 67 67 70
Kipepesi: (33 1) 45 66 06 22
Barua pepe: secretariat@icomos.org
http://www.icomos.org



### *Umoja wa Kimtaifa wa Uhifadhi*

World Conservation Union (IUCN)
Rue Mauvernye 28
CH-1196 Gland
Switzerland
Simu: (41) 22 999 0001
Kipepesi: (41) 22 999 0010
Barua pepe: mail@iucn.org
http://www.iucn.org

### *Baraza kuu la Makavazi*

International Council of Museums (ICOM)
1 rue Miollis
75732 Paris Cedex 15
France
Simu: (33 1) 47 34 05 00
Kipepesi: (33 1) 43 06 78 62
Barua pepe: secretariat@icom.org
http://www.icom.org

© UNESCO 2004

### *Ofisi ya Urithi wa Ulimwengu ya Nordic*

Nordic World Heritage Office (NHWO)
Sanduku la Posta 8196 Dep.
N-0034 Oslo
Norway
Simu: (47) 22 94 05 80
Kipepesi: (47) 22 94 05 81
Barua pepe: nwho@ra.no
http://www.grida.no/ext/nwho/index.htm

### *Muungano wa Majiji ya Urithi wa Ulimwengu*

Organization of the World Heritiage Cities (WHC)
56 Rue Saint-Pierre
Quebec G1k 4A1
Canada
Simu: (1) 418 692 0000
Kipepesi: (1) 418 692 5558
Barua pepe: secretariat@ovpm.org
http://www.ovpm.org

### *Makao ya UNEP ya Ulimwengu ya Kuchunguza Uhifadhi*

UNEP World Conservation Monitoring Centre (UNEP WCMC)
219 Huntingdon Road
Cambridge CB3 0DL
United Kingdom
Simu: (44) 1223 277 314
Kipepesi: (44) 1223 277 136
Barua pepe: info@unep-wcmc.org
http://www.unep-wcmc.org

### *Shirika la Ulimwengu la Utalii*

World Tourism Organization (WTO)
Capitán Haya 42
28020 Madrid
Uhispania
Simu: (34 91) 567 81 00
Kipepesi: (34 91) 571 37 33
Barua pepe: omt@world-tourism.org
http://www.world-tourism.org

**Kumbuka:** Habari hii inaweza kubadilika. Tafadhali pata ushauri wa Makao Makuu ya UNESCO kuhusu anwani za sasa.



© UNESCO 2004



# Orodha ya Marejeleo

## ■ Vifaa vya UNESCO vya bure*

***Ramani ya Urithi wa Ulimwengu*** (bango la kukunjwa)
Inapatikana katika Kiingereza, Kifaransa na Kihispania

***Orodha ya Urithi wa Ulimwengu***
Inapatikana katika Kiingereza na Kifaransa

***Maelezo mafupi ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu***
Yanapatikana katika Kiingereza na Kifaransa

***Urithi wa Ulimwengu (Kurasa za habari)***
Zinapatikana katika Kiingereza, Kifaransa na Kihispania

***Urithi wa Ulimwengu 2002 (Brosha ya habari iliyo katika rangi tofauti)***
Inapatikana katika Kiingereza, Kifaransa, pia Kihispania

***Mapatano kuhusu Ulinzi wa Urithi wa Ulimwengu wa Kitamaduni na Kiasilia***
Paris, UNESCO, 1972
Yanapatikana katika Kiingereza, Kifaransa, Kihispania, Kirusi na Kiarabu

***Mwongozo tendaji wa Utekelezaji wa mapatano ya Urithi wa Ulimwengu***
Yanapatikana katika Kiingereza na Kifaransa

***Barua ya habari za Urithi wa Ulimwengu (hutolewa mara mbili kila mwezi)***
Habari kuhusu uundaji wa sera na maswala yanayokabili urithi wa ulimwengu. Inapatikana katika Kiingereza na Kifaransa

***Brosha ya Kielimu ya Urithi wa Ulimwengu***
Barua ya kurasa nne inayoeleza elimu ya Urithi wa Ulimwengu na ASPnet. Inapatikana katika Kiingereza na Kifaransa

***Ukurasa wa utambulishi wa ASPnet***
Barua fupi inayoeleza ASPnet kifupi

***Maneno muhimu ya kushiriki katika mradi wa Shirikisho la Mashule wa UNESCO (ASPnet)***
Mwongozo unaoeleza shughuli za ASPnet

### *Patrimonio de la Humanidad*

Ensaiklopidia katika juzuu kumi na mbili
Inapatikana katika Kihispania

### *World Heritage*

Ensaiklopidia katika majuzuu kumi na mawili
Verlagshaus Stuttgart/Plaza y Janes/UNESCO
Stuttgart/Paris, 1996/1997
Inapatikana katika Kijerumani

### *Schätze der Menschheit*

Frederking & Thaler/UNESCO, München/Paris, 1996/1997
Inapatikana katika Kijerumani

### *The World Heritage*

Ensaiklopidia katika majuzuu kumi na mawili
Kodansha/UNESDCO, Tokyo/Paris, 1996/1997
Inapatikana katika Kijapani

### *Our Creative Diversity: Report of the World Commission on Culture and Development*

Paris, UNESCO, 1995Available in Spanish

### Majarida

### *The World Heritage Review|*

Makala ya mara mbili kwa mwezi ya makala yenye undani juu ya maeneo ya Urithi wa Ulimwengu ya kitamaduni na kiasilia.
Inapatikana katika Kiingereza, Kifaransa na Kihispania

## ■ Vifaa vingine vya kulipiwa

### *Masterworks of Man and Nature*

Patonga, Australia, Harper-MacRae Publishing, 1992
ISBN: 0-646-05376-0
Inapatikana katika Kiingereza
Anwani ya kuagiza: IUCN, rue Mauverney 28, 1196 Gland, Switzerland

### *Paradise on Earth*

Patonga, Australia, JIDD Publishers, 1995
ISBN: 0-646-19397-X
Inapatikana katika Kiingereza
Anwani ya kuagiza: IUCN, rue Mauverney 28, 1196 Gland, Switzerland

***Wolrd Heritage Twenty Years Later***

Gland, Switzerland, IUCN, 1992

ISBN: 2-8317-0109-0

Inapatikana katika Kiingereza

Anwani ya kuagiza: IUCN, rue Mauverney 28, 1196 Gland, SwitzerlandGland,

Ili kuagiza chapisho zilizotajwa tazama http://www.iucn.org/bookstore

***World Cultural and Natural Propert***

A series for young people

Tokyo, Gakken, 1994

Inapatikana katika Kijapani

# ■ Orodha ya anwani

*Kwa vifaa vya UNESCO vya bure, wasiliana na:
UNESCO World Heritage Centre
7, place de Fontenoy, 75352 Paris 07 SP, France
Kipepesi: (33 1) 01 45 68 55 70
Barua pepe: wh-info@unesco.org

Mradi wa Ushirikisho wa Mashule (ASPnet)
Sekta ya Elimu
UNESCO, 7, place de Fontenoy, 75352 Paris 07 SP, France
Kipepesi: (33 1) 01 45 68 56 39
Barua pepe: aspnet@unesco.org

**Kwa vifaa vya UNESCO vya kulipiwa, wasiliana na:
Ofisi ya Uchapishaji ya UNESCO
1, rue Miollis, 75732 Paris Cedex 15, France
Kipepesi: (33 1) 45 68 57 41
Barua pepe: c.laje@unesco.org

**Habari kuhusu Urithi wa Ulimwengu na ASPnet pia zinaweza kupatikana kupitia kwa 'server' ya UNESCO :**

**World Heritage Centre**
**http://www.unesco.org/whc**

**Mradi wa Shirikisho za Mashule (ASPnet)**
**http://www.unesco.org/education/asp**